**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |

| | |
|---|---|
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Nne – Tarehe 26 Januari, 2015**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Mwenyekiti: (Mahmoud Muhammed Mussa) Alisoma Dua.*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako napenda kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo endelevu nam 2 ya mwaka 1996 na kuweka badala yake Masharti bora ya kuhifadhi, Kulinda na Kusimamia Mazingira Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo, kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya pili.

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Nam. 2 ya mwaka 1996 kwa ajili ya maendeleo endelevu na kuweka badala yake masharti bora ya kuhifadhi, kulinda na kusimamia mazingira Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo, naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

**Nam. 73**

### Hifadhi ya Mazingira kwa Visiwa Vidogo Vidogo

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad –** Aliuliza**:-**

Kwa kuwa suala la uharibifu wa mazingira bado limekuwa kubwa hususan katika maeneo ya bahari kutokana na watu kukata mikoko kwa wingi na hivyo kufanya maji chumvi kuingia katika maeneo ya kilimo na makaazi kama vile Kisiwa Panza.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuyanusuru mazingira hayo ili kuokoa visiwa vidogo vidogo kama hivyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais –** Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi napenda kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ukataji wa miti ya mikoko husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na hivyo kufanya maji ya bahari kuingia katika maeneo ya kilimo na makaazi kama vile Kisiwa Panza na maeneo mengine ya Unguja na Pemba.

Pia naomba ifahamike kuwa mbali na ukataji wa mikoko, uchukuaji wa mchanga kutoka kwenye fukwe, ukataji wa mawe pembezoni mwa bahari na uharibifu wa matumbawe na miamba ya baharini ni mambo ambayo yanachangia katika kuongeza kasi ya maji ya bahari kuingia katika maeneo ya kilimo na makaazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 73 kama ifuatavyo:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatarajia kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabia nchi katika maeneo zalishi *productive areas* ya ukanda wa Pwani wa Tanzania utakaohusisha maeneo ya Bagamoyo, Pangani, Rufiji na Zanzibar. Eneo la Kisiwa Panza ni miongoni mwa maeneo ya Zanzibar yanayotegemewa kuwemo kwenye mradi huu. Wataalamu wa Mradi wameshakuja Zanzibar kwa ajili ya kukagua maeneo ya Mradi ambayo ni Kisiwa Panza, Tumbe na Ukele kwa upande wa Pemba na upande wa Unguja ni Kilimani na Bwawani. Hivi sasa wataalamu hao

wako katika hatua ya kutayarisha gharama zinazohitajika ili kuweza kufahamu upeo wa mradi kwenye maeneo hayo, hatua ambayo inaweza kupelekea maeneo mengine kuachwa endapo mahitaji ya fedha yatakuwa makubwa kupita uwezo wa mradi. Zanzibar imekadiriwa kupata kiasi cha Dola za Kimarekeni 361,300 kwenye mradi huo.

Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hivi karibuni kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na wananchi wa maeneo husika inaendelea na upandaji wa mikoko jumla ya hekta 50 katika maeneo ya Ndagoni, Furaha na Wambaa kwa upande wa Pemba; na Bumbwini Makoba, Kiongwe Kidogo na Kisakasaka kwa Unguja. Upandaji huo wa mikoko ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhifadhi mazingira ya maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kupunguza maji ya bahari kuingia kwenye maeneo ya kilimo na makaazi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana pia na wananchi wa maeneo husika imeweza kujenga matuta kwa baadhi ya maeneo ya kilimo yanayoingia maji ya bahari, baadhi ya maeneo hayo ni Tumbe Magharibi, Ukele, Sizini, Mziwanda, Gando, Nduuni, Chokaani na Kengeja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa maeneo yaliyoingia maji ya bahari ni mengi, ni wazi kuwa sio rahisi kwa Serikali kuyashughulikia kwa pamoja, hivyo Serikali inaendelea na hatua za kuhamasisha nyenzo ili kuendelea kuchukua hatua za kuyalinda maeneo hayo hatua kwa hatua. Pamoja na hatua hizo zinazochukuliwa na Serikali, naomba nitoe wito kwa wananchi wa maeneo yote ya Zanzibar kuacha tabia ya kukata mikoko, kukata mawe yaliopo kandokando mwa fukwe na kuharibu matumbawe na miamba ya baharini ili kulinda na kuhifadhi visiwa vyetu kuingia maji ya bahari na mmong'onyoko wa fukwe. Aidha, nawaomba waendelee na jitihada za kupanda miti ya mikoko katika maeneo mbali mbali ili kunusuru hali isiendelee kuwa mbaya zaidi.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad**: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa yako maeno mengi yaliyokuwa yana uharibifu wa Mazingira ya ukataji wa Mikoko, lakini katika ripoti ya ukaguzi yakinifu iliyosomwa hapa Kikao kilichopita ilionesha kuwa Kisiwa Panza kuna eneo la Skuli na kuna eneo la Skuli ya Kisiwa Panza ambayo kuwa maji ya Bahari yanaingia mpaka kusababisha wanafunzi kushindwa kwenda skuli.

Je, Mhe. Waziri katika ripoti ile Wizara yako tayari imekwishakwenda kukagua na kama hamjaenda kukagua ni sababu gani za msingi hupelekea katika maeneo kama hayo muhimu musiyafanyie utaratibu mapema iwezekanavyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuarifu Mheshimiwa pamoja na Wajumbe wako wote wa Baraza lako Tukufu kwamba ofisi yangu ikiongozwa na mimi mwenyewe na watendaji wangu tulifika kabla ya Ofisi ya *CAG* kufika katika maeneo hayo na tutaendelea kuyatembelea tena maeneo karibu yote ambayo yamevamiwa na maji ya chumvi.

Kwa hiyo, hali hiyo inajulikana na ofisi yangu kabla ofisi ya *CAG* haijafanya ukaguzi na ndiyo maana hatua za kutayarisha mradi ikaingia eneo la Kisiwa Panza.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ambayo ametoa katika swali lake hilo.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri anajibu swali mama alisema kwamba maeneo yaliyoathirika kwa maji ya chumvi ni mengi sana na akaelezea maeneo mawili ambayo tayari yako katika matarajio ya kupata mradi eneo la Bwawani na Kilimani, lakini nataka nimueleze Mhe. Waziri kwamba miongoni mwa maeneo yaliyoathirika na maji ya chumvi ni eneo la Fuoni Kibondeni na wananchi wa eneo la Fuoni Kibondeni walifanya jitihada kubwa za kuanzisha Taasisi za Ushirika pale na kupambana na suala la Maji Chumvi na wameshapanda Mikoko mingi sana. Sasa swali langu Mhe. Mwenyekiti ni hivi.

Nataka kujua tu Mhe. Waziri wanatumia vigezo gani vya ile athari ya maeneo katika kutoa kipaumbele cha kutoa msaada kwa wizara yake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kwamba kwa Unguja na Pemba tuna maeneo zaidi ya 125 ambayo tayari yameathirika na kuvamiwa na maji ya bahari juu ya ardhi zao. Fuoni Kibondeni likiwa ni mojawapo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuangalia kipaumbele wataalamu wetu wanaangalia jinsi gani hali iko mbaya katika maeneo hayo ili kuanza kuyashughulikia maeneo hayo kwanza ambayo yako katika hatari kubwa na kuyaacha yale mengine, pia kutokana na fedha zenyewe kuwa chache. Hayo maeneo ambayo yako katika hatari ni mengi. Lakini yale ambayo yako hatarini zaidi ndiyo ambayo yamepangwa kwenye mradi kwa mara ya kwanza.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nitambue juhudi ambazo wizara yake inachukua katika kuwanasihi wananchi wasichafue mazingira, lakini kwa sababu wanaochafua mazingira ni binaadamu ambao mara nyengine au mara zote hulazimishwa ni sheria kutofanya hayo ambayo hayastahiki, na kwa kuwa mikoko inakatwa kwa asilimia kubwa sana, na kwa kuwa sheria ipo na inatoa adhabu kwa watu wanaokata mikoko kiholela.

(a) Je, mpaka leo wizara yake imewashitaki watu wangapi na kuwakatama na hatia.

(b) Kwa kuwa maji ya bahari hayasababishwi kuja juu kutokana na kukatwa kwa mikoko tu, mara nyengine athari inatokea kutokana na uchafuzi wa mazingira ambao wataalamu wanatwambia kutokana na nchi za viwanda vikubwa wanaharibu ile *Ozone layer* ambayo matokeo yake yanasababisha maji ya bahari kuongezeka kina chake.

Je, wizara yake imeandaa mpango gani mkubwa sana kwa nchi yetu ambao utasababisha kuzuia maji ya bahari yasipande katika kiwango kinachohatarisha maisha ya visiwa hivi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

(a) Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi idadi ya watu waliokamatwa katika uharibifu wa kuharibu mazingira yetu hasa katika suala la kukata mikoko ni suala ambalo linahitaji takwimu, naweza nikakuletea hili kwa maandishi.

Lakini naomba nikiri kwamba kwa sheria tuliyokuwa nayo ya mazingira ambayo Mhe. Mwenyekiti kwa bahati asubuhi hii nimewasilisha mswada wa kuweza kuifuta sheria ya mwaka 1996 na kuja na sheria mpya. Sheria hiyo inaanzisha ndani yake chombo ambacho kitakuwa na nguvu cha kuweza kupambana na uharibifu wa mazingira.

(b) Hili ni suala la kitaalamu na nikiri kwamba kwa ofisi yetu haina uwezo wa kuzuia kina cha maji ya bahari kupanda juu, hili ni suala ambalo ni la kimaumbile barafu inapoyayuka katika shehemu ambazo zimekuwa na barafu kipindi kikubwa sana lakini kutokana na uchafuzi wa mazingira barafu ile inayayuka na kutiririkia na kuwa ni moja ya kiwango cha bahari kupanda juu, kwa suala hili kwa kweli ni nje ya uwezo wetu sisi kama binaadamu.

Ninachoweza kusema ni kwamba ndani ya sheria hiyo suala la mabadiliko ya tabia nchi linaelezwa kwa kina jinsi gani litashughulikiwa kuanzia ngazi ya Shehia ili kuweza kuelimisha wananchi tuondokane na uchafuzi wa mazingira ili basi hatimae kwa pamoja kwa ulimwengu mzima kama tutaweza kupunguza uchafuzi wa mazingira inawezekana hali hiyo labda inaweza ikadhibitiwa.

**Nam. 18**

**Gharama za Usafiri wa Ndege kwa Viongozi wetu**

**Mhe. Saleh Nassor Juma-** Aliuliza**:-**

Katika Baraza la Nane, Mkutano wa Kumi na Sita, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alijibu swali la msingi lililotaka Serikali kuwa na ndege yake kwa ajili ya kuwasafirisha viongozi wake wakuu ndani na nje ya nchi. Katika majibu ya Mhe. Waziri alijibu kuwa kwa sasa Serikali haina uwezo wa kuwa na ndege hiyo kwa sababu ya ukubwa wa gharama za uendeshaji *running costs*. Kwa kuwa viongozi wetu wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huwa wanatumia ndege za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aina ya "*Foker* 50" au "*Foker* 25" pale wanaposafiri safari zao za ndani.

(a) Je, hizi gharama za uendeshaji *running costs* za ndege hizo wakati wa ziara za viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hubebwa na SMT au ufadhili wa wahisani.

(b) Kwa kuwa ndege hizo zipo tatu, ipo ile ya Rais; *State Jet*, "*Foker* 50" na "*Foker* 25", ambazo zinalala Dar es Salaam na viongozi wetu wakizihitaji wanaziagizia, au zinapokosekana hukodi ndege binafsi. Je, ni lini ndege moja kati ya hizi mbili *Foker* 50 na 25 itabaki hapa Zanzibar kwa ajili ya kuhudumia viongozi wakuu wa Zanzibar na kama pale itakapohitajika upande wa pili, wao wakaagizia.

**Mhe. Waziri wa Fedha –** Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kujibu swali nambari 18 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, gharama za uendeshaji wa ndege za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kwa kuwa kuna utaratibu wa kukodishwa ndege hizo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hulipia gharama za ukodishaji pale zinapotumiwa na viongozi wakuu wa SMZ.

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa ndege hizo zinasimamiwa na wakala wa ndege za Serikali, uamuzi wa mahala pa kuziweka ndege hizo ni wa Wakala. Hata hivyo, kuiweka ndege moja Zanzibar ni jambo linalowezekana lakini kufanya hivyo ni kuongeza gharama za uendeshaji, kwani Wakala atalazimika kuweka vifaa na wataalamu wa ziada wa kuzihudumia ndege hizo kwa kituo cha Zanzibar.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:**

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ndege hizi ametwambia kwamba zinapotumiwa na viongozi wakuu wa Serikali zinakodiwa, ina maana zinakodishwa kutoka katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano zinakodishwa kwa SMZ, na kwa kuwa SMZ ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, haoni Mhe. Waziri kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kushindwa kulipia gharama za uendeshaji pale viongozi wetu wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanapofanya ziara kutumia ndege hizi za SMT, haoni kwamba wanaidhalilisha Zanzibar hususan kwa vile nayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na fedha hizo za Jamhuri ya Muungano zilipatikana baada ya pesa za walipa kodi wa nchi hii ikiwemo sehemu ya Jamhuri ya Muungano na ionekane kama Serikali ya SMT iko *bias***.**

(b) Kwa sababu siku za nyuma hapa tulisikia kwamba kulikuwa na ndege za kijeshi ambazo zilikuwepo zamani enzi za marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ndege hizi sijui zinaitwa vipi nimesahamu mambo ya kijeshi siyafahamu, lakini ndege hizi zilikwenda kukaa Tanganyika yaani zilipelekwa Tanzania Bara.

Je, kipindi kile gharama za uendeshaji zililipwa na nani hata ishindikane kipindi hichi ndege hizi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano angalau moja kukaa hapa, ili hawa viongozi wetu wakapata unafuu wanaposafiri badala ya kwamba lazima waombe, mara ije, mara isije, huu si unyanyasaji mkubwa kwa viongozi wetu au sisi Wazanzibari kodi yetu haikutumika katika ununuzi wa ndege zile.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mhe. Saleh Nassor Juma baba yangu kama ifuatavyo.*(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba ndege hizi zinasimamiwa na wakala na siyo viongozi wa SMZ peke yao wanaozitumia kwa utaratibu wa kukodi, hata viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapotaka ofisi zao zinalipia kwa utaratibu wa kukodi na kwetu sisi ndiyo hivyo hivyo, Ofisi ya Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, wote wanalipia kwa utaratibu wa kukodi na hizi fedha ambazo tunazozilipia sisi pamoja na viongozi wa Muungano ndizo zinasaidia kuendesha ndege hizi.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa asubuhi ya leo kuweza kumuuliza shemegi yangu maswali mawili (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri sana Mhe. Waziri naomba nimuulize swali hili.

a) Mhe. Mwenyekiti, tulisikia SMZ ilikuwa na ndege yake. Je, Mhe. Mwenyekiti, ndege ile ipo wapi na kama imeuzwa. Je, kiasi gani iliyofikia kuuzwa.

b) Kutokana na kodi ambazo tunazolipa ni kiasi gani hata tushindwe kuweza kununua ndege yetu hapa ikaandikwa neno la SMZ.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi shemegi yangu kama ifuatavyo. *(Makofi).*

a) SMZ ilikuwa na ndege yake na sikumbuki katika kikao kilichopita nilijibu suala la SMZ ili kumrahisishia Mhe. Mwakilishi shemegi yangu akaitafute ile *hansard*, atapata maelezo ya kina kabisa ndege ile ipo wapi na tulikuwa kwa utaratibu upi.

b) Mhe. Mwenyekiti, katika swali lile lile nililolijibu kipindi kilichopita nilisema kutokana na hali yetu ya kiuchumi kwa sasa hatutaweza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwanunulia viongozi ndege, lakini *inshaallah* panapo majaaliwa tukichimba mafuta tutaliangalia suala hili, lakini kwa sasa hatutaweza. *(Makofi).*

**UTARATIBU**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, nilisema kuwa hiyo kodi ambayo tunayolipa ni kiasi gani hata kwamba tutashindwa kununua ile kodi yake nilitaka ni kiasi gani ili kulinganisha na kutokuwa na uwezo wa kununua ndege.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri alikuwa anataka ufafanuzi kuhusu kodi kiasi gani.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Kodi ipi anayoiuliza yeye. Kodi ya kukodisha ndege?

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ndiyo, ya kukodisha hiyo ndege tunayokodishwa na SMT.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kujibu swali la Mhe. Makame Mshimba Mbarouk shemegi yangu kama ifuatavyo.

Ukodishwaji wa ndege inategemea kiongozi mwenyewe anataka kwenda wapi. Ukisema unataka kwenda Pemba, bei ya Pemba ni tofauti na unaposema unataka kwenda Dodoma. Ukisema unataka kwenda Uturuki kwa kukodi zile ndege bei ni tofauti. Kwa hivyo inategemeana na pahala ambapo unapotaka wewe mwenyewe kuitumia kwenda.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo sana, tena sana la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, ndege zile za Serikali kutokana na Jamhuri ya Muungano ikiwemo Zanzibar, unaweza kuwaambia wananchi na Wajumbe wa Baraza hili tokea kuanza Shirika lile la Ndege la Serikali, Zanzibar imenufaika kiasi gani.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kujibu swali la swahibu wangu Mhe. Jaku kama ifuatavyo.

Kufaidika kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni pale ambapo viongozi wetu wanapokuwa na safari na kutaka kuzitumia ndege zile pasipo na vikwazo. Mimi ni shahidi na wenzangu ni mashahidi, viongozi wetu nao wana nafasi ya kuzitumia ndege zile pasipo na vikwazo, nadhani hiyo ni faida mojawapo ambayo viongozi wetu na Serikali yetu inafaidika kwamba ndege zile tunazitumia sote; viongozi wa SMT na viongozi wa SMZ bila ya vikwazo vyovyote.

**UTARATIBU**

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie Kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu cha 58 (10) ambacho kinasema kwamba katika mjadala wowote Mawaziri watatajwa kwa kutumia majina ya nyadhifa,

wajumbe wengine wote watatajwa kwa kutumia neno Mheshimiwa kabla ya majina na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu wataitwa kwa mujibu wa nyadhifa zao wanapowasilisha ripoti za Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba sasa tumeanza kutumia majina ya baba, mwanangu, shemegi ambayo Kanuni zetu hazituruhusu za Baraza, tukiendelea kufanya hivyo na sisi humu tuna marafiki, wapenzi. Kwa hivyo tukianza kutumia hivyo ni kushusha hadhi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba utaratibu tuufute tutumie majina ambayo yametajwa katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi. *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe lakini kwa kuweka *hansard* sawa kifungu cha Kanuni ambacho umekitumia sicho na umekusudia kuzungumzia kifungu cha 59 (10). Naomba watu wa *hansard* hilo. Ahsante sana, Katibu.

**Na. 43**

**Tawi la Kitivo cha Udaktari Pemba**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - aliuliza:

Kwa kuwa Wizara ya Afya kwa mashirikiano na Serikali ya Cuba imeanzisha mafunzo ya udaktari *(Zanzibar School of Medicine)* yenye lengo la kuondosha tatizo la madaktari hapo Zanzibar. Na kwa kuwa skuli hiyo inalo tawi lake katika hospitali ya Chake Chake kule Pemba. Na kwa kuwa *SUZA* tayari wameanzisha kozi ya shahada ya mwanzo ya udaktari *(First Degree in Medicine).* Je, ni lini chuo hicho cha Taifa kitaanzisha mafunzo ya udaktari tawi la Pemba ili kupunguza gharama kwa wale wanafunzi wanaotokea Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 43 kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Wizara ya Afya kwa mashirikiano na Serikali ya Cuba imeanzisha Chuo cha Mafunzo ya Udaktari *(Zanzibar Medical School)* kwa lengo la kuondosha tatizo la madaktari hapa Zanzibar. Mafunzo yanaendeshwa kwa wanafunzi waliopo Unguja na kundi jengine kwa wanafunzi wachache waliopo katika Hospitali ya Chake Chake, Pemba.

Wanafunzi waliosomea Unguja tayari wamehitimu mafunzo yao na wanafunzi 12 walioanza katika Hospitali ya Chake Chake Pemba sasa hivi wanaendelea na masomo ya miaka miwili hapa Unguja. Masomo ya udaktari yanaendeshwa na *Zanzibar Medical School* yatasita baada ya wanafunzi hao kuhitimu.

Mhe. Mwenyekiti, pia ni kweli kuwa *SUZA* imeanzisha mafunzo ya shahada ya udaktari kwa msaada wa mabingwa kutoka Cuba kuanzia mwaka 2013/2014. Jumla ya wanafunzi 82 wa mwaka wa kwanza na wa pili wanaendelea na mafunzo yao. Mafunzo yanaendeshwa na wakufunzi watano kutoka Cuba na Hospitali ya Mnazi Mmoja inatumika kwa wanafunzi hao kufanya mazoezi ya vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Kwa hivi sasa chuo hakina mpango wa kufungua tawi la masomo ya shahada ya udaktari huko Pemba kutokana na gharama kubwa za kuendesha mafunzo katika maeneo mawili tofauti, uchache wa wakufunzi na wanafunzi kwa gharama kubwa ya vifaa muhimu vya kufundishia. Chuo Kikuu kinakusudia kuanzisha shughuli zake huko Pemba kuanzia mwezi wa Julai, 2015 katika kampasi ya Chuo cha Ualimu cha William Mkapa, Mchanga Mdogo na upembuzi wa kuainisha aina ya masomo yatakayotolewa katika kampasi ya Pemba unaendelea kufanyika. Mpango huo unalenga kutoa mafunzo kwa kutumia utaratibu utakaoleta tija zaidi kwa gharama ndogo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa miongoni mwa wanafunzi wanaofanya digrii ile ya *medicine* hapa *SUZA* miongoni mwao ni kutoka katika Kisiwa cha Pemba, na zaidi ya asilimia 50. Na kwa kuwa ulizungumzia suala la gharama kwamba kuweka *Faculty of Medicine* tawi la Pemba ni gharama.

Je, gharama wanazopata wanafunzi kwa kuwaweka hapa Unguja wanaotoka Pemba kwa *semister* nzima wakipata *lectures* kutoka *lecturers* hawa hapa na gharama ya kuwaacha kule kwa kufungua *Faculty of Medicine* tawi la Pemba katika Hospitali ya Chake Chake Pemba pale kama walivyofanya darasa la Cuba pale wanabaki pale anasafiri *lecturer* kutoka huku. *Lecturer* mmoja anakwenda kutoa *lectures* pale kwa wanafunzi waliopo tawi la Pemba. Je, ni gharama zipi kubwa kati ya kuwaweka wanafunzi 150 kutoka Pemba hapa na kumpeleka *lecturer* pale hospitali ya Chake Chake kutoa *lectures,* ni gharama ipi kubwa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma kwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza sina hakika kama wanafunzi waliopo SUZA wanafika asilimia 50 kutoka Pemba, yaani asilimia 50 ya wanafunzi waliopo SUZA wanachukua *medicine* wanafikia asilimia 50 kutoka Pemba, hilo sina hakika nalo, itabidi nilifanyie utafiti zaidi.

Lakini la pili, Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kufungua kituo cha udaktari ni gharama kubwa, wakati kituo hichi kipo Unguja na wanafunzi wa Pemba wanaruhusiwa na wanakuja Unguja kusoma pamoja. Sasa Mhe. Mwenyekiti, si suala la *lecturer* kumtoa Unguja kumpeleka Pemba kwenda kuwafundisha wanafunzi hapana, kuna vifaa vinavyohitajika kule vya udaktari ambavyo mwanafunzi anayesomea udaktari itabidi avitumie kwa kufanyia *practical*.

Sasa vifaa hivyo Naibu Waziri amesema ni ghali mno, ni gharama kubwa. Kwa hivyo yeye Naibu Waziri ameona na mimi Waziri naona na wizara inaona si hasara, na ni nafuu kufungua kampasi moja tu ya udaktari pale Unguja ili wanafunzi wachache kutoka Pemba kuruhisiwa kuja Unguja kuchanganyika na wenziwao. Na hii siyo udaktari tu, masomo mbali mbali yanajumuisha wanafunzi kutoka Unguja na Pemba na hilo linakwenda bila ya wasi wasi na bila ya matatizo. Hivyo kufungua kampasi ya udaktari kwa hivi sasa itakuwa ni gharama kubwa wakati tunayo kampasi kama ile hapa Unguja. *(Makofi).*

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimefurahi sana baada ya kusikia au maelezo mawili kati ya Naibu Waziri na Waziri.

Kwa kuwa amesema kuwa sasa hivi ni *expensive* sana huko Pemba. Mhe. Mwenyekiti, Pemba wako watu wengi, Pemba wapo wasomi wengi. Je, Mhe. Waziri haoni ipo haja kwa kuwa tuna kitabia tunapokuwa tunataka kitu ambacho cha muhimu serikali inakuwa inafanya mchango wa hiyari au inatafuta wafadhili wa kuweza kufanya hili jambo.

Je, Mhe. Waziri haoni ipo haja sasa hivi kwa makusudi akafanya mchango huo wa hiyari kwa kupitia Serikali Kuu au kwa kupitia kwa wafadhili ili ikapatikana hiyo kampasi moja Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mshimba swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu mama nilizungumza kama tatizo tulilonalo kufungua *medical school* kwa Pemba mojawapo ni ukosefu wa vifaa na wale *professors* ambao wanatoa hii fani. Lakini kufungua kampasi kama kampasi ya Chuo Kikuu *SUZA*, nilizungumza kama Julai mwaka huu, *SUZA* wanaanzisha kampasi yao pale Mchanga Mdogo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Suala lilikuwa la Mhe. Mshimba na yeye kasema kuhusu utaratibu lakini la msingi *okay* tunakuja kwako, kuhusu utaratibu.

**UTARATIBU**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, suala la msingi ni kuitaka Serikali ifungue *Faculty of Medicine* tawi la Pemba pale Hospitali ya Chake Chake, lakini pale anazungumzia Mchanga Mdogo ambapo wanataka kufungua *Faculty of Education*, hapa sisi tunazungumzia *Faculty of Medicine* pale Hospitali ya Chake Chake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Saleh Nassor Juma hajataka kunifahamu. Kwa idhini yako naomba nimjibu.

Kama uwezo hivi sasa wa Wizara au Chuo chetu Kikuu cha *SUZA* kuanzisha *Medical School* kwa Pemba hatuna uwezo huo. Uwezo wetu ambao tunao ni kuanzisha hilo tawi la *SUZA* kwa Pemba kwa hivi sasa ambalo litaanza kazi mwezi Julai, na nilisema hatuna kutokana na bajeti ambayo tunayo Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tukubali na Mhe. Waziri alisema, hili suala si suala la kukurupuka tu ukaanza ukasema kama unataka kufanya.

Wanafunzi ambao nimesema wa mwaka wa kwanza na wa pili tulionao ni 82. *Resources* ambazo tunazo ndiyo hizo hizo na moja ni Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ambayo inatufaa sana wanafunzi wale kusoma kwa vitendo. Ni vipi tutawachukua wanafunzi tuwapeleke wakati Hospitali ya Rufaa ambayo wanafunzi wanasoma kwa vitendo ipo hapa Unguja kwa hivi sasa.

Kwa hivyo, ni lazima Waheshimiwa Wawakilishi mukubaliane na hali halisi ya serikali na wizara ambayo tunayo kifedha. Tunataka kila sehemu ambayo tuna uwezo wa kupeleka hizi huduma, wapeleke ili wanafunzi wetu wasome kwa urahisi, lakini tatizo tulilonalo ni nyenzo.

**Nam. 120**

**Takwimu za Kesi na Watu Wanaohusika na Ubakaji Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali langu naomba uniruhusu kwa dakika moja tu, ili nitoe mkono wa pole kwa familia ya Marehemu Mhe. Issa Ahmed kwa msiba uliotokea India, niwaombe familia yake wawe pole na sisi sote humu ni maiti watarajiwa, wakati wowote na saa yoyote tutakuwa maiti, *Alhamdulillah Rabil Alamina, Innalillah Wainnaillah Rajiun.* Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba serikali itoe jawabu ya swali namba 120 kwa Wizara isiyokuwa na Naibu Waziri

Pamoja na mikakati inayochukuliwa na Serikali ya kupambana na vitendo vya ubakaji bado tatizo hilo linaendelea kuwa ni kilio kikubwa kwa wananchi wa Unguja na Pemba kupitia ripoti za uchunguzi wa Chama cha Habari cha Wanawake Tanzania Ofisi ya Zanzibar (TAMWA).

(a) Ni watu wangapi mpaka sasa kuanzia Januari 2013 hadi Disemba, 2014 waliopatikana na hatia kwa makosa ya ubakaji na ulawiti.

(b) Ni kesi ngapi ambazo zimeripotiwa katika kipindi hicho zinazoendelea Mahakamani na ambazo tayari zimetolewa hukumu.

(c) Kwa kuwa Sheria ipo ya kukabiliana na vitendo hivyo lakini bado watoto wanaendelea kubakwa, je, Serikali ina mpango gani wa kuleta Sheria kali ambayo itasaidia kukabiliana na vitendo hivyo ikiwemo kuhasiwa kwa watu wanaopatikana na hatia ya vitendo hivyo.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 120 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Ni kweli tatizo la ubakaji bado linaendelea kuwa sugu hapa kwetu, lakini serikali inaendelea kupigana na tatizo hilo kwa nguvu zake zote.

(a) Kuanzia Januari 2013 hadi Disemba 2014 washtakiwa 7 walipatikana na hatia katika kesi 6 zilizofunguliwa mahakamani Unguja na Pemba, kwa makosa ya ubakaji na ulawiti.

    Katika kesi za kubaka makosa matatu yalitolewa adhabu kama ifuatavyo.

Kesi moja mshtakiwa alifungwa miaka mitano, kesi nyengine mshtakiwa alifungwa miaka 15 na kesi nyengine washtakiwa wawili walifungwa kila mmoja kifungo cha miaka 30. Adhabu zilizotolewa za kulawiti zilikuwa kama ifuatavyo.

Mshtakiwa mmoja alifungwa miaka mitano, mwengine alifungwa miaka mitatu na mshtakiwa mmoja alifungwa miaka miwili.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kesi 209 zilifunguliwa mahakamani ambapo 70 zimetolewa uamuzi na kesi 139 bado zinaendelea.

(c) Mhe. Mwenyekiti, adhabu kali pekee sio suluhisho la kutofanyika kwa makosa hayo. Kwani mbali na wanaopatikana na hatia kupewa adhabu kali, lakini bado wingi wa makosa hayo yanaendelea kuripotiwa katika sehemu mbali mbali nchini kwetu. Kwa hivyo, hakuna hata nchi moja hivi sasa ulimwenguni ambayo inayo adhabu ya kuhasiwa kwa mbakaji au anayelawiti. Serikali inaendelea kutafuta ni adhabu gani muafaka iweke kwenye sheria zetu ili kupunguza makosa hayo.

Hata hivyo, jamii pamoja na wazee wakiwemo walimu maskulini na vyombo vyetu kama vile Polisi, vyuoni na taasisi nyengine, nao pia wana mchango mkubwa katika kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa tatizo hili

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu muafaka kabisa ya kujibu swali la msingi Mhe. Waziri asiyekuwa na Naibu Waziri, kwa kuwa tatizo la unyanyasaji watoto ni la muda mrefu.

a) Je, ni lini serikali italeta sheria yenye adhabu kali kuliko zinazotolewa hivi sasa, ikiwemo ile ile ya mtu kuhasiwa. Akibainika lakini pindipo. Ni lini serikali italeta mswada.

b) Kwa kuwa kesi za ubakaji na unyanyasaji wanawake zinachukua muda mrefu mahakamani. Haioni haja wizara yako kuanzisha mahakama maalum kwa vitengo hivi.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, adhabu kali zipo. Ukienda katika sheria ya jinai, yaani wanaita *penal decree* kuna sehemu ya 15 ambayo inatoa adhabu ya makosa kama haya na sehemu hizo kuna mambo chungu nzima. Kwa mfano, ubakaji ni kifungo cha maisha, kwa hivyo hii ni adhabu kali sana, hakuna adhabu nyengine kama kifungo cha maisha.

Kuna suala la kuwakamata kamata watoto ni miaka 14, kuna kosa la kuwaingilia kwa mfano wale ambao ni wagonjwa ni miaka 14. Kwa hivyo, katika sheria zipo zaidi ya adhabu kali kama hizi. Kwa hivyo, ni mahakama ambazo zinatakiwa zi- *practice* hizi na kutokana na matatizo tuliyokuwa nayo haya kesi binafsi serikali tulizungumza katika vikao mbali mbali. Nashukuru kwamba mahakama hivi sasa zinatekeleza wajibu wao kwa vizuri kabisa, kwa sababu vifungo wanavyotoa hivi sasa ni kama nilivyovitaja ni kuanzia miaka mitano na kuendelea, kwa hivyo hizo ni moja katika adhabu kali.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo ambalo tunalipata kwa nini kesi zikachukua muda mrefu. Kama nilivyosema mwanzo ni mashirikiano ya jamii ni pamoja na watu wenyewe binafsi. Kwa mfano, kuna kesi nyingi hivi sasa ambazo tunataka kuzipeleka mahakamani unamwita shahidi uje kuchukua maelezo haji, anakwambia hataki kwenda mahakamani, kwa sababu akienda pale jamii watamuona. Anakwambia hataki kwenda mahakamani kwa sababu akienda mahakamani ile kesi itapata- *publicity* yule mtoto sijui ni mdogo atafanya nini. Kwa hivyo, na jamii yenyewe inatuvunja moyo, kwa sababu ikiwa huna ushahidi huwezi kumtia hatiani mtu.

Sasa kama huwezi kumtia hatiani kwa sababu huna ushahidi, hii jamii ndiyo inayotakiwa ichukue jukumu la kukaa na kutoa ushahidi. Ndio maana unamwita mtu mara ya kwanza haji, unamwita mtu mara ya pili haji unaahirisha kesi, inaweza ikachukua miezi sita au saba haji shahidi mahakamani. Ndio maana kesi nyingi za kulawiti au za kubaka au zenye mambo kama hayo zinachukua muda mkubwa.

Kwa hivyo, ombi langu kwa jamii ni kwamba jamani haya ni matatizo ya nchi, haya ni matatizo yetu pamoja, sote tushirikiane tuweze kutoa ushahidi na ushahidi huu ndio utasaidia kumtia adhabu yule mtu anayehusika. Vyenginevyo kesi zitabakia tu na zikibakia kuna sheria ambayo Mhe. Jaku Hashim na Waheshimiwa wengine hapa

waliipitisha, kwamba kesi kama itakaa zaidi ya miezi minne haijasikilizwa haijaleta shahidi basi kesi ile iondolewe. Sasa unamwita Mhe. Jaku au mtu mwengine haji kutoa ushahidi, ikifika miezi minne, sasa tutatumia sheria nyengine tuiondoe watu watalalamika. Kwa hivyo, hayo ni matatizo mengine ambayo tunayapata. Kwa hivyo, nawaombeni sana jamii kwamba hizi ni kesi muhimu na tunataka tuzishughulikie haraka, lakini kwa ushirikiano wenu, tunapopata ushirikiano kama huo naamini kwamba tutakwenda haraka haraka.

Suala la mwisho alilosema kwamba je tunaweza kufanya kesi kama hizi kuwa na utaratibu wake maalum. Ndio tunaweza, tumeshafikiria utaratibu wa kufanya *special,* kesi hizi katika *session* wanaita *session case*, ambayo ikianza ile kesi inakwenda moja kwa moja mpaka kumalizika. Lakini hii ina utaratibu wake, hatuanzi tu, ni lazima tuhakikishe kwamba ule ushahidi wote umeshakamilika na mashahidi wapo tayari na mambo yote ambayo yanahusu kuendesha kesi moja kwa moja yapo tayari.

Kwa hivyo, hivi sasa tunajaribu kutizama uwezekano wa aina hiyo na uwezekano huu ndio wito wa *Commonwealth*, ambayo nilisema kwamba kesi kama hizi kuwe na *session,* kesi ambazo mtu akishtakiwa inakwenda moja kwa moja bila ya kusimama mpaka inamalizika, kidogo itapunguza ule muda wa kusikilizwa kesi hizi, lakini lazima uwe na mashahidi, lazima uwe na nyenzo zako tayari na kamili, hapo tunaweza tukafanikiwa kwa utaratibu huo. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na sheria ambayo ameitaja, kwamba inatoa mwanya kwa watu wengine ambao wanafanya hivi vitendo kesi kufutwa kama hakuna ushahidi kamili baada ya miezi minne. Kumekuwa na malalamiko juu ya sheria nyengine ambazo zinazohusiana na kutoa hukumu juu ya masuala haya kwamba zinatoa mwanya, yaani zinatoa *loophole* kwa hawa watuhumiwa ku- *walk out freely.*

Je, ni lini serikali kwa nia ile ile njema, dhamira na lengo ambalo imekuja nalo la udhalilishaji sasa basi, italeta sheria hizi ambazo zinatoa *loophole* kwa mtuhumiwa kuachiwa *free* ndani ya Baraza ili tuzifanyie marekebisho kama tunavyoshuhudia sheria nyengine zinavyoletwa kwa hati za dharura hapa.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, sheria zipo nyengine ambazo zinasema kwamba adhabu ya kosa lile ni kifungo au ni faini ziko kweli, na hakimu anaweza akatumia *loophole* hiyo, lakini siku zote unapokuwa hakimu unatakiwa utizame ile *interest* ya serikali na *interest* ya jamii, na kutokana na matatizo haya yaliyokuwa ni mengi na mazito, tunashukuru mahakimu wetu kwa kupitia Mahakama Kuu na Jaji Mkuu baada ya kukaa pamoja tukasema lazima tuwe na kitu ambacho kitadhibiti haya.

Kwa hivyo, hakimu anaweza akatumia sheria ile ambayo inampa *loophole* hiyo, lakini ile imempa uwezo wa kuchagua katika adhabu mbili zile. Kwa hivyo, tumejaribu kukaa nao pamoja na tumekubaliana kwamba suala hilo sasa linadhibitiwa. Nafikiri kuanzia nyuma huko hakuna mtu anayepewa faini au anayeachiwa huru, ni kifungo tu ambayo ndio adhabu kubwa. Kweli zipo lakini kutokana na *will* ya mahakama kifungu hicho hatukitumii, lakini sio busara kukibadilisha kwa sababu kuna makosa mengine yanaweza kutumiwa kwa shughuli hizo, lakini katika suala la *rape* kifungu hicho hakitumiwi.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini kunakuwa na kesi nyengine baada ya kufika polisi tu, baada ya kupewa ushahidi kamili na wanatokea askari ambao wanakuwa ni wapelelezi, lakini baada ya kukuta watu ambao wanakuwa na fedha wakawalisha fedha, basi askari zile kesi kabla ya kuzifikisha pahali panapohusika wanazibanabana wakaziua.

Je, watu kama hawa askari wakiletwa kwa ushahidi wakiwa na mambo hayo, ni hatua gani wizara yako itachukua kwa askari hawa?

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli matatizo hayo yapo, lakini matatizo haya ni ya wazee peke yao na nimeshazungumza mimi na wazee na nimeshatoa wito kwa wazee, lakini bado hawajakubali. Kwa namna gani, kwa sababu kesi inapokuwa polisi au inapokuwa mahakamani basi mzee atakuja atakuomba sana kesi ile uifute. Sasa anakwenda polisi anawaomba polisi wanakubaliana huko ili kesi ifutwe kwa makubaliano yao wenyewe huko. Sasa tukiifuta kesi pale tujue kwamba *society* hii inafikiria vyengine.

Kwa hivyo, wazee musiingilie hizi kesi, mtu akikamatwa akipelekwa polisi nyinyi ni lazima mkazane ili kesi iende mahakamani, lakini msiende kule mkasema mtaisawazisha au mtaozana kisirisiri itakuwa haina maana na kesi bado zitaendelea na matatizo bado yataendelea. Hata kesi zinazofika mahakamani au zinazofika kwa mwendesha mashtaka, wazee chungu nzima wanakuja, basi kesi mwanangu tutafanya hili suluhu tutafanya nje na nini. Sasa tukifanya hivyo makosa haya yataendelea.

Kwa hivyo, wito wangu kwa wazee na kwa vyombo vyengine vinavyohusika, tunapopata kesi kama hizi, tafadhalini tukae kama ni mashahidi ili kesi ziende mahakamani na washtakiwa wakipatikana na hatia waweze kupata adhabu kali ambazo zitakuwa ni fundisho kwa watu wengine.

**Nam. 39**

**Wananchi wa Vitongoji Makaani Kutopatiwa Fidia**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Serikali pale inapotaka kufanya shughuli mbali mbali za maendeleo katika maeneo husika, hufanya tathmini ya uharibifu wa mali za wananchi kabla shughuli hizo hazijaanza na hatimaye kufanya malipo.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hadi leo hii wasiwalipe wananchi wa eneo la Vitongoji pale Wizara hiyo ilipokata mimea pamoja na miti ya wananchi wakati wa kupeleka umeme kwenye ma-*crusher* yaliyoko Makaani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kujibu naomba kuanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inamiliki mtambo wa kusaga kokoto pamoja na mtambo wa kupikia lami katika eneo la Kwareni Vitongoji. Kwa siku nyingi mtambo huo ulikuwa unatumia nishati ya umeme inayotokana na jenereta ambalo lilikuwa likitumia mafuta. Wizara imekuwa ikitumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kuendesha mtambo kwa ajili ya kuhudumia jenereta hilo. Ili kupunguza gharama kubwa hizo iliyokuwa ikiingia serikali, wizara iliamua kuweka umeme ili mitambo hiyo iweze kutumia nishati ya umeme badala ya ile ya jenereta na umeme huo tuliutoa katika eneo la Skuli ya Fidel Castro, katika eneo la Vitongoji.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wizara ilistahiki kuwalipa fidia wananchi ambao mazao yao yaliathirika wakati wa zoezi la kupeleka umeme kwenye eneo hilo la Kware ya Vitongoji Pemba. Hata hivyo, pamoja na nia ya dhati ya wizara ya kutaka kuwalipa wananchi hao fidia, bado tatizo la upatikanji wa fedha kwa wakati limekuwa ni kikwazo kikubwa kutekeleza wajibu wetu huo kwa wakati unaostahiki.

Hivyo, wizara inafanya kila jitihada kutafuta fedha kutoka vyanzo vyetu mbali mbali, ili iweze kuwalipa wananchi hao haraka iwezekanavyo. Wizara inaahidi kuwalipa wote walioathirika katika zoezi la kupeleka umeme katika mitambo hiyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa wizara inaendelea kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi kwa uvumilivu ambao wamejitolea na tunawaomba waendelee kutuvumilia hadi pale tutakapoweza kupata fedha tuweze kuliondoa tatizo hilo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kuvunja moyo sana aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja dogo sana kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tatu tangu wakulima kukatiwa mazao yao ambayo yalikuwa yakiwaendeshea maisha, yaani walikuwa wakipata maisha kutokana na mazao yao hayo, kwa maana ya minazi, miembe, michungwa na kadhalika, huu ni mwaka wa tatu. Kwa kuwa "*justice delaying justice denying".* Kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa ni sawa sawa na kwamba haikutolewa kabisa. Kwa kuwa hadi leo hii unasema serikali ndio kwanza mbali ya miaka mitatu ya nyuma inataka tena siku za ziada, itafute pesa ndogo ndogo hizi kwenda kuwalipa maskini wa Jimbo la Wawi katika maeneo ya Vitongoji, Umangani, Kibokoni, Udusini na kadhalika.

Huoni kuendelea kuchukua muda kutowalipa wakulima hawa ni sawa na kuwadhulumu na ni aibu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hilo ni (a)

b) Kwa kuwa Shilingi milioni arubaini tu wakati wakulima mazao yao mnashindwa kulipa, na leo panajengwa barabara ya Ole/Kengeja ambayo zinahitajika karibu bilioni moja kwa ajili ya fidia. Je, huoni kwamba mtakuwa na kazi kubwa ya kuendelea kuwadhulumu wananchi ikiwa hizi zimewashinda milioni 38, hii bilioni moja mtaipata kulipa fidia ya nyumba za wananchi zitakazovunjwa na mazao yao kutoka Ole mpaka Kengeja, mtazipata wapi pesa hizo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, wajibu wa Serikali ni kusogeza maendeleo kwa wananchi wake, ipo baadhi ya miradi ambayo Serikali tunachukua mikopo ama ufadhili na majibu yetu kama Serikali ni kupata maeneo kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Baadhi ya miradi ya barabara iko ambayo tunalazimika kama sisi Serikali kulipa fedha kama fidia ili kuweza kupisha miradi hii ya Maendeleo kutokana na fedha za mikopo ama wafadhili.

Miradi hii yote tunayozungumza inahitaji kulipwa fidia ambapo Wizara yetu inalazimika kulipa, sasa Mheshimiwa Mwakilishi ni kweli kiasi ambacho wananchi wa eneo la Vitongoji ukiangalia kwa eneo lile tu ni kidogo, lakini unapokirejesha katika jukumu la Wizara ukijumuisha na yale majukumu mengine deni lile linakuwa kubwa, kwa sababu sio tu kama Wizara yetu inadaiwa hizo milioni 30, au milioni 40 kwa ajili ya Vitongoji.

Sasa majibu ya Serikali ni kuona kwamba tunatafuta nguvu ili tuweze kulipa madeni haya mengi kwa maeneo yote yanayohusika, tuna maeneo ambayo tumeanza kulipa kwa nia na dhamira ile ile ya kuona kwamba wananchi wetu hatuwapelekei usumbufu. Niendelee kukuomba Mheshimiwa Mwakilishi uendelee kuwanasihi wananchi wetu hawa wametuonesha ustaarabu na uvumilivu mkubwa kwa kuwa na subira, waendelee kufanya subira yao na sisi hali itakapoturuhusu tutakapopata fedha tutakwenda kulipa deni hili, tunatambua uungwana ni kuwalipa wananchi hawa ili na wao waweze kufurahia miradi ambayo inatekelezwa na Serikali yao.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa kwa kuwa ardhi ni mali ya Serikali na katika sehemu ya Serikali ni wananchi wenyewe wanaounda Serikali, katika jibu lake Mheshimiwa Wangu Naibu Waziri ametaja katika miradi ambayo iliyokuwa muhimu kwa jamii hasa katika masuala ya barabara, wanasema imewalazimu lazima kuweza kulipa fidia wananchi wanaopata athari zile.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna barabara ya Kiombamvua watu wameathirika nyumba zao, watu wameathirika mimea yao ni sababu zipi mpaka leo hii hawajalipwa fidia na wengine wanalala pahali ambapo hapastahiki.

**Mhe. Naibu Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, katika utaratibu wa ujenzi wa barabara eneo ambalo linakusudiwa kujengwa barabara linapokuwa lina majengo ama miti, wajibu wa Serikali ni kuondosha majengo ama miti ile kwa ajili ya kupitisha ujenzi huo. Na sera ya Serikali iko wazi kwamba hatutovunja au haitovunjwa nyumba ya mwananchi yeyote kabla ya kulipwa kwa fidia.

Isipokuwa kwa upande wa miti ni kweli tunakata miti ama vipando kwa ajili ya kupisha ujenzi wa barabara na baadaye tunapopata fedha ama iwe wakati wa ujenzi, au baada ya ujenzi mwananchi huyo analipwa haki zake. Sasa kama kuna mwananchi ambaye atakuwa analalamikia kwamba nyumba yake imevunjwa bila ya shaka mwananchi huyo atakuwa amelipwa fidia, isipokuwa kuna baadhi ya watu ambao wanakuwa na nyumba zao zipo karibu na ujenzi wa barabara zinaweza kuwa nyumba zao hizo zimeathirika wakati wa ujenzi wa barabara mtu huyo atachelewa kulipwa, kwani utaratibu wetu lazima tukafanye tathmini tena tujiridhishe tutafute kwa ajili ya kumlipa.

Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa Mwakilishi kama kuna mtu analalamika basi mwananchi huyo itakuwa imeathirika nyumba yake wakati wa ujenzi wa barabara na sio kabla ya upishaji wa eneo la ujenzi wa barabara, nimuombe tu mwananchi huyo aje Wizarani kwetu tutawatuma wataalamu wetu watakwenda kufanya tathmini na baadaye kama kuna haki zake kadri inavyostahiki.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri wewe mwenyewe utakuwa shahidi katika ujenzi wa barabara kutoka Chwale/Kojani kuna wananchi ambao hawakufanyiwa makisio, lakini kuna wananchi ambao waliathirika baada ya njia kupita, wananchi hao nimeshakuja nao mpaka ofisini kwako na ulifanya jambo zuri ukatuma watu wako kuweza kufanya makisio, lakini mpaka hivi nazungumza jambo hili limekufa na wewe mwenyewe uliniahidi kwamba utafika na mpaka leo hujafika.

Je, ni lini wananchi wale walioathirika baada ya kwishapita barabara watapata malipo yao?

Na vile vile ni lini wewe mwenyewe kwa sababu una ahadi, lini mimi na wewe tutafuatana kwenda kule kwa sababu hii imeshindikana naomba jibu la Serikali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Ni kweli kwamba kama Mheshimiwa Muwakilishi anavyoeleza kwamba wananchi wa Chwale na Kojani kwa maana kile kipande ambacho kimepita barabara tunastahiki kuipongeza Serikali kwa kutelekeza mradi mkubwa na mzuri wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

Lakini mradi huo ambao tunauzungumzia ni mradi ambao umeendeshwa na Shirika la *Millennium* la Marekani, ambapo kwa asilimi 99.9% fidia yote imelipwa na wahusika wa mradi huo, isipokuwa katika eneo hilo ambalo amesema Mheshimiwa Mwakilishi kuna nyumba ambazo ziliathirika wakati wa ujenzi, kama nilivyojibu katika jibu ambalo nilikuwa namjibu Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk, kwamba kwa kuwa hawa wanaolalamika nyumba zao hazikuathiriwa wakati wa kabla kwa ajili ya kupisha ujenzi bila ya shaka jukumu hili limerudi kwa Serikali, na sisi kama Serikali tumepeleka timu ya wataalamu imekwenda kufanya tathmini baadaye imerudi kwetu tunaendelea kutafuta vyanzo na kupata nguvu za kifedha ili twende tukatizame.

Suala langu mimi mwenyewe binafsi kwenda kutembelea eneo hili nimekwenda kutembelea katika kipindi kisichozidi wiki nne, nilikuwa nimefuatana na Katibu Mkuu pamoja na Waziri, kwa bahati mbaya sikuweza kufanya mawasiliano nayo Mheshimiwa Mwakilishi kukujuulisha kama nakwenda Pemba na nitapita eneo la Chwale.

**Nam. 33**

**Ongezeko la Mahoteli Mji Mkongwe Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ilitangaza kupiga marufuku ujenzi holela wa Mahoteli katika Mji Mkongwe wa Zanzibar lakini bado kumekuwepo na kasi kubwa ya ongezeko la mahoteli na mikahawa na kuathiri mila na silka za wakazi wa mji huo.

(a) Ni chombo gani kinaendelea kutoa vibali vya ujenzi wa mahoteli kinyume na uamuzi wa Serikali kupiga marufuku ujenzi holela wa hoteli katika Mji Mkongwe.

(b) Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha mila, silka na desturi za wakaazi wa Mji Mkongwe ambao una maeneo mengi ya ibada na taaluma, zinalindwa na haziathiriki kutokana na ongezeko holela la ujenzi wa mahoteli na mikahawa katika mji huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** – Alijibu:-

Mhe.Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 33 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe ndiyo inayotoa vibali vya ujenzi na ukarabati ndani ya Mji Mkongwe kwa nyumba za kuishi, mikahawa, mahoteli na nyenginezo. Mamlaka ikishatoa kibali cha ujenzi au

ukarabati aliyepewa kibali hicho akimaliza kukamilisha kazi hutafuta leseni ya kuifanya nyumba hiyo kuwa hoteli kupitia Kamisheni ya Utalii bila ya Mji Mkongwe kuwa na taarifa.

Kibali cha ujenzi wa hoteli kimetolewa mwaka 2010 kwa hoteli ya Mambo Msige baada ya kutolewa *Certificate* kutoka *ZIPA*, miongoni mwa madhumuni makubwa ya kuweka uwiano wa hoteli na mikahawa yanayoongezeka kwenye makazi ya wananchi. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Mhe.Mwenyekiti, kuongezeka kwa Mahoteli na Mikahawa kunapelekea kuzidiwa na wingi wa wageni ambao hupelekea kuchangia kuathirika kwa urithi usioshikika zikiwemo silka, mila na desturi za wakaazi wa Mji Mkongwe.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutokuwa na afya naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa taasisi zote ni za Serikali zinatoa kibali cha ujenzi wakati Serikali tayari ndani ya Baraza hili iliahidi kupitia kwa Mheshimiwa Waziri mzoefu Mheshimiwa Ramadhan Abdalla Shaaban kupunguza kasi ya ujenzi wa hoteli katika Mji Mkongwe.

a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri tukifuata kumbukumbu zetu za Hansard zetu utakuweko tayari kujiuzulu nafasi yako ya unaibu Waziri?

b) Serikali kabla ya kujibu ningekuombeni mkafanya utafiti kwanza hivi sasa mahoteli yote karibu matupu na wanashindwa hata kulipa mifuko ya jamii, ulipokuwa unajibu swali la msingi unasema kuongezeka kwa wageni ambacho hicho kitu si cha kweli, baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Waziri naomba lete majawabu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Mwakilishi afahamu kwamba Sheria zinazotumika katika nchi hii zinatungwa na Baraza hili la Wawakilishi, na inapotokezea bahati mbaya kwamba Sheria moja imepewa nguvu upande mwengine na Sheria nyingine imepewa nguvu upande mwengine mgongano kama huu anaoueleza lazima utatokezea, ndio maana Wizara ya Habari na Utalii sasa hivi kwenye Baraza hili linaloendelea sasa hivi wataleta Mswada wa kurekebisha Sheria ya bodi ya Sensa, kuonesha kwamba kuepuka migongano inayotokea baina ya Sheria hii na Sheria nyengine, hiyo ndio jitihada inayofanywa na Serikali sasa hivi kuboresha masuala haya ya Sheria kutogongana na kuwa nguvu inafanywa katika mahala pamoja panapohusika, ndio maana tunafanya marekebisho katika mambo mbali mbali.

Kwa hivyo zile Sheria kugongana ndio zinafutwa hivi sasa, hapa Asubuhi Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais amesema kwamba leo pengine nitatunga sheria na kufuta ile Sheria ambayo pengine inapunguza nguvu kwa ajili ya sehemu nyengine, hata mimi upande wa ardhi imenigusa kidogo lakini sasa nguvu hiyo namuachia yeye katika kulinda mazingira hilo ni la kwao.

Sina hakika kama Mahoteli mengine ni matupu itabidi tufanye utafiti na hilo nakubaliana naye.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana baada ya majibu mazuri naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa sasa hivi duniani kote katika nchi ambayo ilikuwa mwanachama wa hiyo Miji Mikongwe *UNESCO* kama sijakosea ni sehemu ambayo hufanya mambo ambayo ya kuwavutia watalii kuja kuangalia hayo mahoteli na mikahawa.

Mhe. Waziri, je, kwa makusudi huoni iko haja hivi sasa Wawakilishi wako wote wa Baraza hili ukawachukua na kuwapeleka nchi za nje ili wakaona hali halisi ya mambo kama haya, lakini hiyo (b).

Mheshimiwa mimi nafikiri kuwa Sheria iwepo na kama haipo yaletwe marekebisho ya kuondoa mji ule kujengwa kwa tofali ili iendane na ijengwe kama ule urithi wa jiwe na chokaa, je, Mheshimiwa Sheria hiyo ni lini utaweza kutuletea hapa kwa kuweka sawa.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Wizara yangu kusema kweli haina uwezo wa kuwachukua Wawakilishi wote hawa kuwapeleka ulaya kwenda kutizama masuala haya, lakini nitakaposhirikiana na Baraza la Wawakilishi tutaliwekea fedha za kutosha basi kidogo kidogo tunaweza kuwapeleka wakaona hiyo hali, lakini kwa Wizara yangu peke yangu haiwezi kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Mji Mkongwe tunahitaji kuifanyia marekebisho na hilo suala halitachukua muda mrefu litaletwa katika Baraza hili, nayo kufanyiwa marekebisho vile vile.

**Nam. 20**

**Ujenzi wa Mabwawa ya Kuhifadhi Maji ya Mvua**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** – Aliuliza:-

Wenzetu nchi za jirani ya Tanzania Bara, wamekuwa na tabia ya kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi katika mashimo ya chini ya ardhi *(underground water tanks)* au kuyahifadhi katika mabwawa (malambo) na hatimaye kuyatumia kwa ajili ya kilimo, mifugo na matumizi mengine ya nyumbani. Kwa kuwa hapa Zanzibar hakuna utaratibu huo na badala yake maji ya mvua huachiwa yakapotea baharini na mengine kujikusanya kwenye madimbwi na mabwawa kama vile bwawa la Mwanakwerekwe Sokoni, bwawa la Darajabovu n.k ambayo huleta athari kubwa za kiafya na kimazingira na kusababisha maradhi yatokanayo na maji *(water borne diseases).* Na kwa kuwa ni dhahiri Serikali haina uwezo wa kuyatibu maji yale na kuweza kutumika kwa ajili ya matumizi ya binaadamu.

Je, ni lini Serikali itayaendeleza mabwawa haya kwa kuyajengea kuta madhubuti za kudhibiti maji *(retaining walls)* na hatimaye kufuga baadhi ya viumbe kama mamba, samaki aina ya Sato na Sangara ambao siyo tu watasaidia lishe lakini hata kuwa kivutio cha watalii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 20 naomba nitoe maelezo mafupi.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na hoja yake kwamba, teknolojia za uhifadhi wa maji ya mvua na kuyatumia kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uzalishaji kama vile kilimo, mifugo, ufugaji wa samaki, matumizi ya viwandani na hata ya nyumbani hutumika katika maeneo mengi duniani na hasa yale ambayo yenye upungufu mkubwa wa vyanzo vya maji na huleta tija kubwa, hasa katika suala zima la ufugaji wa samaki.

Serikali kupitia Idara ya Mazao ya Baharini pamoja na taasisi zake nyengine zimekuwa zikiwaelekeza wananchi, hasa wale wenye makaazi yao katika maeneo yenye upungufu wa maji kuvuna maji ya mvua kwa matumizi yao ya nyumbani na hata kwa ajili ya shughuli zao za uzalishaji, ingawa muamko unaonekana kuwa mdogo kutokana na kukosa mazoea ya matumizi na kutomudu gharama za uhifadhi wa maji hayo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 20 kama ifuatavyo:-

Kwa hivi sasa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, haijajipanga kuyahifadhi kwa kuyajengea kuta za kudhibiti maji *(retaining walls)* maeneo yenye kutuwama maji ya mvua kama vile bwawa la Mwanakwerekwe sokoni, bwawa la Daraja bovu n.k. kwa lengo la uanzishaji wa miradi ya ufugaji wa viumbe kama vile mamba, samaki aina ya Sato na Sangara kwa sababu zifuatazo:

a. Maeneo haya yamekosa sifa moja kubwa inayowezesha ufugaji endelevu wa viumbe kwa faida, sifa yenyewe ni kuwa na maji ya kutosha katika kipindi kizima cha mwaka. Ni cha maji ambacho zinatokana na mvua tu zinazokuweko kwenye mabwawa hayo ndio hujaa, na hupungua sana kiwango cha kaskazi ambapo kunakuwa na jua kali na ubora wake unatakiwa uwe na 1 na nusu ili kuweza kuwa na sifa za mabwawa kama haya, na inaonekana mabwawa mengi yanayotuwama maji kama hayo hamna.

b. Mhe. Mwenyekiti. asili za maji hayo ni nyingi na zisizo salama, mbali na maji ya mvua yanayodondoka moja kwa moja na kutuama katika mabwawa hayo, vyanzo vyengine vikubwa vya maji hayo ni michirizi

na mikondo yenye mchanganyiko wa maji ya majumbani, masokoni, majaani, magereji ya vyombo vya moto n.k ambayo mengi yamebeba uchafu wa aina mbalimbali ikiwemo taka ngumu *(solid wastes)* na zile za kemikali.

Maji yenye mchanganyiko mkubwa kama huu huondosha usalama kwa utumiaji wa samaki wenyewe hata na walaji kwa binadamu, kwani uchafu huo unaweza kuingia katika njia ya mfumo wa chakula wa samaki na kuwa chanzo cha maradhi kwa watumiaji na walaji hapa nchini.

Lakini kitu kama hichi kilifanyika nchini Japan na kikawaathiri walaji wale wa chaza waliokuwa wakifugwa na aina hiyo ilipatikana aina ya *Macury* ambayo iliitwa na Mata ambao ugonjwa wenyewe ulikuwa haujulikani kabisa kwa jina lake ikaitwa kwa jina la Mjuri.

c. Serikali inaunga mkono ufugaji wa samaki na uhifadhi wa viumbe ambao wako hatarini kutoweka kama vile kasa kwa lengo la uhifadhi wa mazingira na kujipatia kipato kupitia shughuli za kitalii, kwa kuwapa nguvu na kuwasaidia wananchi wenye muamko wa kufanya shughuli hizi hasa wale ambao tayari wanajishughulisha kama vile *" Nungwi Natural Aquarium"* waliopo Nugwi pamoja na wale wa Jozani kifedha.

d. Pia, Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi mtakubaliana na mimi kuwa; mipango yote ya uboreshaji wa maeneo kama haya yatahusisha moja kwa moja mamlaka za mipango miji na taasisi zinazohusika na usimamizi wa mazingira. Kwa hivyo kujenga sifa ya mchakato na mashirikiano baada ya kufanyia maamuzi ya Wizara yangu tu. Jambo hili linahitaji muda mrefu na sio kusema lini tunaweza kufanya hivyo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Asante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba niulize swali dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba hawategemei kuhifadhi maji yale na kuweka viumbe nilivyovitaja, kama mamba kama kivutio cha watalii kutokana na kwamba vyanzo vya maji yale sio salama, ukiachilia mvua inayonyesha ya moja kwa moja, lakini anasema vyanzo vyengine vinatoka katika mifereji ya maji machafu.

- Na kwa kuwa katika kipindi tulichonacho tuna mabadiliko ya tabia nchi, jambo ambalo hizi mvua zinakuwa hazitegemeleki na wakati mwengine tunazikosa sana.

- Na kwa kuwa katika nchi masikini sana zilizoko hasa huku Kusini mwa Jangwa la Sahara wana kitu wameanzisha water *treatment plants*, kwa hivyo maji yale wanayafanyia *treatment, then* wanakwenda kumwagilia katika miti na mengine yanarudi katika majumba tunakoga, tunafanyia shughuli nyengine na wala tukienda hata kule Ulaya hatujadhurika kwa sababu wanapoyafanyia *treatment* wanayarudisha tena majumbani kwa matumizi mengine.

Je, ni lini serikali itatatua tatizo la maji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuweka *special water treatment plants* zitakazoyarudisha maji taka kuwa maji safi na kuyarudisha katika matumizi kadhaa ya kadhaa ikiwemo, kuwapa mifugo, kumwagilia, pamoja na kutumia katika *round works.*

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, nimesema katika jibu langu la msingi kuwa, maji haya ni machafu lakini yanahitaji tafiti nyingi ambazo tunaweza tukazifanya. Lakini hata hivyo tutalichukua swali lake ili serikali iweze kulifanyia kazi kwa haraka iwezekanavyo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba kutumia Kanuni ya 39(3) kwa mujibu wa maswali kwamba bado ni mengi sana na vile vile yana umuhimu kwa Taifa letu. Tunaomba kuongeza robo saa kwa ajili ya kumalizia baadhi ya maswali halafu tutaendelea na taratibu zetu.

**Nam. 84**

**Sera ya Msamaha Kwenye Matibabu kwa Wasiojiweza**

**Mhe. Ali Salum Haji -** Aliuliza:
Kutokana na baadhi ya makundi kutomudu mchango wa matibabu, wenzetu Tanzania Bara katika kukabiliana na changamoto hii wameanzisha sera ya msamaha kwa baadhi ya makundi mfano wazee zaidi ya miaka 60, watoto chini ya miaka mitano, saratani na ukimwi.

Je, Zanzibar hatuoni imefika wakati wa kuanzisha sera hiyo ili kutoa unafuu kwa wananchi wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:
Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu sote kutujaalia tukiwa na afya na wazima na kutoa pole kwa wale wote waliopatwa na misiba mbali mbali pamoja na msiba wa Mzee wetu ambaye alikuwa mshauri wa Rais Mheshimiwa Almarhoum Issa Ahmeid Othman, natoa pole kwa familia yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulieleza Baraza lako la Wawakilishi rasmi, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, haikupata kufuta Sera ya Afro Shirazi Party (ASP) ya matibabu bure kwa wananchi wake wote wa Zanzibar. Sera hiyo bado ipo na inaendelezwa na pia inafanya kazi hadi hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, sera hiyo ilianzishwa mwaka 1964 na inaendelezwa hadi hii leo, licha ya kwamba wananchi wamekuwa mara kadhaa wamekuwa wakikabiliwa na mapungufu ya hapa na pale na kuhitajika kuchangia huduma za afya panapokuwa na mapungufu maeneo ya kwenye dawa ama vipimo, inabidi waende kwengineko kupata huduma kama hizo kwa malipo, na ndipo hapo uchangiaji unafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya hivi sasa inaendelea kuandaa miongozo mbali mbali juu ya uchangiaji wa huduma za Afya na hayo yalianza hata kabla ya wenzetu wa Tanzania Bara. Katika miongozo hiyo makundi maalum yameainishwa ambayo yatapatiwa misamaha mbali mbali katika kuchangia huduma za ziada za afya mbali ya zile huduma za kiwango cha kawaida ambazo zinatolewa bure. Makundi hayo ni pamoja na watoto wenye umri chini ya miaka 5, wazee wasiojiweza, walemavu wasiojiweza, watu wenye maradhi sugu mfano UKIMWI, Kifua kikuu na Saratani.

Hata hivyo, kwa wale wasio na uwezo bado wanaendelea kupata huduma za Afya kulingana na taratibu pamoja na sera yetu iliyokuwepo kwa huduma za matibabu mengineyo. Basi serikali bado itaendelea kuwahudumia kwa kuwalipia kwa matibabu ambayo hayatolewi hapa Zanzibar kwa Sera ile ile ya Afro Shirazi Party ya kupata matibabu bure. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Salim Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mhe. Waziri kwa kusema kwamba Sera ipo, lakini wakati tunatembelea Kamati tulitembelea hospitali za Tanzania Bara hivi karibuni, walitueleza namna Wizara inavyotumia bajeti katika kufidia Sera za wale watu ambao wanapata msamaha wa kodi hizi za matibabu.

Sasa nataka Mhe. Naibu Waziri wa Afya anieleze ni idadi ya watu wangapi ambao waliopindukia miaka 60 na watoto chini ya miaka mitano na Saratani ya Ukimwi ambao walipata msamaha kupitia Sera hiyo ya Afro Shirazi aliyoizungumza Mhe. Waziri na gharama kiasi gani Wizara imeweza kufidia kupitia maradhi hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, swali lake kidogo Mheshimiwa haliko wazi. Kwa sababu wenzetu kule Bara wana hospitali za aina mbili, kuna hospitali za serikali na hospitali binafsi. Nadhani amekusudia hospitali za serikali naomba aliweke wazi kwanza hilo ili niweze kuendelea kujibu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tunaomba Mhe. Mjumbe utuelekeze zaidi.

**Mhe. Ali Salim Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, swali langu liko hapa, kwamba pamoja na kwamba matibabu ni bure lakini kuna michango Wizara ya Afya inachangia. Kwa mfano mjamzito anaambiwa aende na mpira, au ukienda katika masuala la operesheni kuna michango pale unakuwa unaambiwa labda operesheni hii utachangia elfu 50,000/-. Kwa kupitia umri wa hawa wazee ambao nimewataja mimi ni wangapi ambao wamepata huduma hiyo na hiyo misamaha wakaipata na ni kiasi gani ambacho kimetumika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba tena nirudie kwa ufasaha kabisa na ninukuu hotuba za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Ali Muhammed Shein ambazo amekuwa akitoa mara kadhaa na amekuwa akizirudia pia kwa kuweka msisitizo.

Mhe. Mwenyekiti, mzazi hatakiwi kulipia huduma ya aina yoyote. Kumtoza gharama mzazi hilo ni kosa na naomba hilo kosa liripotiwe ili lichukuliwe hatua. Vifaa hivyo ulivyovitaja mfano mipira na vifaa vyengine vyote ambavyo anatakiwa mzazi vinapewa kipaumbele cha kwanza kabisa katika hospitali. Vifaa hivyo mimi mwenyewe nimekwenda kuthibitisha vipo katika hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja pamoja na hospitali nyengine *PSU Plus* ambazo zinatumika kwa ajili ya kuzalisha watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mtu yeyote ana ushahidi atuletee, tatizo kwamba tunazungumza lakini inapofika pahala pa kutoa ushahidi hakuna mtu anayekuja kutoa ushahidi ili mfanyakazi yule aliyetoza zile pesa achukuliwe hatua.

Kwa hiyo kama kuna tatizo hilo na kuna ushahidi basi tunaomba ushahidi huo uletwe Wizarani na daktari Mkuu ama Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja yeye mwenyewe ndiye anayelisimamia hilo Dokta Jamala Adam Twayb na ndiye anayelishughulikia hilo suala. Kama upo ushahidi wa mzazi kutozwa fedha kwa sababu hiyo ni kinyume na UNFPA ambao wanatusaidia katika huduma za mama na mtoto.

Kwa hiyo hilo naomba nithibitishe kwamba mzazi hatakiwi kutozwa gharama yoyote, wala hatakiwi kulipa kuanzia mipira mpaka jiki, mpaka vitu vyengine vyote. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Salim Haji:** Mhe. Mwenyekiti, kataja maeneo mawili amenijibu moja. Watu wanapokwenda operesheni kunakuwa kuna gharama ambazo tunatozwa kwa mfano unaambiwa operesheni hii itahitajika uchangie sh. 50,000/. Nalo katika eneo hilo pia nilijaribu kulizungumzia, katika hilo eneo la operesheni ni watoto wangapi *under 5 years* wamepata msamaha na watu wangapi wa miaka 60 zaidi wamepata msamaha wa kodi na ni kiasi gani ambacho msamaha huo umefanyika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna tofauti kidogo kuna zile huduma za *first track,* huduma zile zinakuwa na gharama zake ambazo zinatozwa na kama mtakuwa mmetizama vitabu vya bajeti iliyopitishwa mwaka 2014/15, hospitali ya Mnazi Mmoja imetakiwa kuchangia nusu bilioni katika ukusanyaji. Kwa hiyo huduma zile za *first track* ndio zinazokusanya kiasi cha shilingi nusu bilioni kwa mwaka. Hiyo ilipitishwa na Baraza hili hili la Wawakilishi katika huduma za *first track*. Lakini kwa huduma za kawaida mgonjwa hatakiwi kutozwa gharama wakati wa operesheni. Isipokuwa pakiwa na mapungufu ya dawa ambazo zinahitajika katika operesheni hiyo maalum pale mgonjwa hachangii pesa moja kwa moja, lakini huambiwa akanunue dawa zifuatazo na hupewa *prescription* ile ili apate kwenda kwenye duka la dawa kununua vile vifaa ambavyo vinahitajika katika operesheni ile, panapokuwa hakuna vifaa hivyo katika operesheni ile.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu mazuri sana na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri pamoja na kauli ambayo anaitoa ya serikali kuhusiana na suala hili la wahudumu katika kuuza au kuwatolesha wazazi vifaa hivi vya uzazi.

Mheshimiwa mbali na majibu haya nataka kujua kwamba inapotokea kwamba muhudumu au daktari yeyote amemtolesha au kumuuzia au mzazi yeyote katika kutoa huduma hizi za uzazi, je, ni adhabu gani inachukuliwa au itachukuliwa kwa daktari au muhudumu yeyote anapomuuzia mzazi vifaa hivyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa huduma zozote zile halali zinazotozwa fedha ndani ya hospitali zetu zote, basi kuna risiti maalum ambayo imewekwa. Mnazi Mmoja wao ndiyo wana risiti yao wenyewe yaani kama Mamlaka ya Hospitali ya Mnazi Mmoja anatakiwa yule mgonjwa kudai risiti na kupewa. Pindipo ikigundulika muhudumu, muuguzi, ama daktari amemtoza gharama yule mgonjwa kinyume cha sheria mfano mzazi au kuchukua pesa moja kwa moja yeye mkononi bila ya kutoa risiti, basi sheria za utumishi zinatumika katika hospitali hiyo.

Kabla ya kwenda kwenye sheria za utumishi moja kwa moja kuna Bodi ya madaktari ya uongozi ya hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja ambayo hukaa na kulijadili lile tatizo. Ndio maana hapo awali nikasema kwamba pakiwepo na ushahidi na ule ushahidi ukiletwa basi ule ushahidi unafanyiwa kazi pale pale hata kabla ya kufika kwenye Sheria Kuu za Utumishi, kwa sababu kuna Sheria zile za ndani ya Mamlaka ya ile Hospitali ambazo zinatumika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, kwa siku nyingi hapa Mhe. Waziri wa Afya sijakuona, nimekuona leo, sijui ulikwenda kututafutia madawa au matibabu mengine kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, nikupe pole sana.

Vile vile Mhe. Naibu Waziri hichi chombo ni cha wananchi pasingekuwa na chombo hichi nafikiri serikali isingekuwepo, serikali ndio wananchi. Sasa haya majawabu mkaja mkayatoa wananchi wanatusikiliza. Hichi unachokizungumza sasa hivi sawa sawa na kusema nguruwe haramu lakini mchuzi wake unaunywa. Unasema Sera ya Afro Shirazi ni yenye matibabu bure, sikatai ni kweli lakini kutoka mtu akaenda pale Hospitali ya Mnazi Mmoja anataka kutibiwa mguu akapewa orodha kubwa ya kwenda kununua vifaa, huoni ni sawa sawa na kwenda kununua ndio matibabu bure.

Ndio ile ile tukaja tukapiga kelele hapa Mhe. Juma Duni, akakataa kuwa wananchi wanabeba mimba ya miezi tisa, haijulikani mimba ile kama kufa au kupona au ya kisu, lakini kwa unyenyekevu wa hali ya juu Mhe. Rais kwa kujali wananchi wake ada ile akaiondoa.

a) Huoni ni kulidanganya Baraza na uko tayari kujiuzulu kama nikikuletea mifano mitatu ya wananchi waliotibiwa kwa kutozwa pesa.

b) Kwa kuwa suala la afya ndio injini ya maendeleo ya nchi, lini serikali itatoa vipande maalum kwa wananchi wasiojiweza kupata huduma hiyo serikalini au kwenye sekta binafsi.

c) Uko tayari kujiuzulu Mhe. Naibu Waziri nikikuletea risiti zaidi ya watu watatu waliogharamia shilingi laki tatu, laki nne kwa kutibiwa miguu na wengine kutiwa vyuma.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kunipa pole ya safari na matokeo yake atakuja kuyaona hivi karibuni katika maswali yanayofuata na atajua nini ambacho tumekwenda kuomba kwa wenzetu na nini tutafaidika kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, katika kujibu swali lake Mheshimiwa Mjumbe naomba kwanza niseme kwamba tutafautishe huduma za afya kwa mafungu mawili. Fungu la kwanza ni ile kwenda ukapata daktari ukamuona akakutibu. Hilo ni fungu la kwanza, hapo anakuwa hajakupa dawa yoyote wala hajakuandikia dawa, lakini amefanya vile vipimo daktari vya kutizama wewe una tatizo gani.

Fungu la pili ni pale anapokuandikia *prescription* ili ukapate zile dawa zenyewe ama vipimo ambavyo wewe vinatakiwa vikutibu. Sasa kama zile dawa hazipo, kwa sababu katika uagiziaji wa madawa Sera ya Serikali inasema kuna zile *essential drugs* ambazo ni dawa muhimu sana, halafu zile dawa za kati na zile dawa za maradhi ya kawaida. Sasa hizo *essential drugs* ndio fedha zinapopatikana mwanzo kabisa huagiziwa *essential drugs,* halafu zile *necessary* halafu zile dawa za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama umeandikiwa na *list* yako haina zile *essential drugs* ina nyengine na hakuna pale hospitali, pale ndio unapotakiwa na cheti chako kwenda kununua zile dawa dukani kama kawaida, kwa sababu hakuna huduma ile pale hospitali. Hutozwi hata siku moja hospitali kwenda dirishani ukawa unalipa ukapewa dawa na kama ushahidi huo unao Mheshimiwa mimi nitakuomba uniletee ili tuchukue hatua. Hatua hizo tutachukua kabla ya watu kujitangaza kujiuzulu wala nini, zitachukuliwa hatua zitaonekana hizo hatua.

Upande wa pili wa swali lako, pale ambapo huduma mfano ya wale wanaovunjika miguu huwa inahitajika huduma ya kuchukua daktari kutoka nje kumleta pale au kuchukua msaada kutoka nje ya hospitali kumleta pale, tunashirikiana na wenzetu, basi huduma zile serikali huchangia katika mfuko wake na pindipo pakiwa hakuna bajeti hiyo na yule mgonjwa anahitaji kufanyiwa operesheni muhimu basi tunakaa pamoja na familia katika kuamua vipi operesheni ile ifanywe na kiasi gani kichangiwe.

Lakini hapo hapo pana huduma ya *social service* ambapo pana Ofisi pale pembeni ya Chumba cha *City Scan* hao kazi yao huwa wanapokea wagonjwa wale waliokuwa hawana uwezo kabisa, wala hawana dawa iliyopatikana na dawa zile hazipo hospitalini, basi kuna fungu maalum ambalo hutolewa wagonjwa hao wakaenda kupatiwa fedha hizo na kuweza kununuliwa dawa hizo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 85**
**X-ray za Dharura Wodini**

**Mhe. Ali Salum Haji -** Aliuliza:

Baadhi ya wagonjwa wanaolazwa wanakuwa na hali mbaya na hutokea kuhitaji X – Ray na huleta usumbufu wa kubebwa na kupelekwa chumba cha X–Ray.

Je, ni lini hospitali ya Mnazi Mmoja itaweka X–Ray za dharura wodini ili kukabiliana na changamoto hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kwahani swali lake Nambari 85 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya tayari imeshaliona tatizo hilo na hivi sasa imo mbioni katika kulitatua lakini kwa hatua ya mwanzo tayari tatizo hilo limeshatatuliwa kwa kununua kwa kununua *mobile x-ray* iliyoigharimu Wizara ya Afya dola 31,000 za Kimarekani ambayo inatumika kwa wagonjwa mbali mbali wenye hali mbaya na wasioweza kuhamishika hasa wale wenye *traction* yaani miguu yao iliyotiwa vyuma na kuvutwa wasiohamishika kutoka kwenye wodi, kutumika huko huko wodini na pia huduma hiyo inatumika katika chumba kikuu cha *x-ray.*

Changamoto tuliyonayo Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kweli tuna upungufu wa *x- ray,* kwa sababu *x-ray* hiyo ni *mobile* inatakiwa itumike kwenye wodi zaidi lakini inatumika kote wodini na kwenye chumba cha *x-ray* na mara nyengine huwa wagonjwa wa *x-ray* ni wengi zaidi kuliko uwezo wa ile mashine. Tuko mbioni kuleta katika bajeti ijayo na Waheshimiwa Wawakilishi mtaiona tunataka kununua *x-ray* mpya kwa ajili ya chumba kile kikuu cha *x-ray*. Kwa sababu ile iliyokuwepo tayari imeshapitwa na muda wake haifai tena kutumika kwa sababu inatumia *system* ya kizamani ya kuchanganya madawa na kadhaliki. Sasa hivi ni kama *printer* tu unakwenda moja kwa moja kuna *tonner* inatoa picha moja kwa moja.

Kwa hivyo tutaileta katika bajeti ijayo ili tununue *x-ray* mpya lakini kwa sasa tunatumia hii *mobile x-ray* kwa ajili ya wodini na kwa ajili ya chumba kikuu cha *x-ray*. Na bahati nzuri wenzetu waliotujengea *ICU* pamoja na miradi mengine mbali mbali ya ORIO na kwa kule Pemba wao wote wana *individual x-rays* zao ambazo zinatumika katika vitengo hivyo.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nishukuru majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kwanza namuomba tu mbio zake zisiwe za *marathon* ziwe mbio fupi ili tuweze kutekeleza mambo haya kwa haraka sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimuulize swali dogo tu Mhe. Waziri, kwa kuwa yuko mbioni kuleta bajeti mwaka huu, na kwa kuwa uwezo wa Serikali tunaujua ni mdogo, je, haoni kuna haja ya kuishawishi Serikali kutumia hali ya dharura kunusuru maisha ya wananchi wa nchi hii kama tulivyotumia hali ya dharura kununua meli.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, bado hatujafikia *stage* kama hiyo ya haja ya dharura kwa sababu mashine hiyo bado inatumika na inaendelea vizuri. Tukifikia *stage* hiyo ninaamini na Waziri wa Fedha yumo humu ndani na hilo kalisikia, aghlabu mara nyingi Wizara ya Fedha huwa inatupa *priority* Wizara ya Afya *priority* ya juu kabisa panapotokea haja yoyote au maradhi ya miripuko au pale ambapo pametokezea ajali katika nchi kama vile wakati ule wa *MV Skagit* na *Spice Islander*. Wizara ya Fedha ilitoa kipaumbele maalum kwa shughuli hizo. Tutakapofikia *stage* hiyo ninaamini tutashirikiana nao tutaweza kufanikiwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali pamoja na muda wa nyongeza umemalizika, sasa tunaendelea na taratibu zetu nyengine.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mswada wa Sheria Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea, na siku ya Ijumaa tulimalizia kwa Mhe. Hamza Hassan Juma na akabakisha dakika zake chache lakini pia simuoni hapa, sasa ninayo orodha ya wachangiaji wengine watano, tutaanza na Mhe. Abdalla Juma.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kusema mawili matatu katika Mswada huu wa kuanzisha taasisi ya ulinzi ambayo katika kamati imependekeza kwamba iwe Taasisi ya Ulinzi lakini tuiite Wakala wa Ulinzi na tulipendekeza hivyo kwa makusudi kwa sababu JKU iko chini ya Taasisi muhimu sana ya Serikali, Idara Maalum.

Na tulivyojaribu kuuona huu mswada kama kwamba unaanzisha chombo ambacho ilikuwa kina muelekeo wa kufanya biashara hizi. Sasa tukasema basi kwa kuwa iko chini ya Serikali na kwa vyovyote vile waajiriwa ambao watakuwa katika Taasisi au wafanyakazi wataokuwa katika nafasi watakuwa wakipata mafao yao ya mishahara na mengineyo kutoka Serikalini, kwa hivyo nitahusisha Serikali moja kwa moja na kwa hivyo isiwe inafanya biashara, kwa sababu Serikali au Taasisi za Serikali haziwi zinafanya biashara zaidi huwa zinatoa huduma.

Kwa hivyo tukapendekeza kwamba badala ya kuitwa Taasisi au Shirika kama ambavyo imeonekana katika huu mswada sasa tuite Wakala wa Ulinzi, maana yake wakala unakuwa wa Serikali moja kwa moja na hata sheria za wakala wa Serikali zinatofautiana sana na sheria za makampuni au *authority* nyengine ambazo zinakuwa zinajitegemea.

Sasa Mhe. Mwenyekiti nataka niseme kwamba nchi yetu Zanzibar na ukiangalia *population* yake ina watu 1,302, 000 sijui 1,300,400 kama ambavyo jana tulikuwa tunapokea taarifa za watu wa sensa. Na bahati nzuri sana tunaweza tukasema Wazanzibari tumebahatika sana kuliko nchi nyingi sana za dunia kwa kuwa na walinzi wengi, maana yake tuna Jeshi la Ulinzi linatulinda sisi na Jeshi la Polisi linatulinda sisi.

Tuna Idara Maalum 5 za SMZ ambazo nazo zinatulinda sisi, kwa kuwa si mwanajeshi siwezi kuona ndani yake huko kuna askari wangapi kutoka kila chombo katika hivi vyombo 7 hivi nilivyovitaja lakini ninaamini tuna utajiri mkubwa sana wa walinzi. Na kwa msingi huo basi, tungetizamia sana kwamba vikosi hivi vitajipanga vizuri tungetizamia sana kwamba matukio kama tukio lililotokezea juzi pale Darajani ingekuwa ni kutokea kabisa. Kwa sababu kwa ulinzi huu ninaamini mhalifu hawezi kwenda hatua hata 20 kabla hajakutana na mlinzi wa wananchi.

Sasa matokeo kama haya yakitokea kwa kweli huwa wengine tunajiuliza maswali mengi kwa kweli, kwamba vikosi hivi havijajipanga vizuri au kuna tatizo la sera au tuna tatizo gani kwa kweli, lakini tusingetarajia kabisa kama sheli zetu za mafuta zinakwenda kuvamiwa watu wanaiba pale tena wanaiba na wanafanikiwa kuondoka. Maduka yetu pale kuna wafanyabiashara wajasiri amali pale Darajani mara nyingi ndio *target* ya wahalifu tusingetarajia kabisa kama matukio haya yatokee pale wakati ukiangalia pale Darajani yenyewe imezungukwa na walinzi watupu, kila upande unaoelekea huendi mita mia moja kuna kituo cha ulinzi. Kwa hivyo mimi nadhani *point* yangu ya kwanza ni kuinasihi Serikali hivi vikosi hivi tuviweke vizuri ili wananchi wapate faida ya kuwa na walinzi wengi kuliko watu wengine duniani, ukifanya *ratio* hapo Wazanzibari watakuwa wanalindwa na askari wengi zaidi kuliko watu wengi kama si watu wote duniani, bahati, lakini kwa nini uhalifu utokee. Kwa hivyo nadhani kuna haja ya Serikali kuliona hilo na wakavipanga hivi vikosi kiasi ambacho viweze kuwasaidia watu zaidi na watu waweze kuishi katika hali ya usalama zaidi.

Zanzibar ni nchi ya utalii na utalii ni sekta moja muhimu sana kwa Zanzibar ambayo inatusaidia kuinua kipato chetu cha nchi na utalii ni biashara moja *flexible* sana, ikiwa hali ya usalama imetetereka kidogo biashara ya utalii ni kama ndege mjanja anakimbia. Kwa hivyo kuanzishwa wakala huu ambao kwa mujibu wa mswada huu madhumuni makubwa ni kuweza kuboresha katika maeneo haya ya *investment*.

Kwa hivyo hebu tujitahidini baada ya kuwa na sheria hii ambayo itatusaidia kuweka usalama wa kutosha, kwa sababu kwa mujibu wa sheria hii wakala huu utakuwa ndio mratibu wa hata taasisi za ulinzi katika maeneo hasa haya ya *investment*, kwa hivyo nadhani tukijipanga vizuri wawekezaji katika sekta ya utalii watakuwa hawana wasiwasi na usalama wao na wataweza kuwekeza vizuri zaidi ili tufaidike basi na *income* hii ambayo inapatikana kupitia utalii.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo nimesema niiambie Serikali kwamba vikosi hivi hata ukisoma sheria zao kama JKU kama linavyosomeka hilo jina lake JKU ni Jeshi la Kujenga Uchumi na hata lilipoanzishwa lilikuwa na madhumuni hayo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hii miaka ya karibuni inaonekana vikosi hivi vilikuwa vinatumika vibaya kidogo, vilikuwa vinatumika vibaya na walikuwa wametolewa maana yake hawakutoka wao wametolewa kwenye lile lengo na madhumuni ya kuanzishwa na matokeo yake vikawa vinaingizwa sana kwenye siasa, jambo ambalo mpaka baadhi ya wananchi walianza kupoteza matumaini na imani na vikosi.

Kuna kipindi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Nilipokuwa nikitoa *speech* yangu nilikuwa nikiwakandia kweli kweli, sana sana nilikuwa ninawasema vibaya mpaka wenyewe wakasema kama hakuna mtu mkorofi kama huyu Abdalla Juma, lakini kutokana na matumizi mabaya ambayo vikosi hivi vilikuwa vinafanya hapa tulipokuwa katika Serikali ya Umoja ya Kitaifa kidogo mambo yalikuwa yanabadilika. Ukienda kwenye vikosi ukiangalia mipango yao unaweza ukasema kumbe hawa watu wana mipango mizuri ya kuendeleza nchi lakini tatizo ni matumizi ya wanasiasa.

Sasa nawaomba sana wanasiasa wenzangu hebu tuviachie hivi vikosi vifanye kazi ya ulinzi na huduma nyengine kazi za kuimarisha uchumi, wana mambo mengi sana ya kufanya hawa hawako *free* kabisa, wana mambo mengi kweli kweli ya kufanya tusiwafanye waache shughuli zao waje wafanye kazi ambayo kwa kweli haistahiki na inaleta matatizo katika nchi. Nafikiri kusema hivyo wataalamu wa kutafsiri maneno wanaweza wakafahamu kile ambacho nakusudia.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti,  humu ukiangalia kwenye mswada kuna kifungu cha 7 ambacho hiki kinatoa uwezo kwa hii taasisi inayoundwa, uwezo wake wa kiulinzi na inasema hiki kifungu cha 7 Taasisi ya Ulinzi itakuwa na uwezo wa mambo mengi lakini ninakusudia (a) (b) (c) hasa inasema itakuwa na uwezo wa kukamata na kupekua sehemu au mali yoyote inayoshukiwa au mtu yeyote aliyevunja kifungu chochote cha sheria hii au sheria nyengine na kumfikisha kwenye mamlaka inayohusika.

Sasa ukisoma sheria ya *Criminal Procedure Act* ambayo ni sheria *very common* katika nchi yetu ambayo hata Jeshi la Polisi na Taasisi nyengine za Ulinzi wanapaswa kuitumia ile sheria katika kutekeleza *arrest,*  ile sheria Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kifungu cha 14 sina hakika uzuri nafikiri Mwanasheria Mkuu unaweza kunikosoa kidogo, ukisoma kifungu cha 14 kinaeleza *procedure* za ukamataji na kumuweka mtu chini ya ulinzi, kuna taratibu zake na kinasema kile kifungu au askari akitaka kumkamata mtu aliyetuhumiwa kutenda kosa fulani anatakiwa afanye mambo mawili.

Jambo la kwanza ajitambulishe yeye kama ni askari maana siku nyengine anaweza akaja na uraia kwa hivyo ajitambulishe yeye kwanza kama ni askari mwenye namba kadha kadha wa Taasisi fulani. Kwa hivyo yule mtu ajue kama huyu aliyeko mbele yangu sasa hivi huyu ni askari, la pili amsomee yule anayetaka kumkamata tuhuma ambayo anatuhumiwa nayo. Bwana mimi ni askari jina langu fulani mwenye namba kadha kadha kadha ninakuweka chini ya ulinzi wewe kwa sababu ya tuhuma kadha kadha kadha, sasa wakati huo kama mtu atabisha atakuwa anavunja sheria, lakini unamwendea mtu ukifika kwanza gongo mpaka chini, halafu unamnyanyasa unavyotaka kinyume cha sheria kwa sababu hujaambiwa wewe umpige mtu gongo wakati haja-*resist* kukamatwa. Sasa hayo Mhe. Mwenyekiti yanatokea katika nchi yetu, na kwa sababu ya kukosa *procedure* za ukamataji ndio ule uhasama kati ya raia na vikosi vyetu ya ulinzi unatokea.

Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwa tunafanya uchaguzi mdogo wa Bububu mimi nilikuwa pale mbele ya Kituo cha Beit el Ras ilikuja gari ya kiraia kabisa *pick up* rangi ya *gray* waliokuwemo mule ndani walikuwa na bunduki lakini wamevaa uraia halafu wamevaa yale madubwasha gani yale ya kuziba uso maninja yale kama yale masoksi makubwa kalitoboa macho kavaa yale. Wakashuka pale na bunduki wakakamata watu wakawapiga vibaya kweli kweli halafu wakawatia kwenye gari wakawachukua. Sasa mimi nikawa ninajiuliza sasa hawa ndio wanafanya nini. Kwa sababu kama ni askari walitakiwa wajitambulishe wakisha kujitambulisha na wale watu wawasomee makosa yao sio wamkamate.

Mheshimiwa nazungumza ndani ya mswada kifungu cha 7(c) *procedure* za kukamata ndio ninazungumza sifanyi jambo jengine. Nazungumza *procedure* za kukamata zinavyokiukwa katika nchi na kusababisha kero, kwa hivyo naomba sana kifungu hiki cha 7 hawa askari watakaoajiriwa bila shaka watawa-*arrest* watu, hiki kifungu kinawapa uwezo askari hawa kuwa-*arrest* watu, kwa hivyo wawa-*arrest* kwa mujibu wa sheria za nchi, *Criminal Procedure Act* inasema wazi, ukitaka kumkamata mtu ufanye nini, naomba hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu tuliujadili kwenye kamati vya kutosha yale mambo ambayo mengi ambayo niliya-*mark* kwa ajili ya kuuboresha, tulikubaliana na wizara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kule kwenye vikao vya kamati, kwa hivyo na kwa kuwa Mhe. Waziri hapa anataka kupata njia apite, nadhani mimi nataka niishie hapo na niseme tu kwamba mswada huu naukubali kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**KUHUSU MUONGOZO**

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Hiyo nini niliyoleta ilikuwa ni Salma Mohammed Ali.

**Mhe. Mwenyekiti:** Alaah! Haya Salma Mohammed Ali, tuendelee Mheshimiwa.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na nikaweza kusimama hapa. Pili, nakupongeza wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwa juu juu madhumuni ya huu mswada utaona ni jambo litakalosaidia, lakini mimi nina hofu kubwa. Kwanza Vikosi vya Idara Maalum tulivyonavyo sio haba. Tuna Kikosi cha KMKM, Kikosi cha Mafunzo, Kikosi cha JKU, Kikosi cha Zimamoto na Kikosi cha Valantia. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 bajeti ya kawaida ya vikosi kwa jumla ilikadiriwa kuwa zaidi ya shilingi bilioni 37, KMKM ilikuwa ni bilioni 12.26, JKU ilikuwa bilioni 9.48, Mafunzo ilikuwa bilioni 7.49, Zimamoto ilikuwa bilioni 3.79, Valantia ilikuwa bilioni 4.66.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ukisoma sheria zote zilizoanzisha idara hizo pamoja na malengo yao mahsusi, lakini kwa ujumla utakuta jukumu lao ni la kulinda, na ndio maana tunavipongeza vikosi vyote kushiriki panapohitajika kulinda usalama.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika hali hiyo je, Mhe. Waziri ana maelezo gani ambayo yataweza kunishawishi mimi nikubali kuongeza kikosi kingine cha ulinzi wa utalii tu kuwa ni jambo la maana. Mhe. Mwenyekiti, mbali na vikosi vya ulinzi tulivyonavyo vya idara maalum, lakini tuna jeshi kubwa la ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia Mhe. Waziri anifahamishe kikosi hiki kinakusudia kufanya kazi vipi? Kama *watchman* wa kulipwa na mahoteli, viwanda au maduka ya watu binafsi au vipi, namuomba Mhe. Waziri hapo anifahamishe. Sasa ikiwa ni hivyo, watalii wanaopita kwenye mitaa na maeneo mengine ni kikosi kipi kitachowalinda? Mhe. Mwenyekiti, mwaka juzi watalii walitiwa tindikali na ikawa zogo sana hapa, sasa naomba Mhe. Waziri anifahamishe hawa watalii wanaopita kwenye mitaa mengine watalindwa na kikosi gani? Na kwa vile maeneo haya Mhe. Mwenyekiti, hayana biashara kama mahoteli. Je, watakaowalipa walinzi hawa ni akina nani? Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, jambo ni kwamba wawekezaji wanapokuja hapa nchini kwetu huwa tunawaambia kama nchi yetu ni salama sana. Sasa je, tutakapoanzisha kikosi hiki cha walinzi wa kulipwa na wawekezaji wakalazimika kulipia usalama wa uwekezaji wao, kwa kulipia walinzi wa kikosi cha serikali. Je, Mhe. Mwenyekiti hili litakuwa ni sahihi? Naomba pia nipate maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba niseme kifungu cha 37 (1) cha mswada huu mimi siwezi kukikubali, maana yake walinzi hawa ambao ni kikosi cha walinzi wa kulipwa hata wafikie pahala waue mtu. Mhe. Mwenyekiti, halafu wasiweze kushtakiwa, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, jambo hili halikubaliki. Na hili Mhe. Mwenyekiti, linanikumbusha mwaka 1992 kule Shumba Mjini, ambapo mtu mmoja alikuwa akipandisha bendera ya chama katika Tawi la CUF, aliuliwa kwa risasi na pale aliambiwa yule hawezi kushtakiwa askari kwa sababu alikuwa katika majukumu yake. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinaweza kutumika vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikae nisubiri majibu ya Mhe. Waziri ili nipate nifanye maamuzi juu ya mswada huu. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu angalau mdogo katika hii hoja iliyoko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umeletwa kwa hali ya dharura, mimi nimepata wasi wasi Mheshimiwa, ni dharura gani iliyopo katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015, haraka haraka pakaletwa mswada huu ambao utawaruhusu baadhi ya vijana kukamata silaha na kuanza kuwahenyesha wengine. Ni udharura gani uliopo Mheshimiwa? Mimi napata wasi wasi sana, serikali kuleta mswada huu kwa njia ya dharura, ina nia mbaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, kama ni suala la ulinzi katika nchi hii, ulinzi tunao wa kutosha sana, tuna Jeshi la Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tena liko makini sana jeshi hili katika kutulindia mipaka yetu na nchi kwa ujumla. Nampongeza sana *CDF* kwa kuweza kulitayarisha jeshi hili kwa ulinzi wa nchi, na juzi juzi hapa palitokea mambo ya mipaka tu pale *Lake* Malawi, kwa kweli jeshi lilipiga jaramba tu mimi huku nikaanza kujificha. Kupiga jaramba tu pale kwenye *Lake* Malawi baada ya ile *statement* ya Rais wa kule kwamba eti sisi hatukuhusika, basi mimi nilifurahi sana kwamba jeshi liko makini mno katika kulinda mipaka na nchi yetu.

Aidha, tunalo Jeshi la Polisi linatulindia sana mali zetu pamoja na sisi raia. Juzi tu hapa kuna jamaa waliiba shamba, walianza kuwatimua kuanzia shamba wakaja wakawakamata hapo Mjini, na wakawahenyesha na wakawaweka katika vyombo vya sheria.

Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa ya kutulinda sisi, raia na mali zetu leo inaletwa hati ya dharura eti kuwepo na kikosi maalum kitakacholinda yaani kinachomilikiwa na JKU kinatakacholinda utalii. Pana nia nyingine hapa Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana. Na kwa kweli tunawavunja moyo hata hawa Jeshi la Polisi kwamba kazi yote ile nzuri wanayoifanya kutulindia mali za watalii na kazi yote mpaka juzi wametuonesha pale. Leo mnataka kuwatilia kikosi kingine kulinda watalii kama wao hawawezi kazi, basi wanaiweza Jeshi la Polisi huu mswada haufai.

Mhe. Mwenyekiti, napata wasi wasi sana kutokana na nchi ilivyokuwa uchumi wake ni dhalili, Zanzibar eti tuko katika *population.* Hakuna mantiki ya kuleta hii. Hakuna mantiki hata mtu kama hajenda shule anajua kwamba mswada huu una nia nyengine, sio hii ya ulinzi wa utalii.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana *population* ya 1.3 million, yaani sisi *population density* yetu Zanzibar ni milioni 1,300,000. Tuna Jeshi la Wananchi, tuna Jeshi la Polisi, tuna vikosi vitano vya Zanzibar ukija ukifanya mchezo itakuwa kila mtu analindwa na askari watatu, raia mmoja analindwa na askari watatu, naona kitu kama hicho itabidi kiwe. Ukiwakusanya majeshi ya wananchi, uwakusanye mapolisi, ukusanye na vikosi uje uwaweke kwa watu milioni 1,300,000 utakuta kila mtu analindwa na askari watatu huku nyuma yake, raia mmoja analindwa na askari watatu. Huku nyuma yake una haja gani mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, huku ni kupoteza fedha za walipa kodi wa nchi hii, kabisa kabisa nachelea kwamba leo tukiupitisha mswada huu ukapita kwa ajili pengine ya matakwa ya watu binafsi kutokana na uchaguzi unaokuja mwaka 2015 Oktoba pale, kesho kutwa tutaanzisha mwengine wa ulinzi wa mawaziri *Ministerial Guard*, baada ya muda tutaanzisha wengine wawe kwa ajili ya *State Guard* ukija ukiangalia uwezo wa nchi hapana.

Mimi nimeangalia wenzetu baada ya *thorough feasibility study* wenzetu katika nchi hizi za Falme za Kiarabu wana majeshi, na vikosi vingi. Lakini vikosi hivi vinajitegemea vyenyewe kwa bajeti zao, kwa mfano kuna *State Guard* katika hizi nchi za Falme za Kiarabu halafu kuna *Royal Guard*. Lakini *Royal Guard* inajitegemea wenyewe wala haitegemei bajeti ya serikali ya nchi ile, leo tutoe ruzuku sisi tunataka kuanzisha kikosi hiki ni tatizo siungi mkono hoja hii Mheshimiwa mia kwa mia.

Mimi nadhani Mheshimiwa mswada huu urudi serikalini, ukisharudi serikalini utushirikishe wadau pamoja na sisi watalaam katika mambo ya watu ili tuweze kutoa mawazo yetu, hakuna hati ya dharura haraka haraka ya kuletwa wala sisi wataalam katika masuala ya jamii hatujashirikishwa na wadau wengine kutoa mawazo, mnatujengea hofu kwamba huu mswada hauna nia nzuri kwa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, niende ndani ya mswada sasa. Mheshimiwa kama utaangalia kifungu hiki cha 1 cha mswada huu kinachoongelea suala la jina fupi, kinasema. Sheria hii itajuulikana kama Sheria ya Taasisi ya Ulinzi ya JKU ya mwaka 2015. Sasa ukiangalia hili jina pamoja na huu muundo wa taasisi katika kifungu cha 4 muundo wa taasisi hapa basi utaona wewe mwenyewe kwamba huu mswada uko *bias,* kwa sababu umeshirikisha JKU peke yake. Mimi nadhani kama mswada huu ukisharudi serikalini na tukiitwa wadau uandikwe tena, kwamba sheria hii inajuulikana kama sheria ya Taasisi ya Ulinzi na Biashara.

Kwa hivyo, paongezwe neno "na biashara" isiwe *military oriented* iwe *business oriented* na hapa ndio mtaisaidia serikali, hebu tuangalie wale wenzetu kule Tanganyika wameanzisha ile SUMA JKT. Mheshimiwa pale wale wamekuwa *well equipped military economical*, nyinyi mnakuja na sheria hapa ili tukipitisha haraka haraka hapa ni tatizo.

Mimi nimetembelea katika kambi ile ya JKT Ruvu, mimi na kamati yetu ile ya Viongozi Wakuu wa Serikali, wale jamaa wamekuwa *well equipped* wamejiweka katika mambo ya biashara, mambo ya kilimo na mambo ya ujasiriamali. Unamkutia mtu mle anaingia na anatoka akiwa amewiva kijeshi, amewiva katika mambo ya *entrepreneurship*, na amewiva katika masuala ya kilimo, wale wanazalisha kilimo, mifugo na kadhalika.

Mimi nimetembelea katika sehemu ya mifugo ile *system* walionayo nimeiona Ulaya tu wakati niko pale kipindi kile mwaka 2001, nilikwenda pale nikaona kuna *battery charge system* ya *port kipping* wamekuwa wanafuga kuku kwa kila kuku ana chumba chake, anahudumiwa vizuri. Leo wale wanalinda lakini vile vile wana mambo kama hayo, wana maeneo ya kufanya *welding*, wana mashule, yaani kuna shule za JKT kule katika *business oriented,* utashangaa sana kila mtu anapenda zile shule. Eti sisi tunaanzisha taasisi ya ulinzi ambayo ni wakala wa serikali inalinda utalii au wageni huku wakulima wa mikarafuu waliopo katika mashaka ya Mabopwe sehemu za Kidundo kule Mtambwe, sehemu za Nanguji huku Kusini, sehemu za Bogoa wako misituni na mIkarafuu na mahela mengi, leo tunaenda kumlinda Mtaliana eti tunamuundia taasisi mtaliana.

Mkulima wa karafuu asijiingie *this is bias,* tena *criminal bias* inasikitisha sana kwamba sisi raia tunatengwa, anapewa hadhi mtaliana aliye na hoteli ya kitalii kule. Sisi mchuma karafuu ambaye yuko Bogoa na vibarua huku akiwa na mamilioni ya shilingi. yeye halindwi. Huu ni ubaguzi mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu usije unatubagua.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mswada huu unabagua sana na unaweza ukatuletea majanga katika nchi, huu muundo wa taasisi kwa sababu haukuwekewa biashara, taasisi hii italinda ndio itakayokuwa wakala wa ulinzi. Hebu tuangalie jamani nyinyi kuna Wamasai wametoka kule wanakuja kulinda hapa wanapata ajira hapa. Kuna Wapemba tumetoka Bogoa, sehemu za Nanguji, Vitongoji kule, tupo tunalinda katika vijiji, UMAWA wanalinda vizuri na wao wale maskari wastaafu, unaleta taasisi hii unawaondosha.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unakwenda kinyume na yale malengo ya serikali ya SMZ, mbona muna *contradiction* katika serikali nyinyi hamuangalii tumejipangia vipi. Tume-*create* ajira nyingi za ulinzi, mnakuja kuziondosha, sisi tukitunga mswada huu tunaziondosha zile ajira za UMAWA, hawa UMAWA ni askari wastaafu, hawa mnawaondoshea ajira. Hawa *Ultimate Security* wataenda wapi tena ajira zitapatikana wapi?

Mhe. Mwenyekiti, mnataka kutusababishia zogo la watu waliokuwa hawana kazi, wizi uongezeke katika nchi, Waheshimiwa mimi nawanasihi kama mtaalam, nawanasihi kama mtaalam musiupitishe mswada huu. Hii ni hatari wala msije mkafikiria katika misingi kwamba wanatayarisha majajanjawiri kwa ajili ya kuja kutudhulumu tu CUF pale, msije huko, huko ndio, lakini msije nyie wengine. Mje kwamba utaongeza kundi la watoto waliokuwa hawana kazi wataiba hawa, hawa Wamasai kuwarudisha Loliondo hawatarudi tena watabaki hapa hapa, wakibaki hapa hapa hawana kazi watafanya nini? Wataiba tu!

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani musitake kutuletea uhalifu katika nchi, huu mswada mimi waziri nakupenda sana, miongoni mwa mawaziri ninaowapenda sana ni huyu waziri aliyeleta huu mswada, likini taratibu urudishe serikalini mutuite wataalam, tuje tukae hapa tushauriane vipi unaweza ukaja huu mswada.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika mswada huu ni kwamba unakiuka vile vile Katiba ya nchi unasuguana na Katiba ya nchi. Haki ya kuishi sijui masikini ni ibara ya ngapi, lakini ipo ile haki ya kuishi katika kifungu cha 13, haki ya kuishi Mheshimiwa inazungumziwa katika Katiba zote mbili.

Haki ya kuwa hai sasa hivi ninayo hii ya Zanzibar, haki ya kuwa hai Mheshimiwa ni kifungu cha 13(1), naomba Mheshimiwa kwa heshima kubwa na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu nikinukuu hiki kifungu kinasema hivi:

“Haki ya kuwa hai kifungu cha 10 cha sheria Nam. 2 ya mwaka 2002, kifungu cha 13(1). "Kila mtu anayo haki ya kuwa hai na kuhifadhi maisha yake", njoo sasa ukilinganishe na kifungu cha 37(1) cha huu mswada. Linganisha hapa wewe unaambiwa kifungu hiki kinasema "Kinga ya Mtumishi". Mtumishi anapewa kinga baada ya kuua huku katiba inataka kuishi, huku mtumishi anapewa kinga baada ya kumuua mtu anasema: "Mtu yeyote ambaye atatenda kosa ambalo halikwenda...

Mhe. Mwenyekiti, samahani kifungu cha 37, Kinga ya Mtumishi. "Hakuna mashtaka au madai yoyote yatakayofunguliwa Mahakamani dhidi ya mtumishi binafsi wa taasisi kwa ajili ya madai ya fidia au maumivu, mali, kifo au uharibifu mwengine au uingiaji usio halali wakati wa utekelezaji wa majukumu ya sheria hii, kwa masharti kwamba ni amri halali ametumia na ametumia nyezo na nguvu zinazostahiki".

Mhe. Mwenyekiti, kwanza huu mswada ndio nasema ni tatizo, tunaunda Jeshi letu la Polisi tena hapa sisi, kwa sababu wenye uwezo wa kukamata ni Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa hivi tutakuwa na polisi wangapi sisi? Mheshimiwa hili ni tatizo ikiwa mna nia nyengine fanyeni, lakini kama ni suala la utawala bora na demokrasia huu mswada haufai kabisa. Hawa JKU waende wakakamate mtu na kumpekua, wampige mpaka wamuue, halafu walindwe, polisi wafanye kazi gani?

Hapa ilipendekeza ile Katiba ya Mhe. Jaji Warioba kwamba kuwe na Jeshi la Polisi na Zanzibar mkaikataa mkasema aa, sasa mnataka kuanzisha Jeshi jengine la Polisi hapa kinyemela, huko si kuhatarisha huo Muungano? Ni tatizo, hebu kuweni wawazi. Mimi nadhani lazima tuitendee haki serikali, mswada haufai urudisheni na wananchi ukipita mswada huu itakuwa Baraza hili lishapitisha watu wauliwe huku wakilindwa na hii sheria.

Sisi katika hili hatujali kwa sababu ikiwa lengo ni sisi kutudhibiti wapinzani, mwanangu katika hili ng'ombe atakavyoanguka ndivyo atakavyochinjwa vile vile, kama kuna watu wanataka amani na utulivu katika nchi hii ni sisi wapinzani na kwa kweli tukikopeshwa sindano sisi tutalipa mtaimbo, mana ukileta amani kidogo sisi tunakuletea tangi zima la amani jamani dogo hilo? Ukileta shari ndogo sisi tunaleta tangi zima la shari hiyo, ndio maana yake. Kwa hivyo sisi hatuna neno, lakini hawa wananchi wa kawaida ambao si wanasiasa.

Mimi siungi mkono hoja na Mhe. Waziri namuomba sana rafiki yangu Mhe. Waziri, mdogo wangu ingawa tunaambiwa tusiwaite ndugu lakini hili haliepukiki Mheshimiwa ndani ya Bunge hili, nyote ni Waheshimiwa lakini vile vile muna wadogo zetu, shemegi zetu, ndugu zetu humu humu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mdogo wangu namuomba sana katika hili aangalie na alirudishe serikalini. Mswada tuurudishe serikalini, Wawakilishi msiupitishe ili serikali ikakae ituite na sisi wadau, wataalam twende pale tukaishauri vya kuleta hili jambo. Kwa sababu hata Muungano utakuwa unahatarishwa kwa huu mswada, kwa sababu watakuwa wanaunda Jeshi jengine la Polisi Zanzibar, jambo ambalo *this is a criminal case*. Mheshimiwa mimi siungi mkono hoja na nakaa kitako. Ahsante sana.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyenijaalia kuwa katika uhai na uzima na afya inaniruhusu pamoja na wenzangu waliohudhuria katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika mswada kwamba kunaanzishwa sheria hii, lakini tukumbuke kama hawa JKU wapo toka zamani. Lengo na madhumuni hawa ni Jeshi la Kujenga Uchumi na tuliona watoto wetu wanavyotoka kwenda katika Jeshi hilo wanavyokuwa wakakamavu kwa kujipanga na mambo ya ajira na mambo mengine, lakini leo hii kuna mabadiliko linakuwa Jeshi la Ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoeleza mchangiaji aliyepita mswada huu wa dharura hauna nia njema, kama una nia njema basi nathubutu kusema isingetajwa tu kuwalinda watalii na wawekezaji. Kwa nini jamii wazalendo wa nchi hii hawakutajwa katika sheria hii, au wakiwalinda wale kule wakitoka huku ni vurugu mechi kwa wananchi wetu? Hatujawatendea haki. Namuomba Mhe. Waziri aangalie sana na afanye marekebisho makubwa au kwa msingi mswada huu urudi tena ukafanyiwe marekebisho, bila ya hivyo tutakuja kufikia mahali pako pabaya.

Mheshimiwa juzi tu, tulipitisha mswada hapa wa kupunguza maafa basi sheria hii ikipita yataongezeka maafa kwa sababu itakuwa hatutendi haki. Tunaomba tuwe makini tunapotunga sheria zetu na kuzipitisha ndani ya Baraza hili la Wawakilishi. Mimi naona dhamira nzuri kule mtu alikuwa anajifunza mambo ya kuchonga, kilimo, akitoka JKU kule basi amekuwa anajua shughuli zote za kwenda kufanya kazi, hapati kigugumizi chochote, kazi yoyote anaweza kufanya. Lakini sasa hivi tunaambiwa sheria hii italinda watalii na wawekezaji wazalendo wao hawana haki.

Mwenzangu kazungumza hapa kuna vikosi mbali mbali ikiwemo Jeshi la Wananchi na Vikosi vya SMZ pia vimeainishwa hapa na hawa Jeshi la Polisi, angalau wangesema watashirikiana na polisi katika mambo ya ulinzi hata polisi hakutajwa. Hivyo, sijui sijaupitia wote lakini katika sehemu nilizopitia sijaona hizo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nikiingia katika mswada huu katika kifungu cha 5(a) kinazungumzia malengo ya taasisi ya ulinzi. Naomba Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako ninukuu.

Kifungu cha 5(a) kinasema kwamba:

> "Kusimamia na kuimarisha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na utalii".

Tunaomba kifungu hiki kiongezwe maneno ili kikae sawa, naomba kisomeke kama hivi: "Kusimamia na kuimarisha huduma za ulinzi katika maeneo ya uwekezaji, utalii na maeneo ya makaazi ya raia". Tusiwalinde hawa wawekezaji tu pamoja na wafanyabiashara ambao ni watalii, lakini ikawa huku hatuna msimamo wa kuwalinda wananchi, tukiwalinda hawa huku tutoke tuje tuwaumize wananchi, haipendezi katika nchi yetu ambayo ni nchi yetu na tunajivunia Mapinduzi ya mwaka 1994 ndio malengo yetu. Na kule kuna kifungu ambacho kinasema katika sheria kuwalinda raia na mali zao, sasa utawalinda hawa tu watu wa kupita si vizuri.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa weka *hansard* sawa mwaka 1994 hakuna Mapinduzi, mwaka 1964 ndio yako Mapinduzi.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Ee, nimesema 1964. Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika kifungu hiki cha 6 hapa kuna kazi za shirika na zitakuwa kama ilivyoainishwa; (a) kutoa huduma za ulinzi, kwa wafanyabiashara kwa taasisi zinazoshughulika na huduma za utalii na nyenginezo. Lakini tukiangalia kifungu hiki kinavyoeleza basi mimi kwa uono wangu nasema kazi za mswada huu zimelenga zaidi katika kuwalinda watalii na wawekezaji kuliko kuwalinda wananchi na kufanya doria wakati wa usiku kwa ajili ya kupunguza uhalifu. Haikutajwa, ingesema kikosi hiki kinachoundwa cha JKU katika mambo ya ulinzi basi kufanya doria.

Juzi hapo Darajani pametokea matukio mangapi, lakini leo tunaelekeza nguvu zetu kuzipeleka huko kunakohusika, kwa kuwalinda watalii pamoja na wawekezaji wenyewe. Si jambo jema hatujawatendea haki wananchi wetu.

Nikiendelea katika mchango katika kifungu cha 9(2) kimeainisha hapa kinasema: "Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa taasisi isipokuwa awe na sifa zifuatazo: Zimetajwa hapa;

(a) awe afisa wa juu kutoka Idara Maalum, naomba kifungu hiki kiongezewe kutoka Idara Maalum za SMZ, liongezwe neno "za SMZ".

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 2(e) kimeelezwa hapa katika sifa hizo awe Mzanzibari. Ni nzuri lakini na hapa naomba paongezwe maneno "awe Mzanzibari wa kuzaliwa". Kwa sababu siku hizi tunaona katika shughuli zetu mtu Mzanzibari halisi kitambulisho hakipati, lakini ambao si Wazanzibari halisi ukienda hapo Wanyamwezi, Wamasai wote wanavyo. Mzanzibari halisi wa kuzaliwa na anajulikana sio katika utata hanacho. Kwa hivyo naomba hapa ili kikae sawa awe Mzanzibari wa kuzaliwa, wengi utakuta ni Wazanzibari hapa lakini ukiangalia sisi masikini wa Mwenyezi Mungu tunaelekea wapi? Hawa wananchi waliotuajiri hawapati haki zao za kimsingi lakini wengine wanapata. Sasa na katika hizo ajira watakosa hawa Wazanzibari wazalendo na watapata watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nakwambia kwamba haitoshi hata kifungu (f) kimezungumzia awe mwenye tabia nzuri. Naomba kifungu hiki kisimalizie hapo na liongezewe neno au maneno, "awe na tabia nzuri na maadili katika jamii". Kwa sababu unaweza kuonekana pengine umevaa vizuri tu ukaonekana huyu mtu ana tabia nzuri na pengine ni jambazi hana tabia nzuri. Kwa hivyo, naomba liongezwe neno katika kifungu hiki awe na tabia nzuri na maadili katika jamii hapo kitapendeza, bila hivyo unaweza kumteuwa mtu na sifa hii ameikosa.

Katika kifungu cha 10, Majukumu ya Mkurugenzi. Hapa yameainishwa lakini mimi katika kifungu hiki cha 10(2)(d), "Kutoa taarifa za shughuli za taasisi katika vikao vya Bodi kila baada ya muda; na" hakumalizia. Kwa hivyo, naomba hapa pawe na marekebisho muda unakuwa ni mrefu, unaweza ukachukua hata mwaka ikawa ni muda tu upo, ingeainishwa moja kwa moja. Mimi napendekeza katika kifungu hiki kiongezwe kila baada ya muda wa miezi mitatu ili shughuli zetu ziende sawa, lakini ukitaja muda tu hukuainisha basi haujulikani muda gani.

Mhe. Mwenyekiti, hapa katika kifungu cha 14(1) imeelezwa kwamba:

"Kutakuwa na Bodi ya Taasisi ya Ulinzi ya JKU ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;
(b) Mkurugenzi wa Taasisi ya Ulinzi;

Haikuainishwa kwamba atateuliwa na nani, napendekeza na huyu ateuliwe na Rais.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu kama nilivyosema utakuwa mdogo naomba niishie hapo, lakini mswada huu kuna haki ya kuuangalia naomba waziri atakapokuja hapa anijibu hizi hoja zangu mpaka niridhike ndio tuweze kupitisha. Nasema naishia hapo sitounga mkono mpaka nitakapopata majibu sahihi ya yale maelekezo tuliyoelekeza. Ahsante.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuchangia Mswada huu wa Kuanzishwa Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi.

Pili napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohammed Shein kwa kufuta michango au ada mbali mbali katika skuli zetu za msingi, yaani darasa la kwanza hadi la saba. Hii ni faraja kubwa kwa wananchi na hata wazazi kwa ujumla. Pia namtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake na Mwenyezi Mungu azidi kumuongoza katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza waziri naye na watendaji wake wote na hasa kwa vikosi vyetu hivi mbali mbali kwa kazi nzuri ya ulinzi na usalama na utulivu wa nchi yetu. Mimi nitakwenda katika ukurasa wa 269 katika kifungu cha (3) ambacho kinaeleza tafsiri ya mpiganaji. Lakini katika mswada neno hili halikutumika.

Nikiendelea nitakwenda katika ukurasa wa 271 katika kifungu cha (2)(c), kinaeleza Mkurugenzi Mkuu awe na sifa zipi. Kifungu hiki kinasema, awe na elimu angalau shahada ya kwanza kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika na serikali. Lakini hapa hakutajwa ni fani gani, kwa sababu ukiangalia katika majukumu ya Mkurugenzi Mkuu kazi kubwa ni kuandaa mpango wa biashara, kuandaa bajeti ya taasisi na kusimamia suala zima la fedha. Kwa hiyo, ni vyema ingetajwa ni fani gani ambayo inatakiwa kutokana na majukumu ambayo yapo.

Pia hapo hapo huyu MKurugenzi Mkuu ameelezwa katika kifungu cha 14(1)(b). Hapa Mhe. Waziri naomba anifafanulie kwa sababu huku kaeleza Mkurugenzi Mkuu ambaye atateuliwa na rais, lakini katika hii bodi kuna Mkurugenzi wa Taasisi ya Ulinzi. Kifungu cha 14(1)(b), lakini katika tafsiri ya maneno huku Mkurugenzi Mkuu haikuoneshwa. Sasa nataka anieleze Mkurugenzi Mkuu huyu ambaye katajwa atateuliwa na Rais ni huyu ambaye ataingia kwenye bodi ambaye kwenye bodi kaelezwa ni Mkurugenzi wa kawaida tu, mkuu haijaandikwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi ni huyu ambaye atakuwa Mkurugenzi Mkuu ataingia kwenye bodi ndio ambaye atakuwa Mkurugenzi wa taasisi? Nilikuwa naomba ufafanuzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kama ndio hivi basi, ina maana kwenye tafsiri pia ielezwe maana ya Mkurugenzi Mkuu. Kwa hiyo, atakuwa tofauti maana ya Mkurugenzi Mkuu ina maana atakuwa na Wakurugenzi wengine mbali mbali. Kwa hivyo, nilikuwa naomba nipate maelezo hapa Mhe. Mwenyekiti.

Jengine kifungu cha 15 ambapo kinasema: "Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na sifa zifuatazo:

(b) awe na elimu isiyopungua kidato cha nne". Hapa nilikuwa naomba kama itawezekana parekebishwe iandikwe, awe na elimu angalau kidato cha nne. Hii tunaweka fursa ambayo hata akiwa na *Form Six, Form* ngapi huko, kuliko kuweka hata isiyopungua. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza iwekwe angalau awe na elimu ya kidato cha nne.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika dhana nzima ya mswada huu. Mswada huu Mhe. Mwenyekiti, awali ulikuwa uwe Shirika la Ulinzi la Utalii, lakini dhana kuu inavyoonekana kama imebadilika na ikawa wakala wa Ulinzi wa JKU na ndio maana hapa katika michango mbali mbali ambayo baadhi ya Wajumbe wamechangia wengine wanaokana kama ulinzi huu labda imetokea kama kutokufahamika.

Kwa sababu dhana hii Mhe. Mwenyekiti, ingekuwa imebadilishwa lakini ilipobadilishwa tungepewa sisi elimu kuhusu mabadiliko haya ya dhana nzima hata ule mchanganyiko katika majadiliano yasingetokea. Wengine wanasema wanalindwa wao siku za uchaguzi, wengine wanasema wanalinda maduka. Lakini ukisema wakala wa Ulinzi wa JKU ina maana wakala anakuwa ni mlinzi wa Taasisi mbali mbali; watalii, kama mtu ana maduka yake sehemu mbali mbali ambao wanahitaji ulinzi, wakala ndio atakuwa anachukuwa jukumu hilo la kufanya kazi hiyo, na sio dhana ile ambayo imezungumzwa na watu wengine Mhe. Mwenyekiti.

Jengine kuanzishwa kwa uwakala huu ina maana kutaongeza ajira na ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, ajira ni changamoto katika nchi yetu. Kwa hiyo, ninachoomba kuna baadhi ya mahoteli huwa wale ambao wamefanya kazi za ulinzi wanaweza wakafika miaka wengine mitatu ningapi na wale wao waangaliwe ikiwezekana na wao wapatiwe mafunzo, ili waendelee na ajira yao na pia kuna suala zima la wale JKU ambao wapo makambini ambao bado hawajapata ajira.

Nilikuwa nashauri tu Mhe. Mwenyekiti, kwa Mhe. Waziri ajira hizi na ziwalenge na wale ambao wako JKU ambao hawajaajiriwa, isijekuwa ajira zinatokea tena wakachukuwa watu wa mitaani ambapo mafunzo hawajapata, lakini wakichukuliwa wale wa JKU ambao wameshapata mafunzo ambapo bado ajira hawajapata, hii itasaidia hata yale mafunzo wakitolewa hayatochukuwa gharama kubwa sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, suala zima la vifaa kwa hawa walinzi wetu. Sasa hivi kuna changamoto Mhe. Mwenyekiti, wahalifu wako wengi wanatumia mbinu mbali mbali lakini hawa wakipata mafunzo mazuri, wakipata na vifaa vya uhakika vya ulinzi wataweza kukabiliana na hali yoyote ile ambayo itawatokea, hatuombei hivyo, lakini ni vizuri kuwatayarisha kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia zote. Ahsante (*Makofi*).

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia asubuhi hii mzima wa afya na kuweza kusimama katika ukumbi huu na mimi kuweza kutoa mawazo yangu katika Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Uchumi na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu uliowasilishwa mbele yetu tumejaribu kuona kwamba bado una kasoro mbali mbali; ambazo baadhi ya kasoro hizo zilifanyiwa marekebisho na kamati, lakini bado matatizo hayo yanaendelea kuonekana ndani ya mswada huu.

Mimi nahisi kwamba ni kutokana na mswada ulivyoletwa, kwa hivyo kuletwa kwake ni kwa haraka haraka na marekebisho yale pia yakafanywa haraka haraka, baadhi ya maeneo yakawa hayendi vizuri katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze katika majukumu ya Mkurugenzi; pale kuna kifungu namna 10(2)(b) hiki kifungu kinasema;-

(b) "Kuandaa mpango wa biashara wa taasisi"

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii tukaambiwa ni Wakala wa Serikali na hii taasisi itakuwa inapata ruzuku kutoka serikalini. Kwa hivyo, kuanzisha biashara kwa taasisi hii kuna matatizo kiasi fulani ningeomba sana kwamba hiki kifungu cha kuanzisha biashara (b) kifutwe na kile kilichowekwa (c) kiwe (b) na kuendelea vyengine ili kupunguza mivutano ndani ya Taasisi hii ya Ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye kifungu cha 15; sifa za Mwenyekiti wa Bodi. Kinasema:-

Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na sifa zifuatazo:-

(b) "Inasema awe na elimu isiyopungua kidato cha nne".

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, ukija katika kifungu cha 19 sifa za Mjumbe wa Bodi inasema kwamba:-

(a) "Awe na elimu isiyopungua Shahada ya kwanza kutoka katika chuo chochote kinachotambuliwa na serikali katika fani ya Utawala, Ulinzi, Sheria, Uhasibu au zinazolingana na hizo".

Hoja yangu iko hapa Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti ndiye Mkuu husika wa Taasisi yoyote ile. Lakini hapa sheria imeanza kumpa kima kidogo cha elimu kuliko wale Wajumbe wake ambao atakuwa anawaongoza. Kwa hivyo, ukiichukuwa hapa Mwenyekiti kidato cha nne lakini wajumbe Shahada ya kwanza. Kitaaluma hapa inaelekea kwamba Mwenyekiti huyu heshima yake ya kielimu mbele ya Wajumbe wake itakuwa ni ndogo fani yake aliyonayo ya taaluma inazidiwa zaidi na zaidi ni wale anao waongoza.
Kwa hivyo, hapa mimi siridhiki na kiwango hiki cha Mwenyekiti kilichowekwa kuwa na kidato cha nne kulikoni wale Wajumbe ambao atawaongoza katika kikao hiki.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalokusudia kulichangia ni kutokana na kifungu cha 37 (1) ambacho ni kinga kwa mtumishi. Katika mswada huu kifungu hiki mimi kimenipa mashaka makubwa sana hii kinga imekuwa kubwa mno kwa mtumishi huyu. Kinga hii inakwenda sambamba na kiongozi wa nchi. Kinga hii inakwenda sambamba na Jeshi la Mmarekani.

Kwa nchi zetu za kiafrika kifungu kinasema kwamba "hakuna mashtaka au madai yoyote yatakayofunguliwa mahakamani dhidi ya mtumishi binafsi wa taasisi kwa ajili ya madai ya fidia au maumivu, mali, kifo au uharibifu mwengine au uwingiaji wa usio wa halali wakati wa utekelezaji wa majukumu ya sheria hii kwa masharti kwamba ni amri halali na imetumia nyenzo au nguvu zinzaostahili".

Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu ni hatari sana na hapa tunaweza kuja kuiingiza nchi katika matatizo makubwa. Kwanza inavyoeleweka anavyosema kiongozi hasa ndugu zetu wa vikosi, neno lolote litakalosemwa kwake ni amri na ni sheria ndivyo inavyoeleweka; kumbe kuna sheria halali na sheria haramu. Sasa mtumishi huyu anaweza kujakufanya jambo ambalo ni kinyume na utaratibu. Lakini kutokana na sheria inavyomlinda inaweza nchi ikajaingia katika hali mbaya kutokana na kifungu hiki. Hivi karibuni tumesikia kwamba wenzetu kule Marekani askari mweupe alimuuwa raia mweusi, kesi ile kufika mahakamani ikaambiwa kuwa hakuna kesi.

Sasa na sheria hii tunayoianzisha kwamba askari huyu atakuwa hana kesi itakapotokea tukio ima mtu kupata maumuzi au mali yake kuchukuwa au kifo, hasa suala zima la kifo akawa mtu huyo hashitakiwi kama kiongozi wa nchi, aaa! Tunakwenda vibaya Mhe. Mwenyekiti, huko tunaelekea kubaya, huyu ni binaadamu kama binaadamu mwengine anaweza akateleza, anaweza akafanya kwa makusudi na ikawa tayari sheria imeshamtoa hatiani.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, sitokubaliana kabisa kabisa na kifungu hiki mamlaka aliyopewa mtumishi huyu ni makubwa mno. Kwa hivyo, naomba kwamba kifungu hiki cha 37(1) kifanyiwe marekebisho. Mhe. Mwenyekiti, iwapo kitafanyiwa marekebisho kifungu hiki basi mimi na vile vifungu vyengine ambavyo wenzangu wameviona kwamba vinakasoro ya mswada huu, basi na mimi hapo vikishafanyiwa marekebisho nitaungana nao kuweza kuupitisha mswada huu. Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi ya kutoa machache kuhusu mswada huu ulio mbele yetu ambayo pamoja na mengi sana mazuri yaliyomo, dosari ndogo ziliomo zinaufanya mswada huu uwe haufai, haukubaliki na uwe hauna maana.

Mhe. Mwenyekiti, sisi sijui tutakuwa Wawakilishi wa aina gani tutakapokubali kuwa mfanyakazi auawe, any'anganywe au vyovyote na tuidhinishe, kwa hivyo ni sawa sawa tutakuwa hawa watu tunawawakilisha vipi, tunaidhinisha vifo hapa. Kifungu kile kinachozungumza hivyo kifutwe na hakifai.

Mhe. Mwenyekiti, serikali ina jukumu la kulinda raia na mali zao. Kifungu hiki kinaipa ruhusa serikali ya kunyang'anya na kuua raia zake; jambo ambalo sisi tutakuwa ndio *"Mas-ul"* hapa duniani kupitia kifungu hiki na kesho mbele ya Mwenyezi Mungu. Jamani tusije kukubali kwamba kifungu hiki kibakie kesho mbele ya Mwenyezi Mungu tutakwenda sema nini? Kwa sababu tutakuwa tumekubali kuidhinisha kwa mikono yetu mauaji ya watu wa nchi hii. Kama ana kosa au hana kosa si kila kosa linalosababisha kuwa mvunja sheria auliwe.

Lakini kumpa mtumishi silaha yeye ni wanaadamu wa kawaida ana ubinafsi, ana hisia zake mbali mbali ana upendo na watu, ana chuki na watu sie tumpe nguvu hizo sijui tutakuwa ni watu wa aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii ni wakala wa serikali, ina maana inawakilisha serikali katika mambo ya ulinzi, uwekezaji, utalii na mengineyo. Lakini mara inaitwa taasisi mara inaitwa shirika, ningeomba Mhe. Waziri achague jina moja tu ama iwe ni Taasisi ya Ulinzi au ni Shirika la Ulinzi. Lakini hapa isiwe shirika, pale ikawa taasisi kwa chombo kile kile ni sisi watu tu mara nyenginje mtu anakuwa na jina zaidi ya moja, lakini taasisi ambayo tumeitungia sheria ni vyema ikawa na jina moja baada ya majina mawili au zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nivichungulie kidogo vifungu vya 36, 37, 38 ambavyo hapa nizungumze katika ujumla wake, lakini hapa nataka nizungumzie kimoja baada ya chengine ambavyo vifungu hivi viko katika ukurasa wa 277 au 278 kama hivyo.

Kifungu cha 36 kinasema hivi:-

> "Mtu yoyote ambaye atatenda kosa ambalo halikuwekewa adhabu yake katika sheria hii atashitakiwa chini ya sheria ya adhabu au sheria nyengine yoyote ambayo itaweka adhabu kwa kosa hilo"

Sasa kwa kuwa kosa hilo sheria hii haikuliwekea adhabu kwa sheria hii kosa hilo litakuwa si kosa. Kwa kuwa sheria ipo na kosa hilo halijapewa adhabu na sheria hii vipi sasa tumuhukumu mtu huyo kwa kutenda kosa ndani ya chombo hiki, lakini kosa ambalo halijawekewa adhabu, kwa kuwa halikupewa adhabu, ina maana Mhe. Mwenyekiti, kwa sheria hii hilo itakuwa siyo kosa.

Mhe. Mwenyekiti, halafu hakuna mashaka, hiyo niiwache ishasemwa sana. Kwa madhumuni ya malipo ya fidia ya maumivu, ulemavu na kifo, kwa nani. "Madhumuni ya malipo ya fidia ya maumivu, ulemavu au kifo kwa mtumishi kilichotokea katika utekelezaji wa kazi au majukumu yake kisheria au mafunzo maalum au ulinzi". Masuala hayo yatashughulikiwa kwa mujibu wa maelekezo yaliomo katika Sheria ya Tume au Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi.
Mfanyakazi yeye kama ikitokezea bahati mbaya katika kazi zake akapoteza maisha, Serikali atapatiwa fidia kwa yale maumivu, atapatiwa kutokana na ulemavu wake. Lakini raia mwengine, yeye lolote atakalofanyiwa mfanyakazi huyu kama malaika hakufanya kosa. Ni sawa sawa umelala kitandani kwako ukatafunwa na kunguni ukamuuwa. Hakuna atakayekuuliza kwa nini kunguni ukamuuwa. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, na mtu auwe iwe aliyeuwa kunguni au mbu. Ningeomba kifungu hiki kinachotoa uwezo huo Mhe. Mwenyekiti, kiondolewe kabisa na siyo kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii kama hivi vyenye kasoro kubwa siyo ndogo vitaondolewa vitaweza kusaidia katika ulinzi katika sehemu za utalii, za wawekezaji na sehemu nyengine zote zile ambazo bado haupo ulinzi huu kisheria. Kwani nchi yetu sasa hivi inakwenda na wakati. Uhalifu unatokea mara kwa mara. Sasa walinzi hawa kwa sababu itakuwa wanamiliki silaha angalau yule mhalifu ataweza kujua kwamba ninaenda pahala ambapo ninaenda kupambana, kinyume na vile mhalifu anakwenda yeye kajiandaa lakini mlinzi ana rungu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu Zanzibar hakuna mtu binafsi anayemiliki silaha *unless* awe kaomba na kupewa kisheria. Sasa hawa wahalifu ambao wamo ndani ya Zanzibar, silaha hizi wanazipata wapi, wamepewa na nani, kama zinatoka nje wanapita vipi. Hii ina maana ulinzi wa bahari yetu ni dhaifu, watu wanaingia na silaha bila ya kuonekana na hatimae wanafanya uhalifu. Kama wanatokanazo nje, kama zipo ndani wanapewa na nani au hizi silaha za mdungudungu wakafanyia hivi, siyo bunduki za kikweli.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa kujua hawa wahalifu hasa ndani ya nchi silaha wanazipata wapi. Nchi ambayo ina ulinzi madhubuti wa kutosha. Mara nyengine wana nguo (c*ombat*) zinazofanana na vikosi vyetu vya ulinzi, wanazibuni au wanapenyezewa. Kwa kweli tuna maswali mengi ya kujiuliza juu ya matokeo ya kihalifu ambayo yanatokea. Sasa taasisi hii ambayo itamiliki silaha kisheria itakuwa na uwezo wa kupambana na wahalifu pale ambapo wahalifu hao na wao watatumia silaha na kupambana na jeshi letu hili la JKU.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kuwa JKU, maana yake ni Jeshi la Kujenga Uchumi, kwa nini tuliundie taasisi isiwe na vitengo tu, kukawa kuna kitengo cha ulinzi, ikawa kuna kitengo cha biashara, kukawa kuna kitengo mbali mbali. Lakini vyote vile vikawa vipo chini ya mwavuli wa JKU wenyewe moja kwa moja, ikawa kuna taasisi au vitengo tu vinavyohusika na mambo mbali mbali. Kama kitengo kimoja kinachohusiana na huo ulinzi wa mali za utalii na wawekezaji, kikawa na kitengo cha biashara lakini mwavuli wote ukawepo kwenye JKU wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kuunda taasisi hii na hii, leo hapa, leo pale. Hii imeonekana kuwa pamoja na kuwa itakuwa na uwezo wa kutafuta pesa wao wenyewe lakini bado itakuwa Serikali inaipa ruzuku. Jinsi tunapoanzisha taasisi ambazo bado haziwezi kujitegemea, ndivyo tunavyoongeza matumizi ya Serikali, ndivyo Serikali itakapoongeza njia za kupata pesa. Serikali inapata pesa kwa kuongeza kodi. Kwa jinsi tunavyoongeza matumizi, ndivyo tunavyombana mtu wa chini kuwa achangie zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo baadhi ya wakati taasisi tunazozianzisha zinaleta athari kwa walipa kodi wetu na wao wana haki ya kufikiriwa, wao ndiyo wavuja jasho. Halafu wachangie chombo ambacho keshokutwa kinampiga mmoja risasi na mpiga risasi pengine apewe nishani kuwa kafanya kazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, mimi siungi mkono hii iliyo mbele yetu. Ahsante sana. *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mohammed Haji Khalid, sasa ni nafasi ya Mhe. Hussein Ibrahim Makungu baadae Mhe. Panya Ali Abdalla.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii nichangie yangu machache katika Mswada huu.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote tukiwa katika afya njema ya mchana huu kwenye kikao chako cha Baraza la Wawakilishi. Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri - Mhe. Haji Omar Kheir kwa Mswada wake huu aliotuletea hapa. Kwa kweli mswada ni mzuri na mimi ninampongeza sana kwa jitihada yake hii aliyoiona katika kuimarisha ulinzi katika nchi yetu. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ni mzuri, hasa hii Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi, Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze haraka haraka na mchango hautokuwa mkubwa. Katika sehemu ya kwanza ya sheria hii inayojulikana kama ni Sheria ya Taasisi ya Ulinzi JKU, 2015. Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mashaka kabisa na Mswada huu. Mswada huu ni mzuri na umekuja ninaweza kusema umechelewa sana lakini Waswahili wanasema unapoamka ndiyo asubuhi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nigusie kidogo kwenye ukurasa wa 270 katika mambo yafuatayo. Kifungu cha 7, taasisi ya ulinzi itakuwa na uwezo ufuatao. Mhe. Mwenyekiti, mimi katika Mswada huu kuna mambo ya kutisha humu ndani lakini ni mambo mazuri na hawa ndugu zetu JKU kwa kweli walivyojipanga na mafunzo yao, wanaweza kufanya kazi vizuri kushinda Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwanza ninaanza kusema ninavipongeza sana vikosi vyetu, hiki cha KMKM, Mafunzo, Valantia na JKU. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri kwa Kikosi hiki cha kwanza cha Valantia, mafunzo yao mimi mwenyewe binafsi nimeyaona na wanajitahidi sana katika mafunzo yao, kwa ukakamavu wao, ulinzi wao, na mambo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini nije katika haya mengine lakini nije suala hili la JKU. JKU pia kwa suala hili la kuanzishwa taasisi hii ya ulinzi Mhe. Waziri ninakupongeza tena ni vizuri, lakini ukurasa wa 7 kuna mambo fulani yameelezwa humu kama kumiliki kutumia silaha katika majukumu yake.

Hili wazo zuri sana na Wajumbe wengi walikuwa wanaliogopa suala hili, lakini ninaweza kusema mfano mdogo, mimi katika mambo yetu sasa hivi, majambazi wamekuwa wengi na majambazi wengi wanaokuja sasa hivi hatujui lakini wana silaha za moto. Sasa kwa nini sisi tusitumie silaha za moto tunapokuwa kwenye ulinzi wetu. Ukimpa sasa hivi mlinzi rungu au panga na mtu anakuja na silaha ya moto haiwezekani kitu hicho. Kwa hivyo mimi ninapongeza sana Mhe. Waziri kwa kurushusu kutumia silaha katika majukumu yao ya silaha za moto. Hili suala ni wazo zuri na nina hakika kabisa, hata wahalifu wakisikia suala kama hili watajua sasa kama hawa wenzetu wa JKU wamejipanga vizuri katika ulinzi wao kwa kutoa huduma yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika hiyo kifungu cha 7 ukurasa wa 270 kifungu cha (b), Kutoa huduma ya ulinzi kwa kampuni, taasisi ya binafsi. Kwa kweli hili ni suala zuri pia. Ninapongeza sana Mswada huu ulivyoweka suala hili. Kwani kampuni kupata ulinzi au taasisi binafsi ni suala kwanza la kuongeza ajira kwa vijana wetu, itakuwa mafao yao nao yanakuja juu na mapato yao yatazidi kuongeza katika nchi yetu. Pia kuimarisha ulinzi, hata wawekezaji hawa na kampuni wakisikia mambo kama haya tumeanzisha basi wao wanapata faraja na kupata moyo mkubwa kuja kuwekeza katika nchi yetu. Hili wazo ni zuri kabisa na kwa nia njema kabisa Serikali imeamua kufanya hivi, siyo kama imeamua kama Wajumbe wengine walivyosema kwa sababu yale ni mambo ya uchaguzi. Haya mambo ya uchaguzi ni yetu na ugomvi saa nyengine inakuwa mambo yetu wenyewe, lakini haya mambo yaliyoekwa hapa ni suala la kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mimi ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa suala na kuwapa vijana wetu vifaa hivi, wacha mbali na silaha za moto na vifaa vyengine pia waweze kuekewa ili kuwatayarisha wakati zinapotokea fujo zozote waweze kujihami. Vifaa vya *riot* vile vya kujikinga wao wenyewe, kofia na nguo wakati wa hatari. Naomba Mhe. Waziri vifaa hivyo uwaangalie vijana wetu hawa wavipate. Pia katika ulinzi wao linapotokea jambo lolote la hatari na fujo waweze kuhimili vishindo hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hili suala ni kwa nia njema kabisa Serikali yetu imeanzisha, hasa kwa hawa JKU na mambo haya ni muhimu sana katika nchi hasa katika miaka hii tunapoendelea mbele.
Mhe. Mwenyekiti, pia katika Mswada umesema kuwa wataanzisha ofisi ndogo ndogo hasa hapa na Pemba. Hilo ni wazo zuri ofisi zao zikianzishwa, wananchi wakitaka huduma wanaweza kuwafikia kwa haraka kabisa.*(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, niingie Mswada huu ukurasa wa 271 katika kifungu cha 9 (1). Hapa kumeelezwa kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Ulinzi ambaye atateuliwa na Rais. Hili ni wazo zuri kabisa, Rais atachagua Mkurugenzi ambaye anastahiki, bila ya upendeleo wowote na atakuwa na uwezo wake kamili wa kufanya kazi kwenye taasisi. Lakini mimi ninapendekeza Mhe. Mwenyekiti, Rais atakapochagua huyu Mkurugenzi asitoke mbali na taasisi hii, atoke kwenye vikosi hivi hivi, mwenye uzoefu na yupo imara kabisa. Achague ndani ya vikosi aweze na kuwa na upeo na yeye na ufahamu mkubwa, ajue malengo na madhumuni ya kazi yao ndugu zetu wa JKU ili waweze kuhimili vishindo vile ambavyo vinaweza kutokezea vya ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika haraka haraka kwenye ukurasa wa 271 kwenye Mswada ni sifa ambazo zilizowekwa kuteuliwa Mkurugenzi awe na sifa zifuatazo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ninampongeza Mhe. Waziri kaweka wazi kabisa, ni vitu vizuri vinaonesha kila kitu hajaficha kitu.

Kwanza kwenye ukurasa wa 271 (2), tukianza na (a) sifa za mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi. Awe Afisa wa juu kutoka Idara Maalum, hili suala zuri kabisa kama nilivyoeleza mwanzo na hapa katika Mswada huu imeekwa vile vile, awe Afisa wa juu na awe na uzoefu, awe mtu mzuri kabisa na anajua jukumu lake hili la suala la ulinzi ambavyo wataweza kuhimili vishindo vya kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka kumi na tano. Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti, ninapendekeza hii miaka kumi na tano pia ni mingi, iwe angalau miaka kumi. Huyu mtu ana uzoefu basi inatosha kabisa, miaka kumi siyo kidogo. Kwa hivyo naomba hapa iwe baada ya 15, hata 10 inatosha kwa huyu Mkurugenzi kuwa na sifa hizo, basi itakuwa suala zuri kabisa. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, awe na elimu isiyopungua shahada ya kwanza. Mimi ninaongezea hata kama shahada ya pili pia anayo au taaluma nyengine nzuri zaidi ikaekwa pia siyo mbaya. Lakini shahada ya kwanza pia nzuri itakuwa

anatosha huyu Mkurugenzi awe na sifa hiyo. Asiwe ametiwa hatiani kwa kosa lolote. Hilo suala zuri, inaonesha wazi kuwa Mhe. Waziri Mswada huu ni mzuri haujaweka mambo kuwa siyo mazuri. Kwa sababu mtu akiwa na hatia mbaya hapa hawezi kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi. Kwa hivyo hili suala zuri kabisa asiwe na hatia yoyote, awe anafaa kuwa Mkurugenzi wetu wa taasisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kifungu cha (e) awe Mzanzibari. Lakini mimi ninapendekeza pia awe mzaliwa wa Zanzibar,kwani anaweza kuwa Mzanzibari lakini hajazaliwa hapa, awe pia kazaliwa hapa itakuwa uzuri zaidi. Na pia awe na tabia nzuri, hapa imeandikwa na awe na tabia nzuri lakini ninapendekeza awe na tabia nzuri kwa jamii, anashirikiana na watu vizuri, awe anaelewana na watu vizuri kabisa, huyu kabisa pia anaweza kuwa Mkurugenzi. Lakini mimi ninapendekeza zaidi awe na tabia nzuri kwenye jamii yetu. Liongezwe neno "jamii" pia iwepo.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye ukurasa wa 273 katika kifungu cha 17. Bodi itakuwa na kazi zifuatazo. Mhe. Mwenyekiti, Bodi hii kweli itakuwa na kazi kubwa lakini mimi niliangalia mambo mafupi tu kidogo, hapa kwenye Bodi na nikaona mambo muhimu, pia yameekwa hii Bodi ifae kuangaliwa. Lakini jambo la kwanza katika kifungu cha 17 (b) kimeweka kupendekeza mishahara na maposho kwa mafao ya watumishi wetu. Lakini ninapenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuliona jambo hili, kwani vijana wetu hivi sasa wengi ajira zinakuwa zinasuasua na wanahangaika lakini tutakapopata vijana wakakamavu, kazi hii wataiweza, basi naomba na Bodi hii iweze kuangalia mafao mazuri na mishahara yao, mizuri waweze kukidhi maisha yao katika mahitaji yao ili wasiingie katika mambo ya uhalifu na wafanye kazi yao kwa nia safi na nia njema, kabisa ya kurubuniwa kwa chochote. Kwa hivyo ndiyo maana Bodi hii imeekewa hapa kuangaliwa na mimi ninaomba sana waangalie maposho na mafao ili hawa ndugu zetu wasiwe na imani mbaya au kufanya uhalifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ninapongeza sana kwa kifungu hiki (b) kwa kupendekeza mishahara na maposho kwa watumishi hawa wanaofanya kazi katika jukumu hili. Lakini pia nipongeze tena kwenye Mswada kwenye ukurasa wa 273, wameekwa kuwa Bodi pia na itakuwa na uwezo wa kuidhinisha ajira mpya kama zilivyopendekezwa.
Kwa hivyo mimi ninapendekeza kama alivyosema Mhe. Waziri sana kwa suala zuri, hii Bodi itakuwa na uwezo pia kuajiri upya kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu ni mdogo tu lakini ninaunga mkono Mswada huu asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*
**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe, sasa ni nafasi ya Mhe. Panya Ali Abdalla na baadae kwa mchana huu tutafungia na Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais na Utawala Bora - Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii nikaweza kusema machache na kwa kweli afya yangu haipo vizuri, sikupenda hata nichangie lakini ninataka nichangie kwa umuhimu wa huu Mswada.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote ambao wameweza kutayarisha mswada huu na wakauleta katika wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, kuletwa kwa mswada huu niseme kutasaidia sana kuweza kuwa na ulinzi wa kutosha, lakini pia kama hilo halitoshi Mhe. Mwenyekiti, itasaidia sana kuondoa kile kilio chetu cha kila siku cha ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi siku zote huwa tunanung'unika kuhusu ajira na kila siku tanasema hapa nafasi zikitokea tunakosa na nini, lakini kwa kuletwa mswada huu ambao unaoneshea au unaashiria kwamba vijana wetu wataweza kupata ajira. Mimi nawapongeza sana kwa kuuleta mswada huu.

Pia napenda niungane na Mhe. Marina ambaye alisema ajira hizi zitakapotolewa basi ziweze kuzingatia wale vijana wetu ambao tayari wameshapitia katika mafunzo ya jeshi letu hili la JKU, kwa hivyo tutakapowathamini wao kuwapatia hii ajira ya mwanzo, italeta faraja kubwa kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuwapatia mafunzo zaidi wale ambao tayari wao wako katika ajira hiyo ya ulinzi, basi mswada huu uzingatie usichukuwe kuwafukuza wale vijana katika kazi, lakini uzingatie katika kuwaongezea ujuzi wa ulinzi wao.

Mhe. Mwenyekiti, serikali haina nia mbaya kwa wananchi wake. Sidhani kama Mhe. Mwenyekiti, serikali inakusudia kufanya mabaya kwa wananchi wake, isipokuwa serikali inakusudia kufanya mambo mema kwa wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu namba 37 ambacho watu wanakilalamikia sana, mimi nahisi kifungu hiki kimelenga wahalifu wale ambao watakwenda kinyume na taratibu ambazo zimepangwa au kinyume na sheria, hao ndio ambao wanahusika na kifungu hiki. Sidhani kama kifungu hiki kitakuwa kinamkamata tu kila mtu na kumuonea au kumnyanyasa. Lakini utakapovunja sheria, nadhani kifungu hiki ndio utakumbana nacho. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama kifungu hiki kiko kwa kuwakamata watu kiholela. Kifungu hiki kiko kwa kuwakamata wahalifu na kupata adhabu ambayo itastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nazidi kupongeza mswada huu na ninaupongeza kwa sababu sisi wenyewe ni mashahidi, tumekuwa tukiona katika nchi yetu matukio mbali mbali ya kihalifu ambayo yanajitokeza Mhe. Mwenyekiti. Ni juzi tu tumeona hapa majambazi ambapo wamefukuzwa na wakakamatwa hapo Darajani na yakapigwa. Sasa kuongeza ulinzi ambapo tukajihakikishia usalama wa nchi yetu, mali zetu na familia zetu ni jambo la busara kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, tusingependa nchi yetu labda tuwe katika hali ya matatizo, tungependa kuona nchi yetu amani na utulivu inaendelea hapa. Nichukuwe fursa hii kuvipongeza sana vikosi vyetu vyote vilivyo katika nchi yetu, kwa ulinzi imara ambao wanauchukua na kuona mpaka leo hii bado tunaendelea kuishi katika hali ya amani na utulivu, Inshaallah Mwenyezi Mungu awajaalie nguvu na busara za kutosha, ili waweze kukilinda kisiwa chetu hiki tuweze kuendelea kuishi katika hali ya ulinzi na usalama kama hivi tulivyo sasa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme machache tu kwa ajili ya kuunga mkono mswada huu. Kwa hayo machache, naomba nichukuwe fursa hii kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na Inshaallah Mwenyezi Mungu aweza kuujaalia upite, ili tufanikiwe kuongeza ulinzi katika nchi yetu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa wasaa huu mdogo na mimi kuchangia mswada huu muhimu kwa nchi yetu, mswada unaozungumza sheria ya taasisi ya ulinzi ya JKU.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona nisimame na mimi kuchangia kuupa nguvu mswada huu, hasa pale niliposikia baadhi ya wajumbe wakihoji umuhimu wa chombo hiki ambacho serikali inataka kukianzisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri wazo hili lilipokuja mimi nilikuwa waziri ninayesimamia Idara Maalum na tulitafakari kwa kina ili kuona twende vipi. Chimbuko lenyewe Mhe. Mwenyekiti, halikuanza serikalini. Chimbuko limeanza kwa wafanyabiashara wenyewe wa hoteli na utalii kwa ujumla, baada kama alivyoeleza Mhe. Mjumbe aliyekaa Mhe. Bi Panya Ali Abdalla, baada ya matokeo mengi ambayo yalikuwa kila siku yanazidi ya uhalifu, ujangiri, kuvamiwa mahoteli, wizi wa kutumia silaha, watalii wanafika na kujeruhiwa. Wakasema jamani utalii unaanza kuingia doa Zanzibar.

Kwa hivyo, ZATO na ZATI taasisi mbili zinazosimamia biashara kwa ujumla ya utalii na mahoteli, walikaa wenyewe wakatafakari tufanye nini. Hao wote Mhe. Mwenyekiti, walikodi vyombo mbali mbali vya ulinzi na usalama, tunaona kofia zao wale wengine wanavaa nguo nyeupe wengine nyeusi *KK Security,* viko kwenye mahoteli mbali mbali. Lakini walinzi wale wanao watu wanakuja na *submachine gun*, watu wanakuja na *automatic grayfor*, yeye ana kirungu haya utamzuia mtu huyo, tena wanakuja kundi la watu wamejikusanya na gari zao. Sasa yeye yuko kwenye eneo lake tu la hoteli, wakasema jamani kwa wimbi hili linalokuja hatuwezi.

Kwa hivyo, wakaja wakasema serikali tunaiomba lazima tukae pamoja tutafakari suala hili. Serikali wakati huo tayari inacho chombo kile tunaita cha *tourism patrol police.* Kupita pita na mapikipiki na magari ili kuona hali ikoje, kama kutoa habari tu halafu polisi wao waingie kati. Lakini tukaona bado uhalifu hasa madhara kwenye utalii bado haijashughulikiwa ipasavyo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kuona hapa kwamba moja katika kazi au kazi mbili zilizotajwa, katika kifungu namba 6 cha shirika au taasisi kwenye ukurasa huo wa 270, kwenye kifungu cha 6(c), inasema;

6(c) "Moja ya kazi za shirika ni kutoa ushauri wa kiulinzi na kiusalama kwa watalii, wadau wa utalii na taasisi nyenginezo";

(d) "Kutoa mafunzo ya ulinzi na kiusalama kwa taasisi zenye kushughulika na utalii na nyenginezo".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kukazia hapa. Utalii sasa ndio mwelekeo wa uchumi wetu katika nchi yetu, utalii ndio roho yetu sasa lazima tuunyenyekee, tuufuatilie na tuusimamie. Utalii Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru neema kubwa sana tumepata baada ya fujo za majirani zetu. Hatuombei fujo, lakini baada ya ghasia zilioko Kenya na Mombasa huko kwa jumla, leo watalii Alhamdulillah wamemiminika Unguja neema kubwa sana.

Zamani tuna msimu mkubwa na tuna msimu mdogo. Lakini leo huo msimu mdogo basi utaona kama kawaida tu, na watalii wanakwenda mule Mji Mkongwe wanatembea kwenye fukwe mule, lakini mapaparazi nao wapo, kwenye fukwe wanawafuata mpaka majini. Utamkuta mtu ana miwani ya jua anamfuata mtalii anakoga kwenye maji ya chini yale anakwenda kumuuzia miwani. Yule hamuuzii miwani ana malengo yake tu.

Sasa haya Mhe. Mwenyekiti, ukitizama hoteli tulizonazo leo zilizotapakaa Unguja nzima, Kaskazini, Kusini, Magharibi, Mashariki na Pemba nako hoteli zinaanza, lakini tayari mote humo, basi hao majambazi nao wana *plan* zao, wanavizia na wanatafakari vipi waingilie kati kuwadhulumu watalii na kutuvunjia sisi biashara yetu hii.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, najaribu kujenga hoja kwa wenzangu waheshimiwa, kwamba tuone umuhimu wa chombo hiki kinachotaka kuanzishwa. Tukaona kweli tunavyo vyombo vya JKU na KMKM kama walivyotaja wengine. Lakini kwa nini tuipeleke dhamana hii kwao, wao wana majukumu yao maalum ambayo tumewapa na kwa kweli hawatoshi, nchi yetu imekuwa mambo mengi, makundi mengi. Umetolewa mfano hapa, huwezi kuamini wewe Darajani mchana saa 6 au saa 8 jamaa wanapiga. Sasa ungetarajia tuweke walinzi mote mule, walinzi hao wako wapi wote.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, najaribu kujenga hoja kwamba hiki chombo muhimu na tunakihitajia kulinda uchumi wa nchi yetu, huu ndio uchumi sasa. Kama tukisema karafuu, basi niseme labda karafuu ya pili, au hii sasa ndio dhahabu yetu. Wewe ukitizama ajira ya moja kwa moja wanaopata ni wananchi wetu kwenye biashara ya utalii au wanaopata kwa njia nyengine. *Alhamdulillah* leo tizameni matikiti yanavyozalishwa ni mangapi yanauzwa kwenye mahoteli humo. Natoa mfano mdogo tu, pweza, ngisi, samaki wa kawaida humpati wewe maskini ya Mungu, wote wanachukuliwa kwenye mahoteli.

Sasa hiyo ajira kwa upande mwengine imesaidia sana kwa watu wenye biashara nyengine nazo kufaidika, sekta nyengine nazo kufaidika. Sasa tusipousimamia utalii, watalii wasije tutaharibikiwa Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, mimi nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe watizame kwa mtizamo wa ulinzi kwenye mahoteli yetu, ndio lengo letu hasa kubwa. Lakini tukasema hatuwezi ku- *specify* moja kwa moja kwenye utalii. Kwa ujumla pale kianzishwe chombo na kwa utaratibu maalum na kwa sheria maalum na tukasema huko JKU iwe wingi maalum ni wingi maalum, hiyo ambayo itasimamia suala hili.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa kumsaidia fikra kidogo na michango Mhe. Waziri na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe kusema kwamba hili suala sio muhimu. Hili suala ni muhimu kweli kweli kwa uchumi wa nchi yetu, roho yetu iko kwenye utalii. Tukimkera mtalii mmoja sumu atakayoipaka nje itatuharibia sana Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, mimi nina washawishi Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, pale kwa kukosoa wanafikra neno hili tulibadilishe watowe fikra yao, lakini tuupitisheni mswada huu. Hii ndio roho yetu Mhe. Mwenyekiti, tukiuchezea utalii saa hizi tutaharibikiwa kuja kuziba viraka tena tutapata tabu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nikazie hapo tu na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ndogo sana ya kuchangia katika mswada huu ambao uko mezani kwako. Mhe. Mwenyekiti, sote tunaelewa kwamba

utalii katika nchi yetu ndio nguzo ya uchumi wa nchi yetu na ndio pahali ambapo tunategemea kwa mapato yote ya serikali, na ndio eneo ambalo mapato yetu yote ya kuendeshea serikali, ya kuendeshea nchi tunayategemea. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa njia moja ama nyengine kama serikali, kama wananchi ni lazima tuchukuwe kila jitihada ya kuona kwamba inakuwa salama. Miaka hii miwili mitatu au minne kumekuwa na majaribio mengi sana ya uvamizi wa sekta yetu ya utalii. Kumbukumbu zinaonesha mwaka 2012 kulikuwa kuna majaribio yafikayo 102 katika maeneo mbali mbali ya hoteli nchini mwetu ambayo yalilenga kufanya uvamizi mkubwa. Mwaka 2013 kumbukumbu zinaonesha kulikuwa kuna majaribio 62 na mwaka jana karibu majaribio 80.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, majaribio haya kwa kweli mara zote yanapotokea wawekezaji wa sekta ya utalii huwa wanailalamikia serikali kwamba serikali haijachukua jitihada za kuonesha kwamba tuko makini na uwekezaji ambao unafanywa. Wao wanagharimika kuekeza nchini mwetu, wanatafuta mikopo mikubwa nchini kwao kuja kuekeza. Sasa jukumu kubwa la serikali ni kuona kwamba vitega uchumi hivi vimekuwa salama. Panapotokea majaribio ya kuona kwamba uwekezaji wenyewe uko hatarini, sisi kama nchi ni lazima tuoneshe na tuchukuwe jitihada madhubuti kuona kwamba nguzo yetu ya uchumi imekuwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, sio mara moja wala sio mara mbili, sio mara tatu wala sio mara nne usiku wenye mahoteli wanatupigia simu, kwamba hoteli zao zinavyovamiwa na watu wenye silaha. Sio mara moja, sio mara mbili wala sio mara kumi simu zetu ziko wazi, saa 5 au saa 6 za usiku mwenye hoteli analia, analalamika kwamba serikali mko wapi hoteli yangu inavamiwa. Kwa kweli huwa ni pirikapirika kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia tusisahau mwaka jana tulipata tatizo moja kubwa ambalo nchi yetu ilitikisika sana pale vijana wawili walipomwagiwa tindikali. Ilikuwa ni aibu kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, ilitikisa sana, ilibidi viongozi wetu wote wajibu na kwa kweli Uingereza ambapo vijana wale ndio raia wake, mpaka leo wanatutaka tuonekane kwamba tumechukua hatua madhubuti ya kuonekana nchi yetu iko salama.

Mhe. Mwenyekiti, dalili zinaonesha kwamba wenzetu bado wanaendelea kutuamini. Takwimu za ujaji wa wageni kwa mwaka uliomalizika mwaka 2014, zimetupa moyo sana. Takwimu ya mwaka 2013 tulipata watalii 180,000, lakini takwimu ambazo tunamalizia kuzikusanya zinaonesha kwamba watalii ambao wamekuja Zanzibar ni karibu 300,000. Sasa huo ni mchupo mkubwa, kutoka 180,000 hadi 300,000 *(Makofi)*

Sasa hii maana yake pamefanywa kazi kubwa ya kujaribu ku- *defend* yale ambayo yamekuwa tukitiliwa nayo mashaka, hali ya usalama mbaya katika maonesho ya kitalii mbali mbali ambapo tumekwenda tumejaribu kuwaeleza wenzetu kwamba nchi yetu iko salama sana na *incidence* ambazo zimetokea, tumewaambia zimetokea kwa bahati mbaya kama ambavyo mahali pengine popote zinatokea. Wenzetu wametuamini hivyo na ndio maana wananchi wao wanakuja kwa wingi nchini mwetu na wanaendelea kuja.

Jitihada hizi Mhe. Mwenyekiti, ambazo zimefanywa zinahitaji kuendelezwa kwa kuwa na mipango madhubuti ya ulinzi ya watalii na ..... hilo jambo muhimu sana. Sio mara moja wala sio mara mbili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi humu ndani mumekuwa mkitutaka, hata wakiilaumu wizara yangu kwamba haionekani kuwa ni imara katika kuona kwamba uwekezaji huu serikali inaufanyia kazi vizuri.

Kwa hivyo, mimi naomba wenzangu tukubaliane kwamba kikosi hiki kitakuwa na maana sana kuona kwamba tunajenga *confidence* ya wawekezaji, na hilo ni jambo kubwa sana. Huwezi kumshawishi mwekezaji aje hapa kama hajajenga *trace,* hana *confidence* ya nchi yako kiusalama, hili jambo kubwa sana.

Kwa hivyo, naomba tukubaliane Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi, tukubali mswada huu kwamba upite na kwamba kama kuna kasoro moja, mbili au tatu ambazo mumeziona katika mswada ni jambo la kawaida kwamba mswada kiujumla madhumuni yake ni mazuri. Lakini kama mumeona kuna vifungu viwili au vitatu vina matatizo, basi Mhe. Waziri yupo, Mhe. Mwanasheria Mkuu yupo, serikali ipo, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais yupo na sisi sote tupo.

Haya mambo ni ya kuzingatia ili kuona kwamba tutarekebisha vipi, lakini mswada huu bado nasema kwamba ili kujenga na kulinda uchumi wa nchi yetu, Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi basi ningeshauri kwamba tukubaliane kwamba mswada huu upite. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri mwenye kushughulika na sekta ya utalii, kwa mchango wako mzuri ambao umemalizia kwa siku ya leo asubuhi hii. Sasa kwa vile muda uliobakia ni mdogo, tuna dakika takriban 20 hazitoweza kumtosha Mhe. Waziri kufanya majumuisho yake.

Kwa hivyo, basi tutamuomba Mhe. Waziri akajipange vizuri zaidi ili jioni saa 11:00 barabara aje atupatie majumuisho, na baadaye Waheshimiwa Wajumbe wote kwa ujumla wetu, tuwemo humu mapema kwa ajili ya kupitisha mswada huu, ili kuendelea na shughuli nyengine kama zilivyo taratibu zetu tulivyojipangia.

Baada ya maelekezo hayo sasa, naomba vile vile kusoma tangazo liliopo hapa mbele linalowataka Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, wafike juu katika ukumbi wetu wa kawaida mara baada ya kuahirishwa kwa kikao hiki. Baada ya maelekezo hayo sasa, tutasitisha shughuli zetu hizi za Baraza hadi saa 11:00 barabara za jioni. Ahsanteni.

*(Saa 6:56 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na amani katika nchi yetu na kuweza kuendelea na kazi za ujenzi wa taifa letu.

Nakushukuru pia wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Wajumbe kuchangia Mswada huu, na kuungwa mkono na takriban ya wajumbe wengi waliochangia Mswada huu. Nawashukuru sana wale wote ambao wamechangia na wameunga mkono moja kwa moja na wale ambao wametia mashaka kidogo. Nina hakika baada ya kuwapa maelezo ya ufafanuzi nao pia wataunga mkono Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati leo nahitimisha kazi ya kutunga Sheria ya Kuanzisha Chombo cha Kuimarisha ulinzi katika sehemu za biashara ya utalii, na biashara nyenginezo ambao ndio tegemeo kubwa la uchumi wa nchi yetu naamini sote tumepata taarifa ya tukio la ujambazi lililotokea Darajani Mjini Unguja. Ni jambo la kusikitisha ambalo limesababisha maumivu kwa wananchi wasio na hatiya, uharibifu wa mali na kuwatia hofu wakaazi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla. Nawapa pole wale wote walioathirika na tukio lile.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii ili kuwapongeza Jeshi la Polisi na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa waliiyoifanya kwa kubiliana na kuwashinda wahalifu hao.

Naomba pia niwashukuru kwa dhati kabisa wananchi waliokuwa eneo la tukio kwa kusimama kidete na kuhakikisha kuwa wahalifu hao wanadhibitiwa na kutoa msaada mkubwa kwa Jeshi la Polisi katika kukabiliana na wahalifu hao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani na pongezi kwa Jeshi la Polisi na wananchi kwa tukio hilo lililotokea siku ya Ijumaa tarehe 23/1/2015 hapo Darajani, naomba sasa niendelee na majumuisho yangu kwa kuwatambua wajumbe wako ishirini waliochangia kwa kuunga mkono walio wengi.

Waheshimiwa waliochangia.

1. Mhe. Ussi Jecha Simai Muwakilishi wa Wananchi jimbo la Chaani ambae pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | - | Kitope |
| 3. | Mhe. Ali Salim Haji | - | Kwahani |
| 4. | Mhe. Mussa Ali Hassan | - | Kowani |
| 5. | Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | - | Chambani |
| 6. | Mhe. Ismail Jussa Ladhu | - | Mji Mkongwe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Mhe. Fatma Mbarouk Said | - | Amani |
| 8. | Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | - | Viti maalum |
| 9. | Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Kwamtipura |
| 10. | Mhe. Abdalla Juma Abdalla | - | Chonga |
| 11. | Mhe. Salma Mohammed Ali | - | Viti Maalum |
| 12. | Mhe. Saleh Nassor Juma | - | Wawi |
| 13. | Mhe. Hassan Hamad Omar | - | Kojani |
| 14. | Mhe. Marina Joel Thomas | - | Uteuzi wa Mhe. Rais. |
| 15. | Mhe. Rufai Said Rufai | - | Tumbe |
| 16. | Mhe. Mohammed Haji Khalid | - | Mtambile |
| 17. | Mhe. Hussein Ibrahi Makungu | - | Bububu |
| 18. | Mhe. Panya Ali Abdalla | - | Viti Maalum |
| 19. | Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini | - | Dimani na Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. |
| 20 | Mhe. Said Ali Mbarouk | - | Muwakilishi wa wananchi jimbo la Gando ambae pia ni Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. |

Mhe. Mwenyekiti, katika hili ninataka niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wawili Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, na Waziri wa Habari Utalii, Utamaduni na Michezo, kwa kuchukua nafsi kubwa ya kutoa ufafanuzi na kuwafahamisha Wajumbe madhumuni hasa ya Mswada huu, chimbuko la Mswada huu na nini faida ya kuupitisha Mswada huu. Tuachane na zile dhana ambazo zimejitokeza katika majadiliano yaliyotokea mchana wa leo. Wameeleza vizuri lakini nitakapokwenda katika kutoa maoni ya michango yenyewe nitatoa ufafanuzi zaidi.

Lakini la pili, nataka nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala Mhe. Ussi Jecha Simai kwa kufanya kazi vizuri zaidi Mswada huu katika Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, na kufanya marekebisho mengi na mazuri ambayo yameifanya Sheria hii iweze kutekelezeka vizuri.

Maoni ya Kamati naishukuru Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kwa marekebisho waliyoyafanya na mengi kati ya hayo karibu asilimia 99.9% nakubaliana nayo, na Mswada huu usomeke pamoja na marekebisho hayo isipokuwa ndio ile asilimia iliyobakia ile, katika kusema asilimia 99.9% ya marekebisho yao nakubaliana nayo.

Katika kifungu cha 6(J) kuwa sasa kisomeke kupendekeza kwa Waziri viwango vya ada zitakazotozwa kwa maeneo wanayotoa ulinzi, yaani yale maeneo yatakayopewa huduma na wakala basi ada na viwango vitapendekezwa na bodi na Waziri ataviidhinisha, marekebisho hayo naomba yazingatiwe katika yale marekebisho ambayo kamati imeyafanya.

b) Kifungu cha 19 katika Kiwango chaUzoefu iwe miaka 15 badala ya miaka mitano, kwa nini nasema hivi kwa sababu tukiweka miaka mitano tutakuwa tunakwenda kinyume na sheria ya utumishi wa umma, ambayo inasema *senior public service* ni lazima afike miaka kumi na tano ndio anaweza akawa sasa, anaweza akapendekezwa au akateuliwa kushika nafasi kuanzia ngazi ya Mkurugenzi na ngazi zinazolingana na hayo, tukiweka miaka mitano maana yake tutakuwa tunakwenda kinyume na Sheria ya *public service* na Sheria hii haiwezi kuwa ni juu zaidi ya ile Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kwa hivyo katika maeneo hayo mawili naomba kidogo niyafanyie *correction* na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati nadhani mtakubaliana na marekebisho hayo, lakini takriban nakushukuru sana Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wako wote wa Kamati, kwa marekebisho ambayo wameyafanya kwenye Kamati na sisi Serikali tumeyapokea na tutahakikisha yanaingia katika Mswada ambao atapelekewa Mhe. Rais baada ya Baraza hili kuyapitisha.

Mtu wa pili alikuwa Mhe. Makame Mshiba Mbarouk wa Kitope, hoja yake ya kwanza ametoa shukurani kwa Ofisi yangu kuandaa Mswada huu, muhimu kwa ulinzi wawekezaji dhidi ya ujambazi na wizi. Namshukuru sana kwa hilo na wajumbe wengine, ningependa nao kama walivyoona Wajumbe wengine umuhimu huu basi na wale ambao walikuwa na mashaka basi wanielewe kwamba nia na madhumuni ya Serikali ni kuweza kuwalinda wawekezaji wetu. Kama tunavyojua nchi yetu ni nchi ya visiwa hivi vinategemea biashara ya utalii, biashara ya uwekezaji na biashara ya mambo mengine ya huduma, uchumi wetu unategemea huduma bila ya kuwapa moyo wawekezaji na

wafanya biashara watakaokuja kuwekeza katika nchi yetu uchumi wetu utadorora. Kwa hivyo huu ndio msingi mkuu ambao umetufanya sisi tulete sheria hii na si vyenginevyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ameendelea na hoja yake nyengine ametaka jina sahihi la chombo hiki na tafsiri ya wakala, napenda kutoa ufafanuzi kwamba jina sahihi la wakala wa ulinzi wa JKU na wakala kwa Tafsiri ya Sheria hii ni chombo kitakachofanya kazi ya ulinzi wa biashara ya utalii, na biashara nyenginezo taasisi za umma na watu binafsi.

Kwa hivyo hii ni wakala sio wakala kama ule ambao unafanya kazi kwa niaba ya kampuni, lakini uwakala huu unafanyakazi kwa niaba ya Serikali, na huko mbele nitakapokwenda nitakuja kusema hata kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma imetafsiriwa nani wakala wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ile.

Mheshimiwa pia aliulizia uwezo wa wakala wa ulinzi kuchukua watu wengine ambao sio askari je, wakifanya hivyo mafunzo yatakuwaje. Ufafanuzi ni kwamba watu wote watakaofanya kazi katika taasisi hii ni lazima wawe wamepata mafunzo ya kazi na kufaulu ndio wataruhusiwa kufanya kazi hasa ikizingatiwa kuwa watakuwa na jukumu la kuwa na silaha za moto. Lakini pale ambapo imesema kwamba kuna watu wengine pale itakapotokezea ikawa katika vikosi vyetu hakuna watu wenye taaluma fulani na wanahitajika haituzuii kuweza kumuajiri raia katika kufanya kazi hiyo, kwani katika majeshi yote Duniani wanafanya hivyo hata katika vikosi vyetu yako maeneo ambayo tunaajiri raia badala ya kufanya kazi askari kulingana na yale mahitaji ambayo yapo.

Hoja yake nyengine ilikuwa ni Wakala wafungue mara moja ofisi za Mikoa na Wilaya, Serikali imeona hili si jambo la msingi kabisa kuamua kuweka ndani ya Sheria, kwamba baada tu ya wakala wa Serikali wa Mambo ya ulinzi kuanza kazi tukaanza kufungua ofisi nchi nzima. Ofisi zitafunguliwa kutegemea na mahitaji kwani haitakuwa vyema kufungua ofisi wakati bado hakujajitokeza haja ya kufanya hivyo ili kupunguza gharama wakati wa kuanzisha chombo hiki.

Yaani tunakusudia kwamba tutafungua ofisi nyingi zaidi pale haja itakapotokezea hivyo, lakini tutaanza katika yale maeneo ambayo tayari yatakuwa yana shughuli na yanaweza yasilete hasara, wajumbe wengi hapa wamezungumzia habari ya bajeti tutazingatia hilo. Kwa hivyo kufungua ofisi kila pahala itatutia gharama kabla kujua ukubwa zile shughuli zenyewe zitakavyokuwa, lakini tutaanza kufungua ofisi katika maeneo ambayo tayari shughuli hizo zitakuwa zimeanza mara moja.

Hoja nyengine ilikuwa tuondoe sharti la sifa ya tabia nzuri na badala yake iwekwe sifa ya akili timam, nimuombe Mheshimiwa Mwakilishi aelewe kwamba suala la tabia nzuri lazima liwepo kwani mtu anaweza kuwa na akili timamu lakini asiwe na tabia nzuri, kwani hata wahalifu wanakuwa na akili timamu lakini tabia zao hazikubaliki ndani ya jamii.

Kwa hivyo sharti la kuwepo kwa tabia nzuri lazima liwepo katika sheria lakini akili timamu unaweza kuwa na akili timamu lakini ukawa huna tabia nzuri, ukawa mwizi, ukawa jambazi, ukawa huna maadili na wewe una akili yako timamu na hiyo akili yako timamu ndio ikawa inakufanya uweze kufanya hayo mambo ambayo yanaweza yakawa si mazuri ndani ya jamii yetu.

Hoja yake nyengine alitaka yatolewe mafunzo ya matumizi ya mitambo ya kuzuia uhalifu, kuna kifungu naomba nimuarifu Mheshimiwa Muwakilishi kwamba, kuna kifungu kinacholazimisha kupata mafunzo kwa watumizi wa wakala ili kufanya kazi zao vizuri. Mafunzo yatakuwepo mwanzoni na wakati wakiwa kazini.

Kifungu cha 39 kinaelezea suala hili naomba Mheshimiwa Muwakilishi akipitie vizuri zaidi kifungu hicho kinatoa maelekezo juu ya namna gani watumishi wa wakala wa ulinzi watakavyokuwa wanapata mafunzo.

Hoja yake nyengine ilikuwa Ofisi ya wakala zitakuwa tofauti na zile za JKU, ufafanuzi ni kwamba Ofisi zitakuwa tofauti ingawaje zitakuwa chini ya uzimamizi wa JKU, kwa vile suala la udhibiti wa silaha ni muhimu sana ndani ya nchi yetu na ndani ya taifa letu.

Hoja nyengine ilikuwa risiti za malipo zisiwe za kawaida, naomba niwahakikishie wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na Mheshimiwa Muwakilishi kwamba risiti zitakazotolewa ni zile zinazokubalika na Serikali, na kwa hili tutafuata miongozi inayotolewa na Wizara ya Fedha chini ya Hazina.

Hoja nyengine ilikuwa ni Wajumbe wawili wanaopendekezwa kutoka JKU watakuwa ni askari walio kazini au waliostaafu, hawa watakuwa ni wale walio kazini na sio wale waliostaafu.

Hoja nyengine ilikuwa mtu aliyekusudiwa katika kifungu cha nane ni yupi. Mtu huyu ni yeyote ambaye atakuwa ameingia katika mkataba wa kulindwa na wakala wa ulinzi, yaani hapa wajumbe wengi walionesha kwamba labda sisi nia yetu ni kulinda watalii tu peke yake. Hapana tutalinda wawekezaji wa sekta ya utalii, tutalinda wawekezaji wa sekta ya viwanda. Tutalinda wawekezaji wa sekta zote zitakazokuwa zinafanya biashara, hata Makampuni binafsi na watu binafsi tutakuwa na uwezo wa kuweza kuwalinda.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kamati ilifanya marekebisho kidogo juu ya hili na sisi tumekubaliana nalo, kwa hivyo si uwekezaji katika sekta ya utalii tu lakini hata katika maeneo mengine kama una shamba lako kubwa la karafuu unahisi msimu ukifika kuna wahalifu watakwenda kuiba karafuu, basi unakwenda tu kwa wakala wa ulinzi unatoa mahitaji yako wao watakuletea ulinzi, watalinda lakini utatakiwa ufuate yale masharti ambayo wakala wa ulinzi watakuwa wameyaweka.

Mchangiaji wa tatu alikuwa Mheshimiwa Ali Salim Haji wa Kwahani, hoja yake ilikuwa Je, tumepata uzoefu wa Tanzania Bara kutoka Suma JKT, jibu ndio tumepata uzoefu huo kwa kufanya nao mazungumza, kupata nyaraka zao na kuzipitia na kuzielewa na kubadilishana uzoefu juu ya hili.

Kwa ufupi JKT na JKU ni vikosi ambavyo vina mashirikiano ya kutosha, na kwa taarifa yenu ni kwamba kama vile Kamati ya viongozi wakuu wastaafu walivyopata fursa ya kwenda kutembelea. Vile vile na kamati inayohusika na sekta hii tunatarajia si muda mrefu itakwenda kutembelea katika maeneo yale, ili na wao wapate taaluma hiyo ya kuweza kujifunza.

Lakini sisi tumepata uzoefu wa kuanzisha kitu hiki kutokana na uzoefu wao na taaluma waliyoanayo.

Watakaoajiriwa wale ni wale waliokosa nafasi za ajira vyombo vya ulinzi kutoka JKU na JKT, hili litazingatiwa lakini ni lazima wawe na sifa za kuajirika hasa kwa upande wa umri na elimu kama inavyoeleza sheria ya Idara Maalum za SMZ, Sheria namba 6 ya mwaka 2007.

Kwa hivyo suala la kuzingatia vijana wetu tutalizingatia, lakini nao lazima wawe na vile vigezo ambavyo vimetajwa ndani ya sheria ya Idara Maalum.

Hoja nyengine ilikuwa watu watakaoajiriwa watakuwa wanatumia silaha. Hivyo, ni lazima pawe na tahadhari. Tunashukuru kwa mchango wake huo Mhe. Ali na tunakubaliana na ushauri wake na tutauzingatia. Taratibu za ajira za watumishi wa aina hii zitafuatwa na tutaufuata ushauri wake. Kwani unapoajiriwa katika vikosi au katika Idara Maalum lazima baadhi ya taratibu uweze kuzifuata au ziweze kutimizwa.

Hoja nyengine iliyofuata ilikuwa wataoajiriwa wawe na uwezo wa kuzungumza lugha za kigeni ili waweze kuwasiliana na wageni wengine. Hoja yake tumeichukua lakini kufuatia hoja hiyo watumishi wote watakaoajiriwa watapatiwa mafunzo. Suala hili litazingatiwa wakati wote ama wakati wa ajira kwanza na ikiwa sehemu ya mafunzo kazini. Kwa maana katika kazi kuna utaratibu wa mafunzo kazini, kwa hiyo, tutafanya kazi hiyo. Katika hili nataka niwaambie Waheshimiwa Wawakilishi tutaitumia shule yetu ya Sekondari ya JKU iliyopo pale Mtoni ili kutoa mafunzo haya.

Hoja nyengine ilikuwa kiwango cha kulipia kimewekwa kwa wewekezaji tu vipi kwa watu wengine. Ufafanuzi ni kwamba watu wote watakaopatiwa huduma na wakala wa ulinzi watapaswa kulipia huduma hizo na viwango vya malipo vitapengekezwa na Bodi wa Wakurugenzi na kuidhinishwa na Waziri.

Hoja nyengine ilikuwa alisisitiza suala la kuanzisha Ofisi za Wilaya na Mikoa lipewe umuhimu. Tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa na litafanyiwa kazi kulingana na mahitaji ya wakati huo. Hoja ya mwisho kwa Mhe. Ali, ilikuwa ni muda wa kutumikia Bodi kwa Mwenyekiti na Wajumbe ni tofauti, hili limechangiwa na Wajumbe kiasi watatu naomba nitakapotoa ufafanuzi basi na wale wengine vile vile niwe nimetoa ufafanuzi wao.

Lengo la kifungu hiki ni kuepusha kuondoka kwa Wajumbe wote kwa wakati mmoja na hivyo kusababisha hali ya upya kwa wajumbe wanaokuja. Kubakia Mwenyekiti au wajumbe waliotangulia kutasaidia muendelezo wa fikra na utendaji wa Bodi sambamba na kushauriana kati ya taasisi na mwenyekiti wa kati bodi ikiwa imemaliza muda wake. Inafika pahala kwamba mkiwawekea wote muda mmoja wa miaka mitatu wajumbe pamoja na mwenyekiti wao, kuna mambo ya dharura yanaweza yakatokezea.

Mhe. Mwenyekiti, *Management* peke yake haiwezi ikamaliza mambo yale, lakini bado akiwa mwenyekiti yupo wanaweza wakashauriana kwa kuweza kuchukua hatua juu ya lile jambo. Yale ambayo yanahusu sera yeye anajua wapi pakuyapeleka na yale yanayohusu utendaji basi vile vile anajua wapi pakuyafikisha ili tatizo lile liweze kufanyiwa kazi.

Mchangiaji mwengine alikuwa Mhe. Mussa Ali Hassan, yeye alikuwa na hoja kama ifuatavyo. Hoja ya kwanza ilikuwa hivi sasa JKU wanalinda, je, kikosi hiki kitakuwa na mafunzo maalum mbali na haya sasa. Kikosi hiki kitakuwa na mafunzo maalum yanayolingana na yale ya askari, lakini hawa watapata mafunzo ya ziada yanayohusiana na utalii na uwekezaji mwengine na mahitaji ya majukumu yao. Kama tulivyokwisha kusikia baadhi ya Wajumbe wameshauri kwamba walinzi hawa pia wawe wanajua lugha mbali mbali za Kimataifa, kwa hivyo, inawezekana pengine tukawaongezea mafunzo yale ambayo yatakuwa yanalingana na ulinzi katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ilikuwa Wakala utakuwa na uhuru gani wa kujitegemea. Sheria imeshaweka mipaka ya utendai kati ya JKU yenyewe na Wakala. Kutakuwa na uwezo wa kukusanya mapato yake wenyewe na kujitegemea katika kujiendesha.

Hoja nyengine ilikuwa, je, watumishi hawa watapata mafunzo nchi za nje. Ufafanuzi ni kwamba kupata mafunzo nchi za nje ni muhimu, lakini itategemea hali na mahitaji ya wakati kama inavyoelezwa katika kifungu cha 39 cha Mswada huu.

Hoja nyengine ya mwisho ya Mhe. Mussa, ilikuwa amependekeza wapatiwe vifaa kama magari na vyombo vya baharini. Ufafanuzi ni kwamba tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa na tayari serikali imejipanga kuwapatia vifaa tofauti kulingana na mahitaji na ukuwaji wa taasisi hii, yakiwemo magari, pikipiki, mawasiliano ya redio na boti kwa maeneo yale ambayo yatahitaji kupatiwa boti.

Suala hili pia lilichangiwa na Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Hussein Baa na wengineo, kwa hiyo, ufafanuzi wetu ni huo. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi wa Chambani, alisema vikosi vina upungufu mkubwa wa mavazi na vifaa hivyo, je, hiki tunachokiunda itakuaje? Kwanza tumeupokea ushauri wake, lakini tunachotaka kumuhakikishia Muheshimiwa na Baraza lako tukufu kwamba tunakubaliana na ushauri wa Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi, hata hivyo kwa sasa hali ni nzuri kwa upande huo, lakini tunamuahidi Mheshimiwa kwamba wakala huu utakapoanza utakuwa vizuri kulingana na maandalizi ambayo tayari yameshafanyika.

Hoja ya pili, ilikuwa Mkurugenzi awe ni Ofisa wa cheo cha juu na atoke JKU na sio sehemu nyengine. Umuhimu wa kwanza utakuwa ni JKU katika kumpata huyu Ofisi. Lakini imewekwa hivyo ili ikikosekana kumpata kutoka katika kikosi cha JKU wapatikane kutoka Idara nyengine kati ya zile Idara Maalum za SMZ.

Tumeona tusijifunge hivyo lakini umuhimu utawekwa. Ninahakika kwa hivi sasa sheria hii ikipita mtaalamu huyu au mkurugenzi huyu tunao uwezo wa kuweza kumpaka JKU kwa sababu wamo.

Hoja nyengine ilikuwa malipo yao yaangaliwe kwa uzito mkubwa.Tunakubaliana na ushauri wake na tunamuhakikishia kwamba watakuwa kama watumishi wa taasisi nyengine zinazojitegemea.

Mtu wa sita alikuwa ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu, yeye tunamshukuru sana kwa hoja zake ambaye yeye alikuja kwenye vifungu moja kwa moja katika kuchangia Mswada huu. Hoja yake ya mwanzo ilikuwa vijana waliopelekwa JKT kutoka Zanzibar bado hawajapata ajira. Hili samahani halikwenda kwenye vifungu lakini ameeleza kile ambacho yeye ameelezwa na baadhi ya vijana ambao wapo JKT.

Lakini kupitia Baraza hili tukufu nataka nilihakikishie Baraza kwamba malengo ya ujenzi wa Taifa katika JKT na JKU sio kupata ajira, bali ni mafunzo ya amali ambayo yamelengwa kumfanya kijana kuweza kujiajiri. Hilo ndio lengo la msingi katika serikali yetu kuweka azma ya vijana wanaomaliza masomo yao kujiunga na JKT na JKU.

Ajira ni fursa ambayo hupata vijana hawa wanapokuwa makambini wakati wa kujenga Taifa kutokana kuwa vyombo vya Ulinzi na Usalama huchukua waajiriwa wao kutoka JKT na JKU, pamoja na hivyo nitafatilia vijana walioko JKT wanaotoka Zanzibar na Tanzania Bara ili kuona na kubaini ukweli wa jambo hilo.

Lakini nataka nitoe indhari kwamba, vijana wengine wanaweza wakawa ule muda wa kutumia JKT haujafika, lakini nafasi hizi za ajira zikawa tayari zimepelekwa JKT. Kwa hivyo, tuelewe kwamba kuwepo kwa JKT na JKU kuna muda maalum ambao kila kijana anatakiwa autumie. Hata hivyo, naliahidi Baraza hili kwamba tutafatilia ili kujua undani wa jambo hili likoje.

Hoja nyengine ilikuwa, je, watakaoajiriwa wapya watatoka JKU au nje. Kwani wasipoajiriwa waliokuwepo JKU suala hili litachukua muda kuweza kuanza. Ufafanuzi ni kwamba wakala utaanza na wale waliokuwepo JKU na kidogo kidogo utakuwa ukiajiri kwa kuwatumia vijana wanaojenga Taifa ndani ya JKU na nje ya JKU pale watakapohitaji watu wenye sifa maalum. Wale watakaotoka nje ya JKU ni wale wenye sifa maalum. Lakini zaidi tutaajiri kutoka JKU na JKT.

Hoja nyenginje ilikuwa ni kwamba ulinzi ushirikishe wananchi wenyewe. Tunakupa ufafanuzi ni kwamba tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa ingawaje hii ni Sera ya Serikali kuwashirikisha katika ulinzi wananchi. Ufichuaji wa uhalifu na mambo mengine unawategemea sana wananchi. Kwa hivyo, na sisi tutajitahidi suala hilo kulifanya kwa nguvu zetu zote.

Hoja nyengine ilikuwa ni kwamba Sheria ya JKU haikutajwa ni ipi. Ufafanuzi ni kwamba Sheria ya JKU ni Sheria ya JKU, Nam. 6 ya Mwaka 2003 ndiyo iliyokusudiwa hapa.

Hoja nyengine ilikuwa watumishi walioshikizwa kutoka Taasisi nyengine ni taasisi gani. Ufafanuzi ni kwamba ni Taasisi hawa ni kutoka JKU na ikibidi watatoka katika Idara Maalum nyengine za SMZ, ndio watumishi ambao watashikizwa kabla ya kuajiri wale watumishi wapya.

Hoja nyengine ni kwamba Mkurugenzi na Mkurugenzi Mkuu, ni ipi sahihi. Kilichokusudiwa ni Mkurugenzi, sio Mkurugenzi Mkuu na hata Kamati hili nadhani waliliona limefanyiwa marekebisho, hilo la Mkurugenzi Mkuu limenakiliwa kimakosa, lakini hasa ilivyokusudiwa ni Mkurugenzi. Sula hili vile vile limeulizwa na Mhe. Joel Thomas, kwa hivyo, jibu lake atakuwa amelipata vizuri.

Hoja nyengine ni ilikuwa ikiwa ni wakala huu wa serikali je, itakuwa *Board Cooperate*. Ufafanuzi ni kwamba wakala sio *Board Cooperate,* bali ni wakala kulingana na Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya Mwaka 2011, kifungu cha 55 imeelezwa nini maana ya Wakala wa Serikali, kwa hiyo, sio *Board Cooperate*.

Hoja nyengine ilikuwa sheria imeingiza *vision* na *mission,* vipi jambo hili. Naomba niliarifu Baraza lako tukufu kwamba tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa kuyaondoa mambo hayo na yatawekwa katika vifungu vyengine kwa namna tofauti badala ya kuwepo hapo ambapo imewekwa.

Hoja nyengine ilikuwa huduma za utalii na nyenginezo, nyenginezo hizi ni zipi. Huduma nyenginezo zilizokusudiwa hapa zitakuwa ni Taasisi za Kibiashara, uwekezaji na taasisi nyengine za umma au watu binafsi. Kama nilivyosema mwanzo hata kama mtu binafsi anataka huduma hii basi tuko tayari kumpa huduma hii.

Hoja nyengine ilikuwa kifungu cha 6(d), je, ni suala la jumla kwa kila muwekezaji au kwa kila anayetaka. Ni kwa wote na sio suala la lazima, ni suala la hiari kwa mtu anayetaka huduma hii basi tutampa huduma hii.

Hoja nyengine ilikuwa wakala umepewa jukumu la kupekuwa na kukamata wakati hili ni jukumu la polisi, vipi jambo hili. Naomba niliarifu Baraza lako tukufu kwamba huu ni uwezo ambao umetolewa kwa Idara Maalum zote kwa sasa kwa kulingana na majukumu yao. Hata hivyo, kifungu hichi kimefanyiwa marekebisho kwa kuongezwa maneno; "...bila ya kuathiri sheria nyenginezo". Yaani kuna sheria nyengine ambazo ambazo zitazingatiwa pia katika utekelezaji wa sheria hii.

Hoja nyengine ilikuwa Mamlaka ya nidhamu ni ipi. Mamlaka ya nidhamu mwanzo wa nidhamu itakuwa ni Mkurugenzi. Yaani Mamlaka ya mwanzo ya nidhamu itakuwa ni Mkurugenzi kulingana na Kanuni za nidhamu za

JKU kwa watumishi walioajiriwa kwa masharti ya kiaskari na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa watumishi raia. Suala hili limeelezwa katika kifungu kilichoengezwa cha 40 na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.Hapa nataka niendelee kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa kuliona hili.

Hoja nyengine ilikuwa ni sifa ya Wajumbe kwamba ni kubwa kuliko ya Mwenyekiti. Ufafanuzi ni kwamba Mwenyekiti anatakiwa kuwa na cheo cha *Kanal* ambacho ni cheo cha juu katika vyeo vya kijeshi. Hivyo, tunaamini kuwa mtumishi aliyefikia cheo hicho atakuwa na uzoefu wa kazi si chini ya miaka 20 wakati Wajumbe wengine wanaweza kuwa na sifa hizo za elimu na uzoefu wa miaka 15 tu na sio miaka 20.

Hoja nyengine ni kifungu cha 21 kimerejea kifungu cha 11 kimakosa. Nakubaliana naye na kifungu hichi kinatakiwa kirejee kifungu cha 14 badala ya kifungu cha 11. Hapa kimeandikwa kimakosa, lakini hasa kifungu ambacho tunatakiwa tukinukuu ni kifungu cha 14 badala ya kifungu cha 11.

Hoja nyengine ilikuwa ni kupitisha kumbukumbu katika bodi sio utaratibu kuweka katika sheria. Tunakubaliana na Mheshimiwa na marekebisho yanafanywa, yaani maelezo yasomeke; "Kuishia kumbukumbu za mikutano" na yale mengine kuthibitisha  na kufanya nini, yale hayana haja ya kuwepo katika sheria.

Hoja nyengine ilikuwa taratibu za maamuzi ya vikao vya Bodi. Tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa na hili litafanyika katika hali ya dharura tu ambapo Wajumbe hawawezi kukutana. Vyenginevyo, kutakuwa na ulazima wa kufanyika kwa vikao vya dharura.

Yaani hili ilikuwa hoja yake ni kwamba tusitumie utaratibu wa kupeleka *circular*  kwa kusaini wajumbe wa Bodi kufanya maamuzi. Sasa ndio tunasema utaratibu huu utatumika kwa sababu hata pale unapoletewa *circular* unayo haki ya kukataa ile *circular* uliyoletewa na kutoa sababu zako isipofikia, idadi ya *quorum* iliyokubalika kwa mujibu wa sheria, ina maana jambo hilo haliwezi kuwa limepita.

Kifungu cha 38, kimesema; Tume, sasa anauliza Tume ipi? Hii ni Idara Tume ya Utumishi, Idara Maalum za SMZ, sio Tume nyengine yoyote ile ya Utumishi. Tume ya Utumishi Idara Maalum ndicho kitakachokuwa chombo kitakachohusika baada ya mambo yale kupita katika ngazi zile zinazohusika kupita katika Bodi na hatimaye inaweza ikenda kwenye Tume ya Utumishi Idara Maalum.

Mgongano wa kifungu cha 40 na 16(1). Kifungu cha 16(1) kimefanyiwa marekebisho na sasa kimeweka jumla ya viwango vya malipo vitapendekezwa na Bodi na kifungu cha 40 kuidhinishwa na waziri baada ya mapendekezo ya Bodi.

Mchangiaji mwengine alikuwa ni Mhe. Fatma Mbarouk Said, hoja yake ya mwanzo ilikuwa ni madhumuni na sababu hazikuoneshwa vizuri. Nataka ni nimfahamishe Mheshimiwa kwamba hii madhumuni na sababu sio sehemu ya sheria isipokuwa zinatoa ufafanuzi na kusaidia uwasilishwaji wa sheria. Hata hivyo, madhumuni na sababu zimeelezwa kwa uzuri katika hati ya kuwasilisha Mswada huu kwa hati ya dharura, zimeelezwa vizuri sana, lakini hii huwa sio sehemu ya sheria.

Hoja nyengine ya Mheshimiwa imekuwa ni kujiuzulu kwa Wajumbe. Suala hili tutalirekebisha ili kwenda sambamba na Katiba  ya Zanzibar. Yaani tutalirekebisha kwenye sheria, tumeshalifanyia marekebisho ili lende sambamba na Katiba ya Zanzibar.

Hoja yengine ilikuwa hajaona kifungu kinachoelezea namna ya kuwasilishwa Hesabu kwa Mdhibiti na Mkatubi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ufafanuzi ni kwamba maelezo yanayopatikana katika kifungu cha 31 cha Mswada, lakini pia, jambo hili ni la lazima kwa kila taasisi ya serikali kulifanya...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe mnaotoka Mhe. Waziri anamalizia, naomba murejee ndani ili tuweze kupitisha vifungu badala ya kutoka nje. Ahsante. Mhe. Waziri, tuendelee.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Maelezo ni kwamba yanapatikana katika kifungu cha 31 cha Mswada, lakini pia, jambo hili ni la lazima kwa kila Taasisi ya Serikali kulingana na Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hivyo, hata kama sheria hii haikusema lakini ile Sheria ya

Mdhibiti na ni Taasisi ya Serikali lazima iweze kufanya au kuifata ile Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mchangiaji mwengine wa nane alikuwa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, yeye alizungumzia juu ya suala la kuteuliwa tena kwa Bodi maana yake ni nini? Bodi ni ya kudumu, Bodi ni Taasisi, wajumbe ni watu, kwa hivyo, Bodi ni chombo cha kudumu mpaka pale sheria hii itakapoamua kufutwa. Lakini wakati sheria hii inafanya kazi, Bodi inakuwa ni Taasisi ya Kudumu, wajumbe wanakuwa ni wamuda baada ya miaka 3 au kulingana na sheria nyengine akiamua mwenyewe kujiuzulu anakuwa si mjumbe.

Halafu aliongezea suala lile lile la Mwenyekiti kutumikia katika Bodi hiyo ambayo ni miaka 3 kwa wajumbe wa kawaida na miaka iwe kwa Mwenyekiti. Maelezo yangu nilisema kule, madhumuni na sababu tulizoweka hivi ni kwamba tunaepusha ule upya na tunaepusha vile vile wakati inapotokezea pengine hoja kubwa ambayo *management* peke yake haiwezi kuamua, ni vizuri washauriane na Mwenyekiti, ambaye Mwenyekiti yeye anaweza akenda kwa Mhe. Rais aliyemteua kuweza kumuelezea lile jambo ambalo lina haja ya kuweza kulifanyia kazi. Suala jengine lililojitokeza kwa Mheshimiwa, lilikuwa ni kujiuzulu kwa wajumbe wahakikishe kuwa Bodi itakuwa salama na ni lazima mjumbe aeleze sababu.

Ni kweli hatuwezi kumruhusu mjumbe ajiuzulu iwapo atakuwa ametenda kosa katika muda wake, pengine muda wake wa kuvunjwa Bodi haujafika, lakini kwa sababu kuna jambo analihofia ambalo amelitenda ndani ya utendaji wake wa kazi itabidi lazima tuzingatie suala hilo.

Suala jengine ameomba kufanyiwa Semina kwa wajumbe, hili limerejewa na hata Mhe. Saleh, maana hii yamezungumziwa suala la wadau kwamba lazima Mswada huu urudi kwa wadau, semina tulitoa na wadau wengi walishirikishwa kama walivyokwisha kusema dokta Mwinyi leo mchana na Mhe. Said Ali Mbarouk, jambo hili chanzo chake sio Serikali, jambo hili chanzo chake kilitokana na Baraza la Biashara, ombi hili lilitoka mwanzo pale kwa wawekezaji wenye sekta ya utalii, ndiko lilikoanzia.

Kwa hivyo, walianza kushirikishwa hao wadau na watu wengine walishirikishwa na mwisho tulimalizia kwa waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mimi orodha ninayo ya nani na nani alishiriki kwenye semina ile pale Zanzibar *Ocean View,* mkihitaji niwaoneshe ninayo nitawaonesha. Kwa hivyo, huu mswada umekwenda kwa wadau, orodha ninayo nimeiomba kwa wahasibu wamenipa na mkihitaji kila yule aliyesema nitamwambia jina lako hili, umeshiriki na umetoa maoni, sasa hatuwezi tena leo hapa tukaja tukasema Mswada huu uondolewe uende kwa wadau, wadau wepi?

Mchangiaji mwengine alikuwa Mhe. Hamza Hassan Juma, hoja yake ya kwanza ilikuwa mafunzo tuliyoyapata JKT ni kuwa walianza Shirika la Suma JKT na iwe Shirika ikaunda Suma *Guard,* wakati sisi tumekwenda wakala moja kwa moja. Ni kweli nakubaliana nae Mhe. Hamza, kwamba wenzetu Suma JKT walianza na Shirika, lakini sisi kwa nini tunakwenda kwenye wakala wa ulinzi kwa sababu tunahisi tungekwenda moja kwa moja kwenye Shirika, tungechelewa na haja ya sasa ilivyo, kama tunavyoona Mhe. Hamza, hivi sasa uhalifu katika maeneo ya uekezaji umeongezeka.

Kwa hivyo, tukaona ni bora kwanza tuwahi kuweka hii wakala wa ulinzi katika maeneo ya uwekezaji na biashara halafu tukikuwa huko tutakwenda katika ile azma nzima kama walivyokwenda wenzetu wa Suma JKT. Lakini sisi madhumuni yetu ni hayo ni kwamba tumeona hivi sasa tuje na mahitaji ya matatizo tuliyonayo hivi sasa yanayohitaji hatua hii tuliyochukua, Shirika linahitaji mambo mengi ambayo yangechukua muda mrefu kuyatimiza. Kwa hivyo, utakapofika muda wa kuwa Shirika tutakwenda kwenye Shirika, tutakuja tena kwenu ili kufanya marekebisho ili sheria hii itambue kuwepo kwa Shirika badala kuwepo kwa wakala.

Hoja nyengine ilikuwa ni kifungu cha tatu, tuongeze biashara na wafanyabiashara, tumezingatia hilo Mhe. Hamza, tumeongeza biashara, maeneo ya utalii, maeneo ya uekezaji, maeneo ya biashara na hata watu binafsi. Mhe. Hamza hata wewe ukihitaji ulinzi nyumbani kwako kwa njia hii ya biashara ama ni Mwakilishi, ama ni raia mwema tutakuletea ulinzi.

Hoja nyengine ilikuwa ulinzi na suala la Muungano, je, tuna sera ya ulinzi? Ufafanuzi ni kwamba sera ya ulinzi ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini inatoa fursa kwa Zanzibar kuanzisha vyombo vya ulinzi kama hivi, yaani kuanzisha hizi Idara na wakala zinazoshughulikia masuala ya ulinzi.

Hoja nyengine ilikuwa kuanzishwa kwa wakala hakutaleta migongano na Kampuni binafasi zinazotoa huduma za ulinzi. Sisi Serikali tunahisi kuanzishwa kwa wakala hapatakuwa na mgongano kwani yeyote anayetaka kulinda ataingia mkataba na Kampuni au Taasisi inayotaka kumlinda. Isipokuwa katika sheria hii sasa hivi wakala ndio atakaekuwa ana waratibu hawa Makampuni ya Binafsi. Tukiri kwamba na hapa limezungumzwa sana suala la kuwa na hofu juu ya kampuni zetu ambazo zinalinda za wananchi, tunachosema hatutaifuta kampuni, isipokuwa kampuni itatakiwa ifate masharti ya kutoa ulinzi ulio bora na wenye viwango na itabidi lazima tuweze kuzipitia hizo kampuni.

Kwa sababu kuna kampuni nyengine zinaweka walinzi ambao hawana uzoefu, unaweza ukapita kwa mlinzi analinda Taasisi mlinzi amevaa *uniform* anatoa saluti kwa mkono wa kushoto, sasa huyo hawezi kuwa mlinzi. Ni dhahiri inaonesha kwamba yule hana taaluma ya ulinzi, kwa hivyo, tutakachofanya sisi ni kuhakikisha wale wanaoweka kampuni za ulinzi wanafata vile viwango ambavyo vinakubalika ili athari na matokeo ya kiuhalifu yasiweze kutokea.

Ofisi ndogo zisiwekwe masharti Unguja na Pemba bali wenyewe waachiwe kuangalia mahitaji. Nadhani wako wajumbe ambao walitaka iwe hivyo, lakini sisi tunakubaliana na Mhe. Hamza na maoni aliyoyatoa na sisi ndio madhumuni ya sheria yetu inavyosema. Tuwasiliane na ndugu zetu wa Tanzania Bara kubadilishana uzoefu, ni jambo jema tunakubaliana nalo tutaendelea kubadilishana nao uzoefu kama tunavyofanya hivi sasa.

Mhe. Abdalla Juma, yeye alikuwa na hofu, mimi nina hakika Mswada huu yeye tokea kwenye Kamati aliukubali na alitoa mchango wake, lakini nadhani baadae akaona bora aje aseme maoni yake. Hofu yake ni kwamba uwakala huu usije ukatumiwa vibaya, matumizi ya vikosi na utaratibu wa ukamataji. Nadhani nimesema kwamba askari wa wakala watakapotekeleza majukumu yao kule mwanzo nimesema watazingatia sheria hii na sheria nyengine.

Kwa sababu sheria hii haiwezi kufanya kazi peke yake, sheria hizi zinategemeana; kuna sheria ya makosa ya jinai na kuna sheria nyengine za Jeshi la Polisi ambazo zinahusu masuala ya upekuzi na ukamataji, kwa hivyo, humu imewekwa makusudi ili asije akatokea mtu akasema huna mamlaka ya kunipekua. Na uzoefu huu tunao katika Idara zetu zote za SMZ kimo kifungu hiki cha askari kumkamata mtu na kufanya upekuzi, lakini anapotekeleza hilo lazima afate yale masharti ambayo yamewekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Kwa hivyo, nina imani Mheshimiwa sisi Serikali unajua kwamba hatuna nia ya matumizi ya vikosi, vikosi vinafanya kazi nzuri ya kulinda nchi na mali za wananchi ambao wanazingatia sheria. Sasa yule ambaye atakuwa hazingatii sheria sasa utaratibu kwa kuitumia sheria hii katika maeneo yale yaliyokusudiwa sheria hii itabidi lazima ifatwe.

Mhe. Salma Mohammed Ali, yeye ni mmoja kati ya wajumbe watatu waliosema tokea mwanzo kwamba hawakubaliani na sheria hii. Mimi nataka nimuombe Mhe. Salma, aondoe mawazo yake hayo na akubaliane na sheria hii, hatuna nia hiyo hata chembe. Nia yetu ni kuweka utaratibu mzuri wa kulinda uwekezaji wa aina zote na wafanyabiashara. Nchi yetu hii sasa hivi wote hapa tunaimba wimbo kwamba inategemea sekta ya utalii, wawekezaji ndio ambao wameonesha hofu.

Namba yetu Mhe. Waziri wa Utalii amesema asubuhi kwamba namba ya watalii imeongezeka, kwa nini imeongezeka? Imeongezeka kwa sababu ndani ya ukanda wa Bara la Afrika kuanzia Misri, Kenya na kwengineko watalii sasa wamekuwa hawendi pahala pakukimbilia ni Zanzibar.

Sasa sisi tumeamua kufanya hili jambo, kwanza ni jambo ambalo lililetwa na wananchi wenyewe kwa maana ya wadau, yaani wahusika wengine, watu wa sekta ya utalii na wafanyabiashara. Na ukizingatia matukio mabaya kama takwimu alizozitoa Mhe. Waziri wa Utalii, matukio 80 yametokea mwaka jana na matukio 60 yametokea mwaka huu, tukisema tunakaa tu bila kuzingatia kuwalinda wawekezaji wetu, ina maana nchi yetu itakuwa mbaya zaidi kiuchumi, hatuwezi Serikali kubaki huko.

Kwa hivyo, kikosi hiki kitakuwa kinajitegemea na kitakuwa na mapato yake, vikosi viliopo vinafanya ulinzi wa jumla sio kulinda biashara, ndio maana tukaanzisha chombo hiki ili anayetaka kulindwa kibiashara katika sehemu yake apewe fursa hii. Tunataka vile vile kuondosha, hivi sasa kuna askari wetu wa JKU, Valantia na nini, wanalinda katika maeneo ya uwekezaji. Tunachotaka kufanya ni kutofautisha kati ya walinzi wa mambo ya jumla ambao siku yasiku likigarambuka wote wanakwenda mstari wa mbele.

Hawa ni maalum ambao hawatawatisha watalii na wale watu wanaotaka kuja kufanya biashara Zanzibar, unajua wale waliofunzwa kijeshi jeshi wale wakikaa pale ni tatizo, ndio maana Serikali tumeona tufanye hivyo. Kwa hivyo, hawa watakuwa ni askari maalum na waliopata mafunzo maalum, yanayolingana na kulinda katika maeneo ya biashara na wale wa kwenda mstari mbele wale tutawaacha huko maporini na kwenye makambi yao ili waweze kutekeleza majukumu ya kulinda nchi kwa ujumla.

Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Wawi na yeye amekuja na kauli kidogo ameniita ndugu yake, mdogo wake na mimi nakubali yeye ni kaka yangu, lakini mimi nadhani saa nyengine tunakuwepo kwenye hivi viriri tusitafute lugha ambazo zinawafanya wananchi huko watuelewe vyenginevyo. Kwa mfano ile akipewa sindano atalipa mtaimbo, mimi nafikiri haikuwa lugha safi ya kuisema kwenye Baraza hili, kwa sababu wenye kazi zao wakiamua kumtafuta sasa kumuuliza alikuwa na nia gani, atasema nini?

Pamoja na kwamba tunayo kinga lakini kinga hiyo lazima tuitumie vizuri, sasa mimi sitaki nikariri yale ambayo ameyasema, lakini nataka nimsihi kidogo kwamba anapozungumza baadhi ya lugha aangalie lugha nyengine zinakuwa hazistahili kuzungumzwa hasa kwenye chombo kikubwa kama hiki, wenye kazi zao wapo, wanaweza wakakutafuta wakakuuliza halafu ikawa balaa, mimi nadhani sio vizuri.

Yeye alizungumza Mswada kuletwa kwa hali ya dharura ni dharura gani, ni dharura zile ambazo zimeelezwa kwenye hati ile aliyoiwasilisha Mhe. Mwanasheria Mkuu na zile ambazo zimeelezwa kwenye sheria, hakuna dharura nyengine, ni uharaka tu wa kutaka hili jambo au hii sheria itekelezwe haraka kulingana na mahitaji ya sasa yalivyo. Kwamba tuna biashara ambayo ni tete tunataka hii biashara tuwape moyo wawekezaji, juzi Mhe. Rais kwenye sherehe za Mapinduzi alitangaza kuwepo kwa mji mpya kule Fumba.

Mji kama ule wa Fumba tunatarajia vile vile uwekezaji kama ule ufanyike katika maeneo kama ya Bwawani, Darajani *corridor,* kuna hoteli moja kubwa sana ya vyumba 500 kule Muyuni, Kaskazini "A" inataka kujengwa na kuna kiwanja cha ndege kidogo kitajengwa. Sasa haya yanahitaji kuwa na ulinzi wa uhakika, ndio udharura na uharaka ambao umetufanya sisi Serikali tuamue kuuleta kwa hati ya dharura na si dhana nyengineyo, huu Mswada hata kidogo haukusudii uchaguzi. Suala la uchaguzi ni suala mbali na suala la sheria hii ni suala mbali. *(Makofi)*

Mbali na maelezo niliyoyatoa katika maelezo ya uwasilishaji wa hati ya dharura, maelezo ya ziada ya dharura ya suala hili ni pamoja na maelezo ya Mhe. Dokta Mwinyi na Mhe. Said Ali Mbarouk, yale waliyoyatoa mchana, yale pia yamefanya huu Mswada uwe wa dharura. Matokeo yaliyotokea Kenya na nchi nyengine zinazotegemea Utalii kama Misri na nyenginezo yanatusukuma kuanzisha uwakala huu kwa wakati huu ili kujihami na kujenga imani ya wawekezaji wetu.

Hoja nyengine ilikuwa chombo kuundwa kwa malengo ya Kisiasa kama nilivyokwisha kusema kwamba hatuna chembe ya kukiunda chombo hiki kwa malengo ya kisiasa. Chombo hiki kimeanzishwa kwa lengo la kulinda uchumi wetu na sio kwa siasa na siasa hairuhusiwi katika vyombo vya ulinzi. Pia, kwa mfumo wa utawala hapa Zanzibar chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hatuna upinzani ambao Serikali una lengo la kuudhuru kupitia uwakala huu. Au Waheshimiwa Wawakilishi niwaulize ndani ya nchi humu ndani ya Baraza kuna *opposition party?* Humu kuna chama kishiriki naomba niishie hapo.

Hoja nyengine ilikuwa kauli ya kuwa yeye atalipa mtaimbo nishaisema, sitaki niirejee, maelezo yangu ni yale yale nimsihi kaka yangu huyu kama alivyoniita ndugu yake na mimi nakiri kwamba ni ndugu yake nimsihi kauli nyengine zinakuwa hazijengi insafu nzuri katika kufanya kazi ya kuwatumikia wananchi. Ninachoweza kusema kwamba nchi yetu ni ya amani, tunaomba ibaki kuwa ya amani tusipandikize chuki kwa kutumia jambo ambalo limelenga manufaa ya nchi yetu, hakuna atakaefaidika na balaa likizuka nchini, tujifunze kwa wenzetu wanaopata tabu kutokana na kulipizana visasi.

Hoja nyengine ilikuwa Mswada urudi serikalini ili kupata maoni ya wadau, nimeshasema, mmoja kati ya watu niliowaona katika orodha ya wadau walioshiriki ni pamoja na Mhe. Saleh Nassor. Sasa sijui alitaka tuandae kikao kipi cha wadau, orodha ninayo anayetaka atakuja kuona.

Mswada utaua ajira ya Wamasai, UMAWA na vijana wanaofanya kazi za ulinzi. Mimi nadhani nimeshatoa ufafanuzi kwamba Mswada huu hauuwi hizo ajira, kwa sababu hatuji kufuta zile kampuni nyingine, hapana.

Tunachoweka ni utaratibu mzuri wa zile kampuni za ulinzi kufanya kazi kwa mazingira mazuri, wao watapewa taaluma ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi. Mswada huu una lengo la kuwatengenezea ajira kwa vijana ambao watachukuliwa kutumia uwakala kwa upande mmoja na upande wa pili kuratibu shughuli za ulinzi za hizo taasisi nyengine na sio kuzizuia wala kuziondosha kabisa.

Suala jengine la Mhe. Saleh, ilikuwa Mswada umekiuka Katiba kuhusiana na haki ya kuishi na kuingilia haki za Jeshi la Polisi. Nataka nisikubaliane nae, Mswada huu hauna hali hiyo kwani umezingatia sheria ambazo zinapaswa kuzingatiwa na watumishi katika kutekeleza majukumu yao chini ya kifungu hiki, lakini hata kifungu cha 7(c), kimefanyiwa marekebisho kuingiza maneno kwa kuzingatia sheria.

Yaani ili utekeleze kifungu hiki, lazima uzingatie sheria nyengine, matumizi ya nguvu yatazingatia sheria zilizopo.Kutoshitakiwa hapa ni kwa mtumishi binafsi kama atatenda kulingana na sheria, lakini akikiuka sheria huyu anakuwa hana kinga kwa mujibu wa kifungu hiki. Na nawaomba wajumbe tukisome vizuri kile kifungu kinavyoeleza, kwa sababu karibu hata huko kwenye Jeshi la Polisi. Kwa mfano, mimi nitapenda kulitolea mfano hili tukio la juzi. Miongoni mwa wale ambao wamekamatwa na kuyapata waliyoyapata ni jambazi sugu na walikuwa na silaha.

Sasa mtu kama yule kama angeamua ile silaha aichukue angepoteza maisha mengi sana pale ya wananchi, kama asingewahiwa. Sasa inapotokea hali kama ile askari lazima watumie zana zao.

Ni jambazi sugu, ana matukio mengi ambayo ameyafanya Tanzania na Zanzibar, ameshafungwa jela, akitoka kazi ni ile ile. Sasa haya mambo jamani lazima tuelewe katika mazingira ya kileo hatuwezi kwenda vile. Kwa hiyo, lazima askari nae usipompa kinga kwa tukio kama lile la juzi, tutakuwa na askari humu ndani? Hatuwezi kuwa na askari na vijana hawa watavunjika moyo, kwa sababu kufariki mtu ni jambo lililoelezwa na Mwenyezi Mungu kwamba kuzaliwa na kufariki ni lazima. Lakini kufariki kwa tukio lile la juzi kama mlibahatika kwenda pale Darajani mngewaona ni kwa jinsi gani wananchi walivyotoa mashirikiano kwa tukio lile la juzi.

Sasa inapotokezea tukio kama lile la juzi, askari kwa sababu waliamua kupiga silaha juu lakini wakakaidi amri, sasa ungetegemea iweje? Kwa hiyo, inapotokezea bahati mbaya kama ile askari huyu usipompa kinga hivi itakuwa tunawatendea haki askari. Lakini hawezi kutumia silaha kwa mtu mwenye firimbi, hawezi kufanya hivyo au kwa mtu mwenye kirungu, lakini anapoamua kufanya hayo *against* na hivi maana yake sheria nyengine zile hana kinga katika hilo, sheria zimeeleza na tumezitaja sheria mbali mbali hapa.

Mhe. Hassan Hamad Omar, mswada unataka kuibadilisha JKU kutoa kuwasaidia vijana kuwa wakakamavu na kulifanya Jeshi la Ulinzi. Hapana, hiki ni kikosi cha ulinzi katika maeneo ya uwekezaji wa aina zote, biashara lakini hata kwa mtu binafsi kama nilivyosema mwanzo. Mswada hauna nia hiyo kwani unazungumzia masuala maalum yanayohusiana na kufanya kazi ambazo hivi sasa zinafanyika, lakini unaziweka kisheria zaidi hivi sasa.
Suala la ulinzi wa jumla liko chini ya Jeshi la Wananchi na hapa tunazungumzia suala la maeneo ya uwekezaji na vikosi vyengine vikiwemo Vikosi vya Idara Maalum na hata Jeshi la Polisi, Magereza kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Ulinzi na Usalama hivi vyote vinakuwa ni vikosi vya akiba, jeshi linatangulia mbele na hivi vinakuwa ni vikosi vya akiba na mfumo huu ni katika nchi zote duniani ndivyo ulivyo. Kwa hiyo, hiki ni kikosi tofauti kabisa na hawa kama nilivyosema mwanzo.

Kifungu cha 5, kiongezwe maneno na makaazi ya raia, ulinzi wa raia na mali zao ni kazi ya Jeshi la Polisi na JKU na Idara nyengine Maalum kushiriki pale zinapopata maagizo baada ya kuombwa na Jeshi la Polisi.

Mhe. Marina Joel Thomas, masuala yake mengine nimeshayatolea ufafanuzi. Jina kuwa wakala, taasisi au shirika, ni kwamba jina sahihi ni wakala au jina halisi ni wakala wa serikali, wakala wa ulinzi wa serikali na tafsiri ya wakala kama nilivyosema imetafsiriwa katika sheria ile ya utumishi wa umma.

Ajira itoke JKU kwa kuwatumia vijana, tunakubaliana nae madamu vijana hao watakuwa na sifa za ajira katika Idara Maalum basi wata-*qualify* vile vile kuajiriwa katika chombo hiki.

Vifaa viwe vya kisasa, tunakubaliana na Mheshimiwa na hilo limo katika mipango yetu ya kuanza kwa kikosi hiki.

Mhe. Rufai Said Rufai, kuhusiana na marekebisho katika Mswada. Tunakubaliana na Mheshimiwa kuhusiana na marekebisho na tunaahidi kuyafanyia kazi kama tulivyokwisha kuyafanyia kazi yale ambayo tumepewa na Wajumbe wa Kamati.

Suala jengine alisema katika majukumu ya Mkurugenzi, jukumu la kuandaa mpango wa biashara kwa wakala liondolewe, tunakubaliana naye Mheshimiwa.

Mtu wa kumi na sita alikuwa Mhe. Mohammed Haji Khalid, nae alikuwa ni miongoni mwa wajumbe watatu waliokataa Mswada huu, lakini kama nilivyotoa nasaha kwa wale wawili na yeye nasaha zangu ni zile zile. Sheria kama haikutaja makosa hapa, maana yake si kosa. Kifungu cha 36 kinaelezea wazi kuwa kama mtu amefanya kosa, lakini halikuelezwa hapa na wakati huo huo lipo chini ya sheria nyengine, sheria hiyo itatumika katika kumtia makosani.

Suala jengine lilikuwa watalii na wahalifu kuwa na silaha wakati silaha hairuhusiwi hapa Zanzibar. Ni kweli lakini silaha kikawaida hazipiti bandarini, bali watu hutumia maeneo wasiotambuliwa kupitisha vitu vya aina hiyo. Sheria bado inatambua kuwa ni makosa na hatua zitachukuliwa kwa yule atakayekamatwa na silaha.

Suala jengine kwa nini JKU isiwe na vitengo vyengine vya biashara, ulinzi na mambo mengine. Hivi sasa inayo baadhi ya vitengo vya aina hiyo, lakini mipango ya baadae ya JKU ni kuwa ni Shirika la Biashara ambalo litakuwa na vitengo hivyo. Yaani JKU inayo adhma hiyo hapo baadae.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, ametupa pongezi tunakubaliana na pongezi zote nadhani kutokana na muda maeneo yake mengine tumeshayatolea ufafanuzi, naomba aridhike na ufafanuzi ambao nimeutoa.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, yeye kwa kweli nataka nimshukuru pamoja na Mhe. Saidi Ali Mbarouk, ametoa ufafanuzi ambao umesaidia sana Waheshimiwa katika kufahamu adhma ya mswada na sababu zilizochangia kuleta mswada huu. Kama nilivyosema pale mwanzo yeye ameeleza chimbuko la mswada huu ni nani? Sina haja ya kurejea, *Hansard* zipo zitaweza kutoa ushahidi juu ya yale ambayo serikali imeeleza.

Mhe. Said Ali Mbarouk na yeye nataka nimshukuru ametoa ufafanuzi ambao umewasaidia sana waheshimiwa katika kufahamu adhma ya Mswada na sababu zilizochangia kuleta pia, amefafanua hali ya utalii ilivyo sasa na haja ya kulinda utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine naomba kukushukuru tena wewe na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuchangia mswada huu na naamini wameridhika na jinsi tulivyofanyia kazi ushauri wao na hoja zote za Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na wajumbe mmoja mmoja waliochangia mswada huu.

Tukiendelea kushirikiana kwa namna hii, kila zito litakuwa jepesi na namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tudumishe mshikamano wetu ili tuweze kuwatatulia wananchi na wageni wetu matatizo yanayowakabili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, ahsante kwa namna ambavyo umetoa ufafanuzi mbali mbali kwa nia ya kupunguza mabuti. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaoafiki kuunga mkono Mswada huu wanyooshe mikono juu, wasioafiki. Wanaoafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

**KAM ATI YA KUTUNGA SHERIA**

**Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Ulinzi ya JKU, 2015**

**Sehemu ya Kwanza**

**Masharti ya Utangulizi**


Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 2 Matumizi ya sheria
Kifungu 3 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake


**Sehemu ya Pili**

**Kuanzisha kwa Taasisi ya Ulinzi ya JKU Pamoja na Kazi Zake**


Kifungu 4 Kuanzishwa wakala wa ulinzi wa JKU
Kifungu 5 Malengo ya Taasisi ya Ulinzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 6 Kazi za Taasisi ya Ulinzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7 Uwezo wa Taasisi ya Ulinzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 Wajibu wa kulipa ada na malipo mbali mbali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9 Sifa za kuteuliwa Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10 Majukumu ya Mkurugenzi
Kifungu 11 Vitengo vya Taasisi ya Ulinzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12 Wakuu wa Vitengo pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13 Watumishi wa Taasisi ya Ulinzi
Kifungu 14 Kuanzishwa kwa Bodi ya Taasisi ya Ulinzi
Kifungu 15 Sifa za Mwenyekiti wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16 Uwezo wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 17 Kazi za Bodi
Kifungu 18 Muda wa Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake
Kifungu 19 Sifa za Wajumbe wa Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20 Muda wa Wajumbe wa Bodi
Kifungu 21 Kusimamishwa na kukatishwa ujumbe wa Bodi
Kifungu 22 Kujiuzulu kwa Mjumbe wa Bodi
Kifungu 23 Vikao vya Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 24 Maamuzi ya Bodi pamoja na marekisho yake
Kifungu 25 Akidi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 26 Mtu asiye Mjumbe kuhudhuria vikao vya Bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 27 Malipo ya posho pamoja na marekebisho yake
Kifungu 28 Majukumu ya Katibu wa Bodi


**Sehemu ya Tatu**

**Mapato, Matumizi na Usimamizi wa Fedha**


Kifungu 29 Vyanzo vya mapato vya Taasisi ya Ulinzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 30 Matumizi ya bajeti
Kifungu 31 Akaunti za benki na matumizi
Kifungu 32 Ukaguzi wa hesabu
Kifungu 33 Uwekezaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 34 Taarifa za kila mwaka


**Sehemu ya Nne**

**Mengineyo**

Kifungu 35 Makosa na adhabu
Kifungu 36 Makosa ya jumla
Kifungu 37 Kinga kwa…

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki mimi bado kinanipa wasi wasi, nilipokuwa nikichangia nilijenga hofu kuwa mtumishi akifanya kazi yake na kasababisha ama uharibifu wa mali au hata kuua kuwa yeye hakuchukuliwa hatua yoyote. Kwa kweli hii ni kinga kubwa mno aliyopewa mtumishi huyo na kwa sababu watumishi ni watu wa kawaida kama sisi anaweza…

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa Mjumbe, naomba uende kwenye hoja.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Naam.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nenda kwenye hoja yako moja kwa moja.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Kifungu hiki kinanipa wasi wasi kwa kinga aliyopewa mtumishi ni kubwa mno, ndio hoja yangu.

**Mhe. Mwenyekiti:** *Inshaallah* Mhe. Waziri msaidie majibu ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa nilipokuwa nikitoa ufafanuzi sikumuona pale, lakini imejieleza vizuri sana kwamba ukikisoma mpaka mwisho kifungu hiki hayo mashaka ambayo wanayo hayapo. Kwa sababu hata askari waliopo sasa wanatakiwa watumie kifungu kama hiki, lakini kwa kufuata sheria ziliopo, hana kinga iwapo atakuwa amefanya jambo lile kumdhibiti muhalifu kinyume na sheria ziliopo na hiki ndivyo kinavyosema.

Kwa sababu alikuwa anakielezea, yeye alikuwa anakisema mpaka katikati, lakini akisome mpaka mwisho, akikisoma mpaka mwisho hiki kifungu hakina matatizo na maelezo nimeyatoa sana pale mpaka Mwenyekiti umeniletea *memo*, kwamba muda makusudi ili Mhe. Mohammed Haji Khalid afahamu, lakini alikuwa hayumo ndani. (*Makofi)*

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Pamoja na kuwa sikuwemo ndani, lakini nilimsikia Mhe. Waziri kwa sababu nilikuwa nimo katika jengo. Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu mimi sijakisoma nusu nusu nimekisoma chote na nimefahamu kama kilivyokusudiwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mohammed Haji Khalid, bado mimi sijakufahamu pia, kwa sababu Mhe. Waziri amekwishakuelezea na ameelezea wakati wewe mwenyewe hupo na ametolea tena ufafanuzi sasa hivi na ameelekeza kwa hali halisi ilivyo. Sasa bado wewe hujafahamu kitu gani naomba unisaidie zaidi ili niweze kukusaidia.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Wasi wasi wangu upo lakini kwa kuwa tumefikia hivyo na tuendelee.

Kifungu 37 Kinga kwa mtumishi
Kifungu 38 Fidia kwa maumivu, ulemavu na kifo
Kifungu 39 Mafunzo kwa watumishi
Kifungu 40 Uwezo wa waziri kutunga kanuni pamoja na marekebisho yake

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe tuwahoji wanaoafiki mikono juu. Wasioafiki, walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Ulinzi ya JKU, 2015**

*(Kusomwa kwa mara ya tatu)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Ulinzi ya JKU, 2015 sasa usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwahoji wanaoafiki mikono juu. Wasioafiki, walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)*

**Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015**

*(Kusomwa kwa mara ya pili)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na kwa heshima kubwa naomba kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku hii ya leo tukiwa na afya njema. Napenda kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuwajibika na kutekeleza majukumu yenu ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kuchukua nafasi hii kutoa maelezo yangu juu ya kuwasilisha Mswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa hati ya dharura kutokana na hali halisi ya mswada huu ikiwa ni pamoja na sababu kuu zifuatazo:

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Zanzibar inashuhudia uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira ambao udhibiti wake unahitaji msukumo mkubwa wa kisheria na kitaasisi kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa maendeleo endelevu Nam. 2 ya mwaka 1996 na mfumo wa kimazingira uliopo hivi sasa haukidhi matakwa ya kuweza kudhibiti uharibifu na uchafuzi wa mazingira unaoendelea kuongezeka siku hadi siku ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama vilivyo visiwa vingi duniani Zanzibar nayo inakabiliwa na athari kubwa zinazoambatana na mabadiliko ya tabianchi. Sekta zote za kiuchumi ikiwa ni pamoja na utalii, uvuvi, kilimo, makaazi na nyenginezo zinaathiriwa sana na mabadiliko ya tabianchi na kama hatua za dharura hazitochukuliwa ni wazi kuwa Zanzibar inaweza kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea ya kiuchumi. Hivyo ni vyema kuwa na mfumo wa kisheria utakaosaidia kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi ili kupunguza athari hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hivi sasa Zanzibar inakusudia kujihusisha na utafutaji wa mafuta na gesi, ni wazi kuwa shughuli ya utafutaji wa masuala ya mafuta na gesi pamoja na uchimbaji wake kama haukudhibitiwa kimazingira unaweza kuleta athari mbaya kwa jamii, mazingira na uchumi kwa jumla. Hivyo, Sheria ya Mazingira lazima iwe na vifungu vinavyoelezea masuala ya mafuta na gesi mambo ambayo hayakuzingatiwa kwenye sheria iliyopo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya kuhami mazingira ya Zanzibar yasiendelee kuharibiwa na kuchafuliwa na kwa ajili ya kuhakikisha kuwa utafutaji na uchimbaji wa mafuta unakuwa salama pamoja na kuhakikisha kuwa masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanasimamiwa kisheria, ni dhahiri kuwa kuna kila sababu ya kuuleta Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar mwaka 2015 kwa hati ya dharura kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Madhumuni na Sababu za Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuweka mfumo bora wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi wa mazingira. Uwekaji wa mfumo huo unatokana na haja iliyopo kwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

1. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa maendeleo endelevu Nam. 2 ya mwaka 1996 iliyopo hivi sasa inatoa muongozo wa kisheria wa usimamizi wa mazingira katika visiwa vya Zanzibar. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo zinapelekea sheria hiyo kufutwa na kutengeneza sheria mpya. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa vifungu ambavyoutekelezaji wake umekuwa mgumu. Kwa mfano, kifungu cha 9 cha sheria hiyo kinataka kuanzishwa kwa Kamati Maalum ya Mazingira ya Baraza la Mapinduzi kuwa ndio chombo cha mwisho cha maamuzi kwa masuala ya mazingira, jambo ambalo utekelezaji wake uko kinyume na utaratibu.

2. Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2013 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilizindua sera mpya ya mazingira kufuatia kubadilishwa kwa sera ya mazingira ya mwaka 1992. Sera hiyo inatoa muongozo wa kutayarishwa kwa sheria mpya ya mazingira na kufutwa sheria iliyopo ya mwaka 1996 ili kwenda sambamba na hoja za kimazingira zilizoainishwa kwenye sera hiyo mpya.

3. Mhe. Mwenyekiti, haja ya kutenganisha shughuli za kiutekelezaji na uzingatiaji wa sheria na kiusimamizi wa shughuli za kimazingira kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira uliopo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala la mazingira ni suala mtambuka ni wazi kuwa mapendekezo ya mswada huu yatasaidia uhifadhi na usimamizi wa mazingira Zanzibar na hivyo kusaidia kupatikana kwa ufanisi katika kufikia malengo ya sera ya mazingira ya mwaka 2013 na sera nyengine mbali mbali zinazoambatana na mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kufutwa kwa sheria ya mazingira iliyopo hivi sasa na kuwekwa sheria mpya ya mazingira kutasaidia kuondoa kasoro zilizomo kwenye sheria hiyo na kuongeza ufanisi wa utekelezaji na uzingatiaji wa sheria kwa ajili ya kufikia usimamizi endelevu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015 una jumla ya sehemu kumi na sita na vifungu 87 kama ifuatavyo:

Sehemu ya Kwanza: Sehemu hii ya Mswada wa Sheria inahusu utangulizi na ina vifungu viwili ambavyo ni jina fupi na kuanza kutumika na ufafanuzi wa maneno yaliyotumika kwenye sheria hii.

Sehemu ya Pili: Sehemu hii inahusu majukumu ya jumla ya kimazingira yenye vifungu vinne ambavyo ni kifungu cha tatu hadi kifungu cha sita ambavyo ni jukumu la kulinda mazingira, usimamizi wa mazingira katika mipango ya maendeleo, haki na wajibu wa kuwa na mazingira bora, safi na salama na misingi ya usimamizi wa mazingira.

Sehemu ya Tatu: Sehemu hii inahusu utawala na muundo wa kitaasisi. Sehemu hii ina vifungu 17 ambavyo vimeanzia kifungu cha saba hadi kifungu cha 23 vinavyohusu uanzishaji wa Kamati ya ushauri wa mazingira, muundo wa Kamati ya ushauri wa mazingira, kazi za Kamati ya ushauri wa mazingira, mikutano na akidi ya Kamati ya ushauri wa mazingira, uwezo na kazi za waziri, uanzishaji wa mamlaka ya usimamizi wa mazingira, muundo na uteuzi wa Wajumbe wa Bodi, muda wa kutumikia afisi kwa Wajumbe, kazi za bodi, vikao vya bodi, maamuzi ya bodi, Katibu wa Bodi, uteuzi na uajiri, kazi za mamlaka na uwezo wa mamlaka.

Sehemu ya Nne: Sehemu hii inahusu tahadhari ya kimazingira ambayo itakuwa na kifungu kimoja cha 24 kinachohusu tahadhari ya kimazingira.

Sehemu ya Tano: Sehemu hii inahusu vitengo vya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambayo ina vifungu viwili, kifungu cha 25 na kifungu cha 26 vinavyohusu uanzishaji wa vitengo vya mazingira na mabadiliko ya tabianchi na kazi za vitengo vya mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Sehemu ya Sita: Sehemu hii inahusu ukanda wa pwani wa Zanzibar ambayo ina vifungu viwili, kuanzia kifungu cha 27 hadi cha 28 ambavyo vinahusiana na eneo la ukanda wa pwani la Zanzibar na uanzishaji wa ukanda maalum wa pwani.

Sehemu ya Saba: Sehemu hii inahusu usimamizi wa maliasili zisizorejesheka yenye jumla ya vifungu saba kuanzia kifungu cha 29 hadi cha 36. Vifungu vinahusu uanzishwaji wa Kamati ya pamoja ya usimamizi wa maliasili zisizorejesheka, muundo wa Kamati ya pamoja ya usimamizi, kazi za Kamati ya pamoja ya usimamizi wa maliasili zisizorejesheka, akidi ya vikao vya Kamati ya pamoja ya usimamizi, kibali cha maliasili zisizorejesheka, jukumu la kuendeleza eneo lililochimbwa, kumbukumbu za maliasili zisizorejesheka na katazo la mchanga wa ufukwe na fungu.

Sehemu ya Nane: Sehemu hii inahusu elimu ya mazingira na utafiti yenye vifungu viwili, kuanzia kifungu cha 37 hadi cha 38 vinavyozungumzia upatikanaji wa taarifa za kimazingira na utafiti wa mazingira.

Sehemu ya Tisa: Sehemu hii inahusu tathmini ya athari za kimazingira na kijamii ambayo ina jumla ya vifungu tisa kuanzia kifungu cha 39 hadi 47. Vifungu hivi vinaelezea mahitaji ya tathmini ya athari za kimazingira, vigezo vya kuzingatia kwa shughuli zinazohitaji kufanyiwa tathmini ya athari za kimazingira, utambuzi wa kampuni na wataalamu wa kufanya tathmini ya athari za kimazingira, kusikiliza maoni ya jamii, ufuatiliaji, taarifa zinazohitajika, ripoti ya kimazingira, ukaguzi wa kimazingira na nani anapaswa kugharamikia tathmini za athari za kimazingira.

Sehemu ya Kumi: Sehemu hii inahusu mkakati wa tathmini za kimazingira na ina vifungu viwili ambavyo ni kifungu cha 48 na 49 vinavyohusu mkakati wa tathmini za kimazingira pamoja na majukumu ya Mkurugenzi wa Mazingira, juu ya utekelezaji wa mkakati wa tathmini za kimazingira.

Sehemu ya Kumi na Moja: Sehemu hii inahusu uzuwiwaji wa uchafuzi wa mazingira na usimamizi wa taka. Sehemu hii ina jumla ya vifungu 11 kuanzia kifungu cha 50 hadi cha 60 vinavyohusiana na viwango vya kimazingira, katazo la uchafuzi, katazo la kutupa taka kwenye eneo la bahari, usimamizi wa taka na maji machafu, katazo la kuharibu au kuangamiza bidhaa zisizofaa kwa matumizi, ufuatiliaji na ukaguzi, taka za hatari, vitu vya hatari, taka za hospitali, utafutaji, uchimbaji au usafirishaji wa mafuta au gesi na umwagikaji wa mafuta au uvujaji wa gesi.

Sehemu ya Kumi na Mbili: Sehemu hii inahusu uhifadhi wa bioanuwai na usimamizi wa vyanzo vya maji. Sehemu hii ina jumla ya vifungu vitano kuanzia kifungu cha 61 hadi cha 65 vinavyohusu kutangazwa maeneo ya hifadhi, usimamizi wa eneo la hifadhi, miongozo ya uhifadhi wa bioanuwai, katazo la bioanuwai na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Sehemu ya Kumi na Tatu: Sehemu hii inahusu usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi ambayo ina vifungu vinne vya 66 hadi 69 na vifungu vinataja taasisi za maana ya kusimamia mabadiliko ya tabianchi, uanzishaji wa Kamati za mabadiliko ya tabianchi, muundo na kazi ya Kamati ya uongozi ya mabadiliko ya tabianchi na muundo na kazi ya Kamati ya kitaalamu ya mabadiliko ya tabianchi.

Sehemu ya Kumi na Nne: Sehemu hii inaelezea vifungu vya fedha na ina jumla ya vifungu vitano vya 70 na 74 ambavyo vinaelezea fedha za mamlaka vyanzo vya fedha za mamlaka, matumizi ya fedha na mapato ya mamlaka, kuanzishwa kwa mfuko wa mazingira na matumizi za mfuko wa mazingira.

Sehemu ya 15: Sehemu hii inahusu makosa na adhabu na ina jumla ya vifungu 7, kuanzia kifungu cha 75 hadi 81 ambavyo vinaelezea makosa yanayohusiana na Afisa mwenye mamlaka, makosa yanayohusiana na kushindwa kutii amri ya kusitisha, makosa yanayohukumiwa nje ya Mahakama, makosa yanayohusiana na kurudia au kuendelea kutenda kosa, makosa yanayohusiana na jaribio la kutenda kosa, adhabu za jumla na vifungu vya ujumla vinavyohusiana na adhabu.

Sehemu ya 16: Sehemu hii inahusu masharti mengineyo na ina jumla ya vifungu sita, kuanzia kifungu cha 82 hadi 87 vinavyoelezea uteuzi na uwezo wa Afisa mwenye mamlaka, kinga, muendesha mashtaka wa mazingira, uwezo wa waziri kuzuia, uwezo wa waziri kutunga Kanuni na kufuta na kubakiza.

Hitimisho: Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waupokee, waujadili na hatimae waupitishe mswada huu kuwa sheria ili tuweze kulinda na kuhifadhi mazingira yetu kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu na afya zetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya kusimamia Afisi ya viongozi wakuu wa kitaifa, naomba kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na mswada wa sheria ya kufuta sheria ya usimamizi wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu namba 2 ya mwaka 1996 na kuweka baada yake masharti bora ya kuhifadhi kulinda na kusimamia mazingira ya Zanzibar na mambo mengineyo nayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kufika hapa na kuweza kukutana mbele ya Baraza lako Tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo na ustawi wa nchi yetu pamoja na watu wake.

Mswada huu ulio mbele yetu, Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 2 ya mwaka 1996 na kuweka badala yake masharti bora ya kuhifadhi, kulinda na kusimamia mazingira hapa Zanzibar umeamuliwa na makusudi na serikali hapa Barazani ili kuweza kuweka mazingira mazuri ya kuhifadhi mazingira kwa nchi yetu.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuwasilisha kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, pia, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Kamati, kuishukuru kwa dhati serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kuweza kuona umuhimu wa kuleta mswada mbele ya Baraza ili uweze kujadiliwa na kupitishwa na kuweza kufikiwa lengo lililokusudiwa la kuwa na sheria madhubuti itakayoweza kusaidia kupunguza, kuzuia na pia kukabiliana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika visiwa vyetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya utangulizi huo Kamati yangu kwa mara nyengine inapongeza hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kutokana na umuhimu wa mswada huu utasaidia sana kupunguza changamoto na athari zinazoikabili jamii na nchi yetu kutokana na shughuli mbali mbali zinazofanywa na binaadamu ambazo kwa namna moja ama nyengine huchangia katika kuharibu mkubwa wa mazingira katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipokuwa tukiujadili na kuupitia mswada huu ambapo waliujadili bila kuchoka kutwa nzima ili kuhakikisha kwamba lengo la mswada huu linafikiwa na hatimaye nchi yetu inakuwa na sheria madhubuti ya kuzuia na kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mawazo na mapendekezo yao yamewezesha mimi leo hii kufika hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu na hatimaye kupitishwa kwa ajili ya kufikiwa lengo lililokusudiwa na serikali kwa maslahi ya nchi yetu.

Naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama hawa wafuatao:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
5. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Mohamed - Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
9. Ndg. Makame Salim Ali - Katibu

Hawa kwa kiasi fulani wamesaidia sana kuratibu haya maudhui yote tulipokuwa tukipitia mswada ule.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa napenda kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya Mswada huu uliopo mbele yetu kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, maoni hayo ya Kamati yamejikita zaidi katika kuuboresha mswada wenyewe, lakini pia kusawazisha baadhi ya makosa ya kiuandishi na uchapaji kama ifuatavyo:

Kama tulivyosema pale awali kwamba Kamati yetu iliridhia mswada huu hasa kutokana na umuhimu wake wa Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nikianzia na kifungu cha 10 (1) tumeongeza neno "kikawaida" kabla ya mwaka na inaweza kukutana kwa dharura pale itakapoonekana inafaa.

Sababu ya kuongezwa kwa maneno hayo ni kuipa nafasi Kamati kisheria kuweza kukutana wakati wowote pale itakapolazimu kufanya hivyo, vyenginevyo kukiacha kifungu hicho kama kilivyo kwa kuweka mikutano minne tu kwa mwaka hasa kwa umuhimu na unyeti wa kazi yenyewe ya uhifadhi ya mazingira ndio maana Kamati yangu ikaonelea ni vyema kuongeza kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu cha kumi cha mswaada ili kutoa nafasi kwa Kamati kuweza kukutana vikao vya dharura.

Mhe. Mwenyekiti, hili tuliweza kuliweka tulijadiliana sana kwamba wenzetu wizara waliona kwamba Kamati kuweza kukutana mara nne halafu tukaweka na vikao vya dharura, ingeliweza labda kutumia nafasi ile kuweka labda vikao ambavyo pengine visingekuwa na tija sana matokezeo yake ikatokezea matumizi mabaya ya fedha ya umma.

Lakini Kamati yangu iliona kwamba umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na ile Kamati wakati wowote inapotokezea matatizo mbali mbali hasa ya uchafuzi au uharibifu wa mazingira, basi ni busara waweze kukaa na kumshauri waziri kufanya kazi au kufanya maamuzi yanayofaa kwa wakati muafaka hasa kuzingatia kwamba katika sheria hii kuna chombo ambacho kitaundwa chombo ambacho kitakuwa na nguvu kubwa.

Kwa hivyo, wakati mwengine nguvu vya chombo kile kinaweza kikapelekea baadhi ya athari ya maeneo mengine. Kwa hiyo, hapa ile Kamati itakuwa na nafasi ya kumshauri waziri kwa jambo lolote ambalo wanahisi waziri anaweza akatoa maelekezo.

Kwa hiyo, ndio maana Kamati yangu haikuona kwamba labda hapa kunaweza kukatokezea matumizi tu mabaya ya fedha za umma, lakini tunaamini matumizi haya yatakuwa zaidi ya kumsaidia Mhe. Waziri ili maamuzi yatakayofanywa na ile taasisi basi yaweze kuwa ni maamuzi ya busara ambayo hayatoathiri taratibu nyengine. Mhe. Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo naendelea kifungu cha 24 (3).

Kifungu cha 24 (3), Kamati yangu inapendekezwa kushushwa kwa kiwango cha chini cha adhabu kutoka milioni kumi na kuwa milioni mbili na pia kuongezwa kwa kiwango cha juu cha adhabu kutoka milioni mia moja hadi kufikia milioni mia tano.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi vile vile nitaomba nitoe ufafanuzi kwa nini tuliomba kwamba kile kiwango ambacho kiliwekwa mwanzo cha adhabu kutoka milioni kumi hadi milioni mia moja na sisi tukashusha tukasema na sisi adhabu inaze milioni mbili hadi milioni mia tano na hii sababu kwamba katika ukiukaji wa masharti ya mazingira sio lazima kwamba labda taasisi au wawekezaji wenye uwezo mkubwa tu ndio ambao wataweza kukiuka hizi taratibu za mazingira.

Lakini hata wananchi wetu wa kawaida wakati mwengine wanapochoma mwitu pengine kusafisha mashamba yao inawezekana ikatokezea uharibifu mkubwa wa mazingira ambao kwa ile faini iliyowekwa ya milioni kumi basi wananchi hawa wanaweza wakaozea jela kwa kushindwa kuweza kulipa faini hizi.

Sasa tukasema kwamba kwa kuwa kutakuwa na uwekezaji mkubwa na uwekezaji mdogo basi ni busara hata hizi faini zijaribu kuangalia wale wahusika wote ambao watakuja kuguswa na sheria hii. Kwa hiyo, ndio maana tukasema basi kwa wakulima wa kawaida au kwa wananchi wa kawaida faini ya shilingi milioni mbili wanaweza wakaja kuimudu kuilipa, lakini vile vile kwa wale wawekezaji wakubwa kwa kuwa Hakimu au Jaji atakuwa amepewa mamlaka ya kuweza kuamua ni faini gani aweze kuitimua aidha ile ya chini au ile ya juu kabisa au ya kati na kati kwa kuangalia lile kosa ambalo lililotolezea, vyenginevyo tunaweza tukamfunga hapa Hakimu kwamba akaja akatoa adhabu kubwa ambayo sheria haikumpa mamlaka ya kuweza kupunguza adhabu ile.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndiyo moja ya sababu ya Kamati yangu ikaleta pendekezo hili na zaidi inalenga katika kuweza kutoa adhabu kwa watu wote kulingana na uwezo wao na ukubwa wao wa makosa yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 34 (5), kinachoruhusu adhabu Kamati inapendekeza kuongezwa kwa adhabu hiyo kutoka milioni kwani Kamati inaona ni ndogo na inaweza kuchochea kwa makampuni makubwa kuweza kufanya uharibifu wa mazingira kwa makusudi. Hivyo, inashauri kuongezwa na kuwa adhabu hiyo iliyowekwa katika Mswada na kuweka adhabu ambayo inatisha kidogo ili sheria isije ikakiukwa kwa makusudi na hasa kwa wale wawekezaji ambao wanauwezo mkubwa wa kuona labda adhabu iliyokuwepo labda ni ndogo. Hasa kwa kuzingatia uchumi ambao unaotarajiwa hasa wa Gesi na Mafuta uharibifu wake wa mazingira utakua mkubwa, kwa hiyo, ni vyema kuweka tahadhari mapema kisheria katika kuhifadhi na kulinda mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 14(3), vile vile, tunashauri kukirekebisha ili kuweza kuifanya mamlaka kuwa ni chombo chenye kujitegemea katika shughuli zake chenye uwezo wa kushtaki na kushtakiwa pamoja na kuwa na muhuri wake kama zilivyo mamlaka nyengine zinazojitegemea, yaani *Body Corporate.*

Vile vile, Mhe Mwenyekiti, kifungu cha 58 kinachohusu Taka za Hospitali. Kamati yangu inashauri kwamba kuwepo na utaratibu mzuri hasa kwa hospitali binafsi ili kuweza kuondosha usumbufu wowote ule unaoweza kujitokeza.

Aidha katika eneo hili pia Kamati yangu inashauri Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba inatekeleza wajibu wake wa kimazingira na kisheria katika kuangamiza taka zinazozalishwa kutokana na shughuli zao za kila siku, kwani hata na wao wakati mwingine hasa katika Hospitali ya Mnazimmoja huwa wanatupa taka ovyo kwa upande wa Baharini, jambo ambalo ni uharibifu wa mazingira na kawaida ya Sheria huwa haibagui wizara, mtu binafsi au taasisi katika kufuata Sheria.

Kwa hiyo, hapa tunatoa wito kwa Hospitali yetu kuu ya Mnazimmoja, lakini vile vile na Hospitali nyengine hata taasisi zinazotoa taaluma au zinzotoa elimu katika nyanja ya afya kuhakikisha kwamba zile takataka zao au yale mabaki yao, yaani masalia yao wanayahifadhi vizuri kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tunaweza kuvuta kumbukumbu kwa wenzetu wa Tanzania Bara katika miezi ya hivi karibuni kulitokea kadhia kubwa ambayo kuna viungo vya binaadamu vilikwenda kutupwa katika jaa la kawaida kinyume na utaratibu na ikaleta taharuki kubwa sana kwa wananchi kwamba wakafikiria kwamba labda watu wale pengine walinyongwa au waliuliwa na viungo vyao vikenda kutelekezwa. Lakini kumbe vilikuwa ni viungo ambavyo vinafanyiwa mafunzo ya vitendo katika vyuo mbali mbali vya taaluma ya afya.

Kwa hiyo, ili kuepukana na suala kama lile kwa hapa Zanzibar, basi sheria hii inalazimisha kwamba kuwe na maeneo maalum ya uhifadhi au utupaji wa taka taka kama zile zisizofaa hasa za kihospitali.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 73 (1), Kamati imefuta maneno "Sheria ya Utumishi wa Umma" na badala yake kuweka Sheria ya Fedha za Umma (*Public Finance Act)* ya 2005 kifungu 11 (1), (2) hadi (5) kinachozungumzia *Special Fund,* yaani kuanzishwa kwa mifuko maalum kwani ndiyo inayohusiana na Uanzishwaji wa Mifuko ya Umma. Hapa katika Mswada ilielezewa kwamba katika sheria ya Utumishi wa Umma, lakini Kamati baada ya kuangalia na kimsingi tulikubaliana na wizara kwamba ile Sheria ilikuwa ni *Public Finance Act*.

Kwa hiyo, aidha kifungu cha 82 (3), kuhusu kutangazwa kwa Afisa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Kamati inapenda kutoa angalizo kwamba kipengele hiki kiangaliwe vizuri zaidi na kwa umakini mkubwa ili kuepusha upotevu wa muda, kwani uzoefu unaonyesha Afisa anaweza kuteuliwa na akatangazwa na sheria inaelekeza kwamba baada ya kuteuliwa lazima litoke tangazo kwenye gazeti la Serikali, jambo ambalo huwa linapita muda mrefu lakini baada ya kutangazwa huchukua muda mrefu kabla ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Kwa hivyo, uteuzi ule unakuwa na utata wa kisheria. Kwa hivyo, ndiyo maana tukajaribu kutoa angalizo kwa upande wa Serikali hasa baada ya Afisa kutangazwa basi Gazeti Rasmi la Serikali lisichelewe kuweza kuchapisha nafasi ile.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu vile vile inaipongeza Serikali kwa kuleta Mswada huu ingawa umeletwa kwa Hati ya Dharura jambo ambalo limeikosesha Kamati kupata muda wa kutosha wa kuzipitia sheria za nchi mbali mbali, pia, kuweza kujifunza kwa wenzetu ambao wanazo sheria kama hizi au sheria kama hii ya kwetu na kuona changamoto za utekelezaji wa sheria kama hii. Kwani kwa kawaida kwa kuwa na sheria nzuri ni jambo moja lakini kuweza kuzitekeleza, hilo ni suala jengine.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoshuhudia hapa Zanzibar tumekuwa na sheria nyingi nzuri, lakini tunakwama katika utekelezaji wa sheria hizo, jambo ambalo linavunja moyo sana wananchi na hata sisi tunaotunga sheria hizo na kupelekea kuonekana kwamba sisi tunapoteza fedha za umma kwa kutunga mambo ambayo hayatekelezeki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mtindo huu uliozoeleka hapa Zanzibar kwa kutunga sheria ambazo sisi tunazozipitisha bila ya kujifunza na changamoto, tukiwa hatuna uelewa mzuri na sheria hizo, jambo ambalo baada ya utekelezaji huo ndiyo huona matatizo katika utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mapungufu yote hayo yaliopo baada ya kuona umuhimu mkubwa wa Serikali kuleta sheria hii, bado kuna umuhimu mkubwa wa Serikali kuleta hii, kwani hali ya uharibifu wa mazingira imekuwa kubwa hapa duniani na hapa Zanzibar kwa ujumla na kama Serikali au kama hatukuchukua hatua za haraka basi tunaweza tukajikuta tupo katika hali mbaya sana ya kimaisha, kwani nchi yetu ni visiwa na tupo katika maeneo hatari, aidha ya visiwa vyetu kuliwa na bahari au kuweza kukosa kuvuna mazao katika mashamba yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba hivi sasa tunayo Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira lakini imekuwa na ugumu katika utekelezaji wake, kwani kuna baadhi ya makosa yaliyotajwa katika sheria hiyo, kwani yamekosa adhabu katika utekelezaji wake. Kwani taasisi iliyopewa mamlaka ya kuhifadhi mazingira, haikupewa meno ya kutoa adhabu kwa aliyekosa, jambo ambalo ilikuwa ni kikwazo katika utekelezaji wa sheria hiyo lakini sheria hii imekuja kusawazisha kasoro hii.

Mhe. Mwenyekiti, hali ya Zanzibar kwa hivi sasa siyo nzuri kimazingira, kwani kuna maeneo mengi ambayo kwa muda mrefu wananchi walikuwa wakilima mazao, ikiwemo mpunga, migomba, mihogo na kadhalika. Kwa hivi sasa maeneo hayo yameshavamiwa na maji ya bahari na wananchi hawawezi tena kuyatumia. Kwa maana hiyo tayari

bahari imeshaanza kula visiwa vyetu na kuna maeneo mengine kwa mfano Maisara kuelekea Ngazi Mia kuna maeneo tukiyatumia kwa ajili ya kuyafanyia mazoezi kwa sasa hivi wakati maji yakijaa basi hatuwezi tena kupita kwani maji ya bahari yashavamia maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Kisiwa Paza kule Pemba, tayari kuna sehemu kubwa ambayo hapo mwanzo wananchi walikuwa wakilima mazao ambayo ni sehemu ya mashamba yao, kwa hivi sasa tayari yameshavamiwa na maji ya bahari na hayawezi tena kutumika kwa kilimo.

Hiyo ni baadhi tu ya mifano midogo ambayo athari za mazingira ambayo kwa hivi sasa yamekuwa yakikaribisha umaskini katika jamii kutokana na uharibifu wa mazingira, kwani yale maeneo waliyokuwa wakitumia riski za kukidhi mahitaji yao, wao na familia kwa hivi sasa hawawezi tena kuyatumia maeneo hayo na huo ni mfano mmoja tu, bali kuna maeneo mengi zaidi ya 40 katika Kisiwa cha Pemba yameshavamiwa na maji ya bahari na hayatumiki tena na wananchi walivyokuwa wakiyatumia mwanzo maeneo hayo.

Na suala hili limekuwa likipelekea kuongeza umaskini na wala hawana pahala pengine mbadala ili kuweza kulima na kupata riski zao na familia zao.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kupitisha sheria hii, Kamati yangu inaiomba sana Serikali kufanya tathmini ya athari za uharibifu wa mazingira ulivyoathiri wananchi kwa yale maeneo yao yaliyochukuliwa na bahari au yaliyovamiwa na bahari, basi Serikali kuweza kuwafidia kwa kuwapa mashamba ya Serikali ili kuweza kuendeleza kilimo na kuweza kujikimu na familia zao, kwani kwa hivi sasa wamekosa maeneo ya kulima.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali inayoendelea kwa kasi ya kuvamia kwa maji ya bahari katika maeneo mbali mbali ya kilimo, Kamati yangu inaitaka Serikali kufanya tathmini ya kina ili kujua hali hiyo na kuweza kuandaa mkakati maalum wa kuweza kudhibiti wa hali hiyo kwa yale maeneo ambayo yanaweza kurejesheka na kuyarejesha katika hali iliyokuwa mwanzo ili yaweze kutumika kwa kilimo kama awali.

Mhe. Mwenyekiti, ukiacha maeneo yanayoendelea kuliwa na bahari, tatizo jengine la uharibifu wa mazingira ni uchimbaji ovyo wa mchanga ambapo kuna baadhi ya watu aidha kwa tamaa zao au kwa kutokujua wanachokifanya ni kuchimba bila ya kufuata taratibu na vigezo au ushauri wa Idara ya Misitu au Mazingira. Lakini Sehemu ya Saba ya Mswada inazungumzia suala la udhibiti wa mali asili zisizorejesheka, itasaidia sana kudhibiti hali hii ili isijirejee tena.

Mhe. Mwenyekiti, kitu cha kusitisha zaidi ni kuwa hata miradi mikubwa inayofanywa na Serikali ikiwemo ujenzi wa barabara ni miongoni mwa kati ya miradi inayoongoza kwa kukiuka kwa makusudi na kutokufuata masharti ya uchimbaji wa kifusi na urejeshaji wa ardhi katika hali nzuri ya mwanzo. Lakini kupitia sheria hii na mamlaka (ZEMA) itakayoundwa basi itakuwa na nguvu za kisheria za kumchukulia hatua kali mtu au taasisi yoyote itakayokiuka masharti ya uhifadhi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mswada huu unaoanzisha chombo cha ZEMA ambao kwa wenzetu kule Tanzania Bara ni NEMC. Chombo hiki kama kitafanya kazi zake vizuri basi nchi yetu itayarejea katika hali yake ya kawaida ya kimazingira, lakini chombo hichi kiwe na nguvu, wapewe uwezo wa kufanya kazi bila ya kuingiliwa na wakubwa, hapo wataweza kufanya kazi vizuri kama wenziwao NEMC kule Tanzania Bara, kwani waharibifu wakubwa wa mazingira, asilimia kubwa huwa ni watu wenye uwezo mkubwa wa fedha au wakubwa wenye sauti katika nchi, jambo ambalo hupelekea chombo kama hichi kuingiliwa katika kazi zao na kutoweza kufanya kazi zao kwa ufanisi uliokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumalizia hotuba yangu, napenda sana kuipongeza Serikali kwa kuleta sheria hii, lakini naomba baada ya wananchi kuipitisha Katiba mpya inayopendekezwa ambayo itatoa nafasi kwa Zanzibar kuanza uzalishaji wa mafuta na gesi ambao utakuwa ni uchumi mkubwa na pia wenye uharibifu mkubwa wa mazingira, basi tutaiomba Serikali iandae sera madhubuti mpya ya mafuta na gesi, pia iletwe sheria nyengine maalum ya uhifadhi wa mazingira kwenye miradi ya gesi na mafuta.

Pia, Kamati zako za Baraza zitakazohusiana na usimamizi wa sekta hizo za nishati ya mafuta na kwa upande wa uzalishaji na usimamizi wa mazingira pamoja na Kamati itakayosimamia mikataba ya miradi hiyo, basi ni busara Kamati hizo kuzipeleka nchi mbali mbali ili kujifunza, vyenginevyo hapa tutakuja kupitisha sheria zinazoruhusu uwekezaji mkubwa bila ya kuwa na taaluma yoyote na matokeo yake kuja kujuta hapo baadae, kama yalivyowakuta

wenzetu Jamhuri ya Muungano kuhusu mikataba mibovu ya mwanzo iliyokuwepo ya madini. Kwa hivyo, Kamati yangu inatoa angalizo kwa Serikali pamoja na Afisi yetu ya Baraza kujiandaa na suala hilo mapema.

Mhe. Mwenyekiti, ni matumaini ya Kamati yangu kwamba kuwepo kwa sheria hii ni hatua nzuri ya kihistoria kwa nchi kuelekea safari ya kuvitunza na kuvihifadhi visiwa vyetu kwa miaka mingi ijayo, lakini pia, ni maandalizi mazuri kwa uchumi mkubwa tarajiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena napenda kuipongeza Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuona uzito wa suala zima hili la uharibifu wa mazingira na kuja na sheria hii madhubuti ambayo kama wote tutaitekeleza kwa pamoja na kumpa mashirikiano Mhe. Waziri, kuweza kusimamia mazingira katika nchi yetu, basi tunaamini nchi yetu itakuwa ni mfano mkubwa wa kuigwa katika uhifadhi wa mazingira na kutolewa mfano kama tunavyotolewa mfano katika kupiga vita malaria.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kuwashukuru Wajumbe wangu wote wa Kamati kwa kuweza kunipa mashirikiano kwa muda wote hadi kuweza kukamilisha ripoti ya Kamati hii. Lakini pia, mwisho kabisa naomba kumpongeza Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na timu yake kwamba siku ya jana ya mapumziko wameamua kuacha shughuli zao zote, tukashinda kutwa nzima na kuweza kuupitia Mswada huu na kuweza kukamilisha kwa mashirikiano ya pamoja bila ya migongano ya aina yoyote.*(Makofi)*

Namuomba Mhe. Waziri pamoja na timu yake kuendelea kutoa mashirikiano kwa Kamati yangu ili kuhakikisha kwamba na yale mengi ambayo tunayashauri ambayo pia katika Mswada huu, Kamati ilishauri sana Serikali kupitia Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuleta Mswada wa Sheria ambao utaipa taasisi inayohifadhi mazingira ili kuweza kusimamia vizuri mazingira. Tunamshukuru Mhe. Waziri kwa utekelezaji huo.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa uwasilishaji wako na sasa namkaribisha Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ili awe ni mchangiaji wa mwanzo kama ilivyo kawaida yake, baadae atafuta Mhe. Ali Salim Haji kama nafasi au muda ungalipo.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi niweze kukushukuru jioni ya leo hii kwa kuweza kunipa muda wa mwanzo kabisa kuutia baraka Mswada huu na hasa sisi wengine huwa Masharifu, basi kila anayekuja anakuwa anapitisha tu, kama ulivyopitisha ule Mswada wa JKU.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nisiwe mwingi wa fadhila nimshukuru sana Mhe. Waziri, ni mama mjasiri kwa kazi nzuri anayoifanya hii ya kutuleta sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, leo naomba hasa ile nafasi yangu ya ndani ya roho niweze kuisema hapa, kwa sababu jambo lolote usingoje ukasifiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jifurahishe wewe mwenyewe ndani ya nafsi yako kwa lile ambalo umeliona limekuwa zuri katika utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar - Dkt. Ali Mohammed Shein, mimi niseme nimpe pongezi kubwa sana, anapochagua Mawaziri, Makatibu, Manaibu wake na Wakurugenzi wake, hasa nasema ni *special* hii wizara, maana sisemi kwa wizara zote, hapana, kwa ile wizara ambayo ninayoiona mimi nitaweza kuisemea.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa kidogo *pending* na mimi hapa sitosema, lakini wizara hii, niseme nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, waziri wewe umpigie simu saa yoyote anapokea, unamueleza suala ambalo kwa mujibu wa kazi uliyoiona. Ninampongeza sana Mhe. Waziri wangu kwa suala hilo, yupo mstari mbele, *number one*, anakujali anajua Mheshimiwa fulani ananipigia kuna tatizo aidha wizara yangu au kuna tatizo jengine lolote, anakusikiliza kwanza. Hivi ndivyo tunavyotaka Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme sheria hii kwa asilimia 99 hata ikafika hapa na mimi ukatizame *Hansard,* nilikuwa nikipiga kelele sana na nilikuwa nikimtania rafiki yangu Mkurugenzi, humwambia siku zote huna mashiko wewe, ndiyo nyimbo yangu siku zote kwa Waziri na Katibu Mkuu ninamwambia. Lakini tizama hali halisi ilivyokuwa

wameelewa nini ninachowaambiwa na nini faida ya nchi ya Zanzibar kuwepo na chombo kama hichi cha sheria kali sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Katibu. Katibu ni mmoja ambaye niseme kuringa kwake itokezee majaliwa tu, labda siku hiyo kaona anaumwa ndiyo asipokee simu, lakini hana tabia hiyo ya kutokupokea simu, kwa mfano yupo nchi za nje unampigia simu na anapokea simu na munazungumza kiutekelezaji juu ya hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ninasema ndani ya nafsi yangu, sitomnyima Katibu huyu, lazima haki yake nimpe katika chombo hichi cha sheria kwa sababu ni moja katika sehemu ya utendaji kaweka *number one* kupokea simu, wengine hawapokei, hilo ukweli tuseme, wanaturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi naye halikadhalika mara nyingi nipo karibu naye; Mkurugenzi muhusika ambaye leo hapa aliyetuletea Mswada huu ni mara nyingi sana na kila tunaloona baya, humpigia simu kumwambia pahala fulani watu wanachota mchanga na ndiyo sababu ya kusema sheria imepitwa na wakati, anakwenda kumkamata mtu lakini anashindwa kumchukulia sheria. Lakini anabakia nimeshakwenda lakini sheria imeniambia nimuache, ndiyo anamuacha kweli.

Mhe. Mwenyekiti, leo jambo zuri limekuja hapa nimeridhika sana, nimeiweka *Hansard* vizuri. Nimejaribu kupekechua kichwa changu na nikaona ipo haja ya kuona katika wizara kutoa mapendekezo yangu, ninayo mengi na mutaona mabadiliko katika nchi hii, ikiongozwa na mimi mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninaingia katika kuchangia. Nianze na ukurasa wa 322, anasema Sehemu ya Pili, inasema;

> "Majukumu ya jumla ya kimazingira, kila mtu ana wajibu wa kulinda mazingira kwa manufaa ya vizazi na vijavyo".

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana sisi huwa tuna-*quote* sheria na ukiambiwa kutembea kuna manufaa yake. Niseme siyo sifa wala usiopendeleo lakini nimejaribu kutembelea nchi nyingi sana ambazo zipo katika mstari wa mbele katika masuala ya mazingira. Moja ni nchi ya Austria, nilienda sana na nilikaa mwezi mmoja na nusu pale na niliona jinsi gani wenzetu wanavyokuwa na sheria kali sana kuhusu suala la mazingira.

Huwezi ukakata mti, usipopanda mti na ukaulea mti, sheria hiyo ni kali na wenzetu wanaitekeleza na ndiyo maana utakuta mazingira yao hayaharibiki maisha na utashangaa sana hasa wakati wa theluji, wakati ule inaanguka theluji utashangaa sana utasema hamna miti, kumbe miti ipo imefunikwa tu barafu. Lakini inapoondoka *season* ile tizama miti inavyomea vizuri na kuzidi kustawisha.

Mhe. Mwenyekiti, je, sisi nchi yetu Mwenyezi Mungu katujaalia tuna rutba nzuri, mvua zinakuja wakati na kila kitu lakini tunashindwa kufanya hivyo vitu.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii kwa sababu binadamu wengi hawajui anawajibika vipi katika masuala ya mazingira nafsi yake na ndiyo maana hatuna tabia hata katika nyumba zetu na wengi hata wale wenye nyumba zenye fensi hawana tabia ya kupanda miti na bustani, wako wengine hawapandi hajui nini madhumuni na lengo yake.

Kumbe kama atafanya vitu vile ndani ya ile nyumba yake, ghiba yake inaridhisha na hasa wale akina mama wengine wanapenda kupanda miasumini mule na mambo mengi ya kunukia nukia. Sasa ile peke yake inaleta ghiba, harufu nzuri ndani ya nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, hayo tunakuwa tunashindwa lakini wenzetu wanakuwa lazima wanajiwekea na kuwa na bustani ambayo itakuonesha *green*, kwa sababu *green* kutizama ni moja katika fani nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili kwenye sheria hii inatufafanulia mambo mengi sana. Mimi nashukuru sana na hapa kifungu cha 4 kinasema; "Kila mtu analazimika kuhakikisha kwamba mipango ya shughuli za maendeleo zinatekelezwa kwa kuzingatia usimamizi endelevu kwa mazingira bora.

Mhe. Mwenyekiti, nayo hayo tunakosa, lakini sheria hii sasa inatwambia kuwa tuwe na mipango endelevu ya upangaji mazingira bora. Kila mtu awe na *plan* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri na hili naomba anisikilize. Nilijaribu sana kuangalia humu katika sheria yengine sijaziona, zile ambazo zitaweza kumsadia, humu mna sheria mama tu. Lakini ningeomba hizi sheria ndogo ndogo *by law* tukawagaia hawa ndugu zetu watu wa sheria, yaani tukawapa hizi na wao wakawa *strong* kuweza kutekeleza.

Nalo hili mimi sijaona sana humu nimejaribu leo mpaka kichwa kinaniuma. Mhe. Waziri au Mwanasheria itakuwa haiathiri katika sheria mama, basi tujaribu kuwatengenezea sheria nazo ndogo ndogo tuwape hawa watu wa Mashehia, ili watustawishie mazingira. Kwa sababu mazingira ndipo yanapoanzia, uchafuzi wote wa mazingira unaanzia kwenye Shehia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tuna nia ya mikakati na tuna mikakati mizuri sana kwa Sheria hii *Wallah* mimi nasema kwa Zanzibar sasa hivi tutakuwa na sisi kama wenzetu, tutafikia malengo ya wenzetu, ukweli tuseme, kama hakutiwa mtu mkono katika sheria, mimi nafikiri si kitu cha masihara sana, sheria itafanyakazi kwa mujibu wa utaratibu wake inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 326, sasa hapa ndio inakuja ile dhana yenyewe hasa na ndio maana nikasema sasa Mheshimiwa Mkurugenzi wangu atapumua sasa hivi. Kwa sababu Zanzibar hatukuwa na kitu hicho cha mamlaka na ndio maana yakawa mambo mengi sana kwa sababu unajua kuna mambo likitokezea neno tukalipa nguvu ya utekelezaji, kwa mfano tia pingu, basi ndio maana Mhe. Waziri na Katibu wangu kikawapa tabu kubwa sana, walikaa, nafikiri Mhe. Waziri hilo si lazima unijibu, lakini niseme *how many days* ambazo vikao vya kukaa mka-*discuss* namna hii na wanasheria wenu, maana yake si mchezo hichi kitu kitamu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilijaribu kutafuta na nime-*quote* kidogo sheria za nchi mbali mbali, ili nilinganishe na hii. Lakini hii niseme kuwa iko *power,* hata wenyewe ukawaambia hebu tupeni *reference* ya nchi gani mume-*quote* sheria hii, watakwambia hatuna, *experience* yao kwa sababu na wao wanatakiwa wawe na vitu vya kujenga kwa kufahamu katika akili zao, sio kila siku tu-*quote* sheria wapi na wapi. *Wallah* hilo niwape sifa kubwa .

Mhe. Mwenyekiti, tuna kitu sasa kinaitwa ZEMA, wenzetu kule Bara wana ile NEMC, wametupita tuseme kwa hatua kubwa. Lakini tutakuja kuwapita kwa hatua mbili zaidi kutokana na sheria yetu hii. Kwanza sio tatizo hata wakimbiaji kwenye *relay* utamuona mtu ametoka vizuri sana, lakini nenda kwenye *finishing* yake utakuta yule ameshapitwa zamani, utashangaa kweli kwa nini alianza mwanzo yule halafu katika umaliziaji anakutwa anapitwa.

Mhe. Mwenyekiti, hichi chombo mimi nakubaliana nacho. Naomba sana Waheshimiwa viongozi wakuu wakae pembeni kwenye chombo hichi, wasikitie mkono kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, jamadari Mhe. Hamza Hassan Juma, alisema hapa katika sheria wahaaribifu wakubwa ni viongozi, mimi nakubaliana nae na wala tusikatae kwa sababu sisi ndio tunatoka tukamwambia Mkurugenzi mwachie huyo wakati keshaharibu mazingira, ameshakata miti, ameshachafua na ameshamwaga uchafu kwenye bahari, lakini kwa kuwa mpiga debe wangu, tutakwenda kweli si kitu cha masihara Mhe. Mwenyekiti, usiweke shingo upande.

Lakini hichi kitu Waheshimiwa tuhakikishe tunaondoa mkono wetu, ndio sheria hii itatekelezeka. Laa! Tunakuja *showing off* hapa tuseme tu na tuitie kwenye *briefcase* yetu itakuwa haitekelezeki. Sasa Waheshimiwa mimi naomba sana tuipe baraka zake, tuipe nguvu zake wakubwa tuondoke tukae pembeni tuipishe sheria ifanye kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, humu mna sheria kali sana. Katika ukurasa wa 330 tahadhari tulizopewa kwa mujibu wa sheria kifungu namba 24 (1), kuna mambo ambayo yametakiwa tukio la dharura, sababu za maumbile yenyewe ya kibinaadamu au wizara wanauwezo wa kutoa na tafauti za taasisi zisimamie tena mambo ya maafa, itawajibika na ubaribifu wowote utakaotokea na mtu yeyote ambaye atakwenda kinyume na masharti kifungu kidogo cha 2 na kifungu hiki kimetenda kosa na ikapatikana hatia itakayotozwa isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukidharau kweli na nitoe mifano kwamba, watu hawasikii, watu hawaambili na watu kwa makusudi wanafanya mambo yaliokuwa si mazuri. Nitatoa mfano, sasa hivi baharini watu wengine wanamwaga *oil* tu bila ya kuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, kuna uchafuzi wa mtu kwenda kupiga bomu kwenye bahari na anachafua, kuna watu wanachukuwa nyavu ambazo hazistahiki wanaharibu machafuzi ya bahari pamoja na matumbawe na kila kitu, ukiwakataza hawataki kukatazika. Lakini kwa adhabu ya aina kama hizi kama hajatia mkono kiongozi akasema "mpiga debe wangu huyo", basi si dhani kama mtu mmoja tu akipatikanwa na akipandishwa kwenye kiriri na sheria ikamkamata akatozwa faini  za hizo fedha, hatokezei mtu yeyote kufanya kosa kama hilo hata siku moja.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 331, mimi nakubaliana nacho, kuanzishwa kitengo kitakacho husiana na mazingira ya mabadiliko na tabianchi katika wizara, mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, sheria tumeipitisha kweli, ndio hapo niliposema kuwa jamani tuangalie hata na sheria na wao kuwagaia ndogo ndogo kuanzia kwenye Serikali za Mitaa mpaka kwenye Shehia.

Kumbe nilisema kule sikufanya kosa sikubuni, sasa nilikuwa sijaona hapa, kumbe nilikuwa nimesema katika *time* ambayo inakubalika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nisikitike jambo moja, ufinyu wa bajeti na hii ndio tunayofanya udhoroteshaji wa mambo yetu yote. Hawa watakuwa wanatafuta vianzio vyao vya fedha nakubaliana nalo, kwa sababu wanangoja mpaka mtu wamkamate, haidhuru kuna mambo mengine itabidi na wao wapate asilimia, lakini asilimia ile sidhani kama itaweza kuwatosha katika bajeti yao kufanya mambo yao.

Kwa sababu wenzetu kule NEMC wana zana kamili; wana vifaa vya kiteknolojia vya kisasa, wana vifaa ambavyo wanapata *data*, wewe mwenyewe huwezi kuamini kama sasa hivi unachafua bahari au unachafua jambo jengine lolote. Sasa na hii mamlaka yetu inatakiwa ni lazima iende na *system* yenyewe, *new model* ya sheria na *new model* ya vitendea kazi. Sasa mzigo uko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, hapo ndipo pana tabu na niwahurumie hapo. Sijui kwa nini yale mambo muhimu sana vitengo vya sheria au mamlaka ambazo kwa mujibu wa sheria zinakuwa zinananihii, halafu tunaipatia bajeti wizara kidogo. Kwa kweli Mhe. Waziri ana mtihani mkubwa sana katika ofisi yake kupata bajeti yake, huko kukamilika kwake kwa tabu sana. Sasa hapa niwasikitikie. Lakini panapo uhai na uzima *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia, labda kwa mfumo huu serikali itaweza kuwaonea huruma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana nacho kifungu cha usimamizi wenye uwiano wa ukanda wa Pwani, kwa sababu ndio kisiwa chetu kimezungukwa. Lakini sasa tatizo moja linatukuta hapa, kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, bahari sasa inapenya inakuja kwenye mashamba. Kuna mambo mengine ni mambo ya Mwenyezi Mungu, lakini kuna mambo mengine ni uchafuzi wa makusudi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ya ukurasa wa 332(3), inasema;

> "Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (2) na hiki ametenda kosa na kupatikana na hatia, atatozwa shilingi milioni 5, isiyopungua shilingi milioni 10".

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo naona hii sheria ya milioni 10 na milioni 5, ningemuomba Mhe. Waziri, Mwanasheria kuweza kupandisha kidogo, kwa sababu mara nyingi sana wanaofanya machafuzi ya bahari ni wenyewe wazungu, yaani wale wawekezaji kwa makusudi. Wanatumia zile *bath zone* za 30 *mitres* wanatumia kwa makusudi wanavaa. Maana yake kuna *mitres* zile 30 za bahari ziwe *spaces,* lakini yeye mwekezaji. Twendeni kwa wawekezaji, mutakuta ndio kawekeza kajenga pale bila ya kufanya uchunguzi wowote wa mazingira.

Sasa mimi naomba sana hapa hii kwa mtu huyu, kwa sababu wenzetu NEMC wameweka *standard* zile za bei. Makosa madogo madogo wameweka kuanzia shilingi milioni 2, 3, 5, 6 na makosa makubwa wameweka kwa shilingi milioni 50. Hiyo milioni 50 ina *grade* ya kwenye bahari, uchafuzi wa *oil* wa ovyo ovyo katika mabahari, matumbawe na kuacha meli ivujishe *oil*.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sisi naomba Mhe. Mwanasheria, hapo kidogo dau dogo hili, angalau tuweke kwenye milioni 50 kwa sababu kiwango hiki kina *resist* na wenzetu, hatutoonekana waajabu kwa hapo, kwa sababu na wenzetu wameweka kiwango hicho hicho na sisi mara nyingi sana tunajaribu kukopi. Kwa hivyo, naomba tuangalie hili suala kwa sababu ukweli fukwe zinazotuzunguka tayari zimeshapata uharibifu mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika ukurasa huu ambao unaonesha hapa wa 334 wenyewe kuhusu tatizo la mchanga wa ufukwe na fungu. Mchanga unachukuliwa sana watu wanakwenda kujengea. Utakuta mtu anakuambia ooh! Mimi nataka kujengea ukuta, lakini sasa umekwenda kwenye mazingira, kwa sababu unapochimba hapa uhakikishe tayari umeacha shimo, kwa maana hiyo ikija bahari inachimbua pale tena, tayari umeshaharibu mazingira kutokana na hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naona hii kidogo, nacho hicho kifungu chake cha faini naona kidogo sana na 20 kifungu isipokuwa kwa mwaka mmoja. Kwa sababu kinachopenda kila kitendo kina adhabu yake. Lakini hii 20 kama nilivyosema haitoshi. Mpige mtu milioni 50, milioni 50 unafanya mchezo, kesho yule hatoweza kufanya tena tatizo lile.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hapa tuitizame tena. Mhe. Mwanasheria usione tabu wala haikubani wewe hii. itawabana wale wawekezaji. Kwa hivyo, naomba hii usione tabu kuchezea wino. Mpige mtu milioni 50 ili asituharibie mazingira yetu. Mchanga sasa hivi unachukuliwa mwingi sana pwani, unampiga mtu milioni 50, atakiona cha mtemakuni huko.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo pembeni imeandikwa ni "ufatiliaji" au "utuatiliaji", nafikiria itakuwa ni "ufuatiliaji", hapa uandishi kidogo katika ukurasa wa 336(43) kidogo naomba iwekwe kama ni sahihi ufuatiliaji, basi naomba kifanyiwe *correction* kidogo iwe katika hali nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuzungumza kwa jumla jumla, kwa sababu mimi ni mjumbe ambaye mule ninamoona kidogo nitie nyama kuweza kuchangia wananchi wafahamu, ili na mimi niwasaidie kuwafafanulia vizuri naomba niende hivyo na wao wanifahamu, ili niwabakishie na wenzangu waweze kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, kuna utaratibu sasa hivi wa uchimbaji wa mchanga. Mwanzo nilisema hili, sheria jamani, ee, uchimbaji wa mchanga na kwa kuwa Mkurugenzi wangu hajapewa meno, lakini humu nimeona mambo ambayo yatakayowajibika sasa hivi na ni suala ambalo tunaliingilia sana, kwa sababu leo watu wanachimba michanga mpaka kile kimea chenyewe wanakikokoa, hatari yake wakisha wanaacha hawafuatilii.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ina matobo matobo mengi hasa watengenezaji wa barabara, wakishamaliza hawafuatilii. Sasa kwa kuwa sheria hii tunayo, adhabu iweze kufuata mkondo wake. Kwa mfano, kuna shimo moja kubwa sana nilipokuwa mimi Mwenyekiti wa Mawasiliano hapo Uwanja wa Ndege, kalitizame sasa hivi hulioni, wameliondoa kabisa wamelijaza, huwezi kuamini kama kulikuwa kuna shimo ambalo tuunganishwe mimi na wewe pamoja na urefu wako, basi *Wallah* hatujafika juu.

Lakini leo Mhe. Mwenyekiti, kalitizame leo, utashangaa sana huwezi kuamini kama ukiambiwa lilikuwepo shimo lenye kina kirefu zaidi huwezi kuamini. Ina maana watu wanafanya dharau kwa makusudi, kwa kuwa wakati ule kulikuwa hakuna sheria, lakini leo sheria ipo ambayo hiyo nilikuambia kuwa mtu mmoja akikamatwa akipigwa milioni 60 au milioni 50, sidhani kama anaweza mtu kufanya ile kazi ambayo anajua jana Juma alikamatwa hapa, akapigwa faini ya milioni 50. Bado mimi hata kama kesho niendelee sawa, naona uko *stand by,* bado sijamaliza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka tuweke sheria ya jinsi gani ya uchimbaji wa mchanga, lakini sheria hiyo na kama nilivyosema sasa hivi Waheshimiwa Wajumbe tunaepukana na suala la kujiingiza katika masuala kama haya, kwa sababu kuna sheria ya maadili inakuja. Unajua unapokuwa katika Kamati hizi ndogo ndogo tunakuwa na *interest* ya jambo linaweza likakugharimu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, na sisi tupewe *by chance, just* kushirikishwa na jambo ili tutowe mawazo, kwa sababu sasa hivi kuna mchanga unachimbwa vibaya sana, mtu anaombewa achimbe shimo mara mbili katika eneo lile lile, kwa nini, anaambiwa ni mpiga debe wangu.
Mhe. Mwenyekiti, hatufiki na masuala ya upiga debe kwenye sheria.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili suala likomeshwe, kwa sababu uchafuzi umekuwa mkubwa sana, halafu watu wakishachimba hawarudishi zile ardhi zinavyotakiwa, hawapandi miti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niseme kuwa hii sheria imefika kwa wakati, mtu sasa atachimba mchanga au hachimbi mchanga, kutokana na sheria hii ambayo itafanywa.

Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, pita pale katika eneo la Baje kwenye eneo la Mhe. Ali, tizama ule ukanda wa Baje, vijana wenyewe wamejihamasisha wamepanda mikungu, nenda katizame pale sasa hivi, ile sehemu imebadilika unaona raha kabisa, wamejitolea wenyewe vijana. Kwa hivyo, tungekuwa na *system* kama ile kwa barabara zetu zote tungepanda miti kama wenzetu Bara. Kwa sababu Bara sasa hivi kila kichochoro utakuta mti.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo tunaomba sana yasaidiwe na sisi viongozi ndio maana nikasema kuwa tusaidie ili mazingira yawe katika hali nzuri, sio tuchafuwe mazingira, tusitie mikono kwenye vitu ambavyo vinaharibu mazingira. Kwa hivyo, naomba sana suala hili liangaliwe ili liweze kutusaidia kwa mujibu wa taratibu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Muda wako umekwisha Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Kwa hivyo, kesho naendelea?

**Mhe. Mwenyekiti:** Muda wako umekwisha.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. La kama kesho napewa *by chance* naendelea hakuna tatizo, kama muda umekwenda, hakuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Kesho nikija nitaendelea kuunga mkono kwa asilimia nyengine. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, muda tuliobakiwa nao ni mdogo sana, kwa hivyo, yule mtu wa pili hatoweza kuendelea tena. Kwa hivyo, tutamuweka kesho *Inshaallah* kwenye majaaliwa ili aweze kuendelea. Lakini kesho tukija tutaanza na Mhe. Ali Salum Haji, kwa sababu muda aliotumia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, umepindukia dakika zake za kawaida.

Kabla hatujaahirisha kikao chetu kuna tangazo hapa. Mhe. Mwenyekiti wa Kusimamia Viongozo Wakuu wa Kitaifa, anawaarifu viongozi wenyeviti wa Kamati zote kesho baada ya kipindi cha maswali na majibu waende katika ukumbi mkubwa, ili kuendelea na utaratibu wa kuzidi kwenda kutafakari juu ya suala la mswada wa maadili ya viongozi.

Baada ya maelezo hayo sasa, nachukua fursa hii vile vile kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano ambayo mlikuwa mmenipatia toka asubuhi hadi sasa hivi. Sasa nachukua fursa hii vile vile kuakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 27/01/2015, saa 3:00 barabara za asubuhi. Naomba kuahirisha.

*(Saa 1:38 usiku kikao kiliakhirishwa mpaka tarehe 27/01/2015 saa 3:00 za asubuhi)*